

# 3 UHAMIAJI NA WAHAMIAJI: SIFA NA MAENDELEO YA KIKANDA

## Utangulizi

Sura iliyotangulia inatoa maelezo jumla ya uhamiaji duniani, hasa kwa kurejelea idadi na mtiririko wa uhamiaji kimataifa. Vikundi mahususi vya wahamiaji - wakiwemo wafanyikazi wahamiaji, wakimbizi, waomba hifadhi na wakimbizi wa ndani (IDPs) - na pia fedha au bidhaa zinazotumwa kimataifa, zilizungumziwa. Sura ya 3 inalenga kimsingi kiwango cha kanda ili kutoa taswira ya kina zaidi ya uhamiaji, ambayo inaweka mtazamo tofauti, lakini unaosaidia, wa wahamiaji na harakati katika sehemu tofauti za ulimwengu.[1]

Tutaanzia sehemu ya kijiografia, badala ya mada, ikizingatiwa kuwa jiografia ni mojawapo ya mambo ya kimsingi yanayohimili uhamiaji leo, kama ilivyokuwa zamani. Licha ya utandawazi unaoongezeka, jiografia ni moja ya mambo muhimu zaidi yanayoongoza mielekeo ya uhamiaji na ufurushwaji. Watu wengi wanaovuka mipaka katika uhamiaji wao hufanya hivyo katika kanda zilizo jirani, wakielekea kwa nchi zilizo karibu, nchi ambazo zinaweza kufikika kwa urahisi kiusafiri, ambazo wanazifahamu vyema, na ambako inaweza kuwa rahisi sana kurudi. Kwa watu ambao wamefurushwa kutoka kwa makazi yao, kupata usalama haraka ni jambo kuu. Kwa hivyo, watu, huelekea kuhamishwa kwenda maeneo salama yaliyo karibu, iwe ni ndani ya nchi zao au kuvuka mipaka ya kimataifa.

Lengo la sura hii ni kusaidia watunga sera, wataalamu na watafiti wa uhamiaji kuelewa zaidi uhamiaji wa kimataifa duniani kote kwa kutumia mtazamo wa kijiografia kuwasilisha maelezo jumla ya uhamiaji wa kikanda. Uchambuzi ulio katika sura hii unazingatia kanda sita za ulimwengu kama inavyofafanuliwa na Umoja wa Mataifa, na kutumiwa na Idara ya Umoja wa Mataifa ya Uchumi na Masuala ya Jamii (UN DESA) na mashirika mengine:

- Afrika
- Asia
- Ulaya
- Amerika ya Kusini na Karibiani
- Kaskazini mwa Amerika
- Oceania

Kwa kila mojawapo ya kanda hizi, uchambuzi unahusisha: (a) muhtasari na majadiliano mafupi ya takwimu muhimu za uhamiaji kulingana na data iliyokusanywa na kuripotiwa na UN DESA, Kamishna Mkuu wa Wakimbizi wa Umoja wa Mataifa (UNHCR) na Kituo cha Ufuatiliaji wa Ufurushwaji wa Ndani (IDMC); na (b) maelezo mafupi ya "sifa muhimu na maendeleo" katika uhamiaji kwenye ukanda, kulingana na data anuwai, habari na uchambuzi kutoka kwa mashirika, watafiti na wachambuzi wa kimataifa.

Ili kushughulikia utofauti wa mikondo ya uhamiaji, mienendo na masuala katika kila mojawapo ya kanda sita, masimulizi ya kimaelezo ya "sifa muhimu na maendeleo ya hivi karibuni" huwasilishwa katika kiwango cha

1 Juhudi zote zinazowezekana zimefanywa ili kuhakikisha usahihi wa data iliyorejelewa katika sura hii, pamoja na kupitia uthibitishaji wa data. Hata hivyo, tunasikitika, kwa makosa yoyote ya data ambayo yanaweza kuwa yamebaki. Ingawa kwa ujumla ripoti hii hairejelei data au matukio ya baada ya Juni 2019, takwimu za idadi ya wahamiaji wa kimataifa zilizochapishwa na UN DESA tarehe 17 Septemba 2019 zimejumuishwa kwa kadri iwezekanavyo.

ukanda mdogo. Kuhusu Asia, kwa mfano, njia hii ya kupanga mambo katika mfululizo wa matukio inaruhusu uwasilishaji wa utambuzi kutoka kwa takwimu za Asia kwa jumla, ikifuatiwa na muhtasari wa habari juu ya kanda ndogo, zinazojumuisha Mashariki mwa Asia, Kusini mwa Asia, Asia ya Kusini-Mashariki, Mashariki ya Kati na Asia ya Kati. Mgawanyo wa kanda na kanda ndogo umetolewa katika kiambatisho cha A. Muhtasari huu wa kanda ndogo hutoa habari kuhusu mikondo ya uhamiaji kutoka, ndani na kwenda kwa kanda ndogo.[2] Zaidi ya hayo, umakini umewekwa kwenye sifa mahususi ambazo zinapatikana katika ukanda mdogo, kama vile uhamiaji wa wafanyikazi na fedha au bidhaa zinazotumwa kimataifa, uhamiaji usio halali, biashara haramu ya usafirishaji wa binadamu, ufurushwaji (wa ndani ya nchi na wa kimataifa) na ujumuishaji. Maelezo ya kijumla ya kanda ndogo hayakusudiwi kuwa kamili, lakini yamepangwa kuwa kielelezo cha mienendo muhimu na mabadiliko ya hivi karibuni katika uhamiaji.

Ni muhimu kutambua kwamba sura hii inatumia kama msingi wake sura ya 3 ya Ripoti ya Uhamiaji Duniani 2018, Uhamiaji na wahamiaji: Hali na maendeleo ya kikanda, kwa kutoa sasisho la takwimu na masuala ya sasa. La muhimu ni kwamba imetolewa kama sura inayojisimamia na haiwahitaji wasomaji kurejelea ripoti ya awali.[3] Mabadiliko makubwa katika miaka miwili tangu ripoti ya mwisho kuchapishwa yameonyeshwa katika sura hii, ambayo inajumuisha data na habari hadi mwisho wa Juni 2019. Mabadiliko ya hivi karibuni katika uhamiaji na ufurushwaji - kama mwendo wa watu wengi kupitia Amerika Kusini na Kati kutoka Jamuhuri ya Bolivaria ya Venezuela - yamejadiliwa, na pia ufurushwaji mkubwa wa Rohingya kutoka Jimbo la Rakhine la Myanmar katika nusu ya pili ya mwaka 2017. Sura hiyo inategemea msingi wa ushahidi uliopo, na vyanzo vimetolewa katika tanbihi na sehemu ya marejeleo. Tunawahimiza wasomaji kurejelea vyanzo vilivyotajwa katika sura hii ili kujifunza zaidi juu ya mada zinazovutia.

## Afrika[4]

Uhamiaji barani Afrika unahusisha idadi kubwa ya wahamiaji wanaohama ndani ya na kutoka ukanda huo. Kama inavyoonyeshwa kwenye kielelezo cha 1, katika mwaka wa 2019, zaidi ya Waafrika milioni 21 walikuwa wanaishi katika nchi nyingine ya Afrika, ongezeko kubwa kutoka 2015, wakati Waafrika milioni 18.5 walikadiriwa kuwa wanaishi katika ukanda huo. Idadi ya Waafrika wanaoishi katika kanda tofauti pia iliongezeka wakati huo huo, kutoka karibu milioni 17 mnamo 2015 hadi karibu milioni 19 mnamo 2019.

Kielelezo cha 1 kinaonyesha kuwa, tangu mwaka wa 2000, uhamiaji wa kimataifa katika ukanda wa Afrika umeongezeka sana. Na tangu mwaka wa 1990, idadi ya wahamiaji wa Kiafrika wanaoishi nje ya ukanda huo imeongezeka zaidi ya mara mbili, huku ongezeko la wanaoenda Ulaya likiwa kubwa zaidi. Katika mwaka wa 2019, wahamiaji wengi waliozaliwa Afrika ambao wanaishi nje ya ukanda huo walikuwa wakiishi Ulaya (milioni 10.6), Asia (milioni 4.6) na Amerika ya Kaskazini (milioni 3.2).

Moja ya mambo ya kushangaza zaidi kuhusu wahamiaji wa kimataifa barani Afrika, kama ilivyoonyeshwa katika kielelezo cha 1, ni idadi ndogo ya wahamiaji ambao walizaliwa nje ya ukanda huo na ambao wamehamia huko. Kuanzia mwaka 2015 hadi mwaka 2019, idadi ya wahamiaji waliozaliwa nje ya ukanda huo haikubadilika (karibu milioni 2), wengi wao walikuwa wanatoka Asia na Ulaya.

2 Tafadhali kumbuka kuwa kanda ndogo zinahusiana sana na mienendo ya uhamiaji na kwa hivyo zinaweza kutofautiana na zile za UN DESA. Maelezo yametolewa katika kiambatisho cha A.

3 Ili kuhakikisha, kwa kadiri inavyowezekana, kwamba sura hii inatoa maelezo jumla kamili “yanayojisimamia” juu ya uhamiaji wa kikanda katika miaka ya 2017 na 2018, tumetumia nyenzo zinazofaa zilizojumuishwa katika Ripoti ya Uhamiaji Duniani 2018 (sura ya 3), hasa zile ambazo zinatoa muktadha wa kihistoria wa matukio ya hivi karibuni na mienendo ya uhamiaji.

4 Tazama kiambatisho cha A kwa maelezo juu ya vijenzi vya Afrika.

Kielelezo cha 1. Wahamiaji kwenda, ndani ya na kutoka Afrika 1990–2019




*Chanzo:* UN DESA , 2019a.

*Maelezo:* "Wahamiaji kwenda Afrika" hurejelea wahamiaji wanaoishi katika ukanda huo (yaani Afrika) ambao walizaliwa katika moja ya kanda zingine (kwa mfano, Ulaya au Asia). "Wahamiaji ndani ya Afrika" hurejelea wahamiaji waliozaliwa katika ukanda huo (yaani Afrika) na wanaishi nje ya nchi yao ya kuzaliwa, lakini bado ndani ya ukanda wa Afrika. "Wahamiaji kutoka Afrika" hurejelea watu waliozaliwa barani Afrika ambao walikuwa wanaishi nje ya ukanda huo (kwa mfano, Ulaya au Kaskazini mwa Amerika).

Nchi nyingi za Kiafrika zimepitia mabadiliko makubwa katika wingi wa idadi ya watu katika miaka ya hivi karibuni, kama inavyoonyeshwa katika kielelezo cha 2, ambacho kinapanga kihadhi nchi 20 za juu Afrika zenye mabadiliko makubwa zaidi ya idadi ya watu kati ya 2009 na 2019. Nchi zote 20 za juu zilikuwa Afrika iliyo kusini mwa Jangwa la Sahara na kila moja ilipata ongezeko kubwa la idadi ya watu katika kipindi hiki. Nchi hizi 20 zinaonyesha mwenendo unaopatikana katika bara zima, hivi sasa Afrika ukiwa ukanda unaokua kwa kasi zaidi ulimwenguni na unaotarajiwa kuzidi watu bilioni 2 ifikapo mwaka 2050.[5] Ni muhimu kutambua kuwa mabadiliko ya kiwango kikubwa zaidi cha idadi ya watu kutoka 2009 hadi 2019 yalitokea katika nchi zilizo na idadi ndogo ya watu, kama inavyotarajiwa. Nchi zilizo na watu wengi zaidi Afrika - Nigeria, Ethiopia na Misri - haziko kati ya 20 za juu; hata hivyo, nchi zote tatu pia zilipata ongezeko la idadi ya watu.[6] Ukuaji wa idadi ya watu barani Afrika unakinzana na mabadiliko ya idadi ya watu huko Uropa, kwa mfano, ambayo

5 UN DESA, 2019b.

6 keshatajwa.

imepata ongezeko la polepole la idadi ya watu katika baadhi ya nchi na hata kupungua katika zingine katika kipindi hicho hicho.(Tazama kielelezo cha 14).

Ongezeko kubwa la uhamiaji wa kimataifa ndani ya Afrika (tazama kielelezo cha 1) limechangia ukuaji wa idadi ya watu hivi karibuni katika kiwango cha kitaifa. Ingawa uhamiaji si sababu pekee, huku viwango vya juu vya uzazi na ongezeko la miaka ya kuishi pia vikichangia,[7] ongezeko la uhamiaji wa ndani ya bara limesababisha mabadiliko ya idadi ya watu katika baadhi ya nchi. Kwa mfano, sehemu ya wahamiaji wa kimataifa kama kiwango cha idadi ya watu nchini Equatorial Guinea imeongezeka sana katika miaka ya hivi karibuni. Katika mwaka wa 2005, wahamiaji wa kimataifa walikuwa chini ya asilimia 1 ya idadi ya watu wa Equatorial Guinea; kufikia mwaka wa 2019, idadi hii ilikuwa imeongezeka hadi karibu asilimia 17. Afrika Kusini ni mfano mwingine. Katika mwaka 2005, wahamiaji wa kimataifa walikuwa asilimia 2.8 ya idadi ya watu wa Afrika Kusini; kufikia 2019, idadi hii ilikuwa imeongezeka hadi asilimia 7.

## Kielelezo cha 2. Nchi 20 za juu zilizo na mabadiliko makubwa zaidi ya kiwango cha idadi ya watu barani Afrika, 2009-2019




*Chanzo:* UN DESA, 2019c.

*Maelezo:* Ni muhimu kutambua kwamba kiwango kikubwa zaidi cha mabadiliko ya idadi ya watu kutoka 2009 hadi 2019 kina uwezekano mkubwa wa kutokea katika nchi zilizo na idadi ndogo ya watu.

Nchi za Kiafrika zilizo na idadi kubwa zaidi ya wahamiaji huwa kaskazini mwa ukanda huu. Hizi zimeonyeshwa upande wa kushoto wa kielelezo cha 3, ambapo nchi zimeorodheshwa na idadi yao jumla ya wahamiaji (mchanganyiko wa wahamiaji nchini na wahamaji kutoka nchi hiyo). Katika mwaka wa 2019, Misri ilikuwa na idadi kubwa zaidi ya watu wanaoishi nje ya nchi, ikifuatiwa na Moroko, Sudan Kusini, Somalia, Sudan na

7 keshatajwa.

Algeria. Kwa mujibu wa idadi ya wahamiaji, Afrika Kusini inabaki kuwa nchi kuu wanakokwenda wahamiaji wengi barani Afrika, ikiwa na karibu wahamiaji milioni 4 wa kimataifa wanaoishi nchini humo. Nchi zingine zilizo na idadi kubwa ya wahamiaji kama sehemu ya idadi yao yote lakini haziko kati ya 20 za juu, ni pamoja na Gabon (19%), Equatorial Guinea (18%), Ushelisheli (13%) na Libya (12%).

Kielelezo cha 3. Nchi 20 za juu zaidi za wahamiaji barani Afrika mnamo 2019




*Chanzo:* UN DESA, 2019a.

*Maelezo ya 1:* Wingi wa idadi ya watu uliotumika kukokotoa asilimia ya wahamiaji na wahamaji unategemea idadi ya wakazi wa nchi hiyo ya UN DESA, ambayo inajumuisha wazaliwa wa kigeni.

*Maelezo ya 2:* "Mhamiaji" hurejelea wahamiaji walio wazaliwa wa kigeni wanaokaa nchini humo. "Mhamaji" hurejelea watu waliozaliwa nchini humo ambao walikuwa wakiishi nje ya nchi yao ya kuzaliwa katika mwaka wa 2019.

Njia muhimu za uhamiaji ndani na kutoka Afrika zipo, nyingi ambazo zinahusiana na ukaribu wa kijiografia na uhusiano wa kihistoria, pamoja na sababu za ufurushwaji. Ukubwa wa njia za uhamiaji kutoka nchi A kwenda nchi B hupimwa kama idadi ya wahamiaji kutoka nchi A ambao walikuwa wakiishi katika nchi B katika mwaka wa 2019. Njia za uhamiaji zinawakilisha mkusanyiko wa harakati za wahamaji kwa muda mrefu na hutoa picha ya jinsi mikondo ya uhamiaji imebadilika na kuwa idadi kubwa ya wazaliwa wa kigeni katika nchi mahususi walikokwenda. Baadhi ya njia kubwa zaidi za uhamiaji zinazohusisha nchi za Kiafrika, kama inavyoonyeshwa kwenye kielelezo cha 4, ni kati ya nchi za Afrika Kaskazini kama vile Algeria, Moroko na Tunisia hadi Ufaransa,

Uhispania na Italia, kwa kiasi ikionyesha uhusiano wa baada ya ukoloni na ukaribu uliopo. Zingine, kama zile kati ya Sudan Kusini na Uganda na vilevile Somalia na Ethiopia ni matokeo ya ufurushwaji mkubwa unaotokana na migogoro. Njia muhimu za uhamiaji wa wafanyikazi kwenda nchi za Ghuba pia zipo, kama ilivyo katika hali ya Misri hadi Saudi Arabia na Milki za Kiarabu. La muhimu ni kwamba zaidi ya nusu ya njia kuu za uhamiaji zilizoonyeshwa kwenye kielelzo cha 4 zilikuwa ndani ya Afrika, huku njia ya kutoka Burkina Faso hadi nchi jirani ya Côte d'Ivoire ikiwa ni ya pili kwa ukubwa barani Afrika kwa jumla.

Kielelezo cha 4. Njia 20 kuu za uhamiaji zinazohusisha nchi za Afrika, 2019




*Chanzo:* UN DESA, 2019a.

*Maelezo:* Njia za uhamiaji zinawakilisha mkusanyiko wa harakati za wahamaji kwa muda mrefu na hutoa picha ya jinsi mikondo ya uhamiaji imebadilika na kuwa idadi kubwa ya wazaliwa wa kigeni katika nchi mahususi walikokwenda.

Ufurushwaji ndani na kutoka Afrika ni sifa kuu ya eneo hilo, kama inavyoonyeshwa katika kielelezo cha 5. Wakimbizi wengi na wanaotafuta hifadhi katika bara hili walikaribishwa katika nchi jirani za ukanda huu. Nchi 10 za juu barani Afrika, zikiwa zimeorodheshwa kihadhi kulingana na jumla ya wakimbizi na waomba hifadhi, wote wakiwa wanaishi na kutoka katika nchi fulani, wameonyeshwa kwenye sura ya 5 Sawa na mwaka wa 2017, Sudan Kusini ilitoa idadi kubwa zaidi ya wakimbizi barani Afrika katika mwaka wa 2018

(milioni 2.3), na ikashika nafasi ya tatu ulimwenguni, huku wengi wakiwa wanaishi katika nchi jirani kama Uganda. Baada ya mgogoro wa miongo kadhaa, Somalia ilitoa idadi kubwa ya pili ya wakimbizi katika ukanda huo na ya tano kwa kiwango cha juu zaidi ulimwenguni, huku wengi wakiishi nchini Kenya na Ethiopia. Wakimbizi wengine wengi wametoka Sudan, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Jamhuri ya Afrika ya Kati na Eritrea. Uganda ilibaki kuwa nchi mwenyeji yenye wakimbizi wengi zaidi katika ukanda huu, ikiwa na karibu wakimbizi milioni 1.2 wanaoishi nchini humo; wengi walikuwa kutoka Sudan Kusini na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo. Nchi nyingine zilizokuwa wenyeji wa wakimbizi wengi katika mwaka 2018 zilikuwa Sudan na Ethiopia.

Kielelezo cha 5. Nchi 10 kuu za Kiafrika kulingana na jumla ya wakimbizi na waomba hifadhi, 2018




*Chanzo:* UNHCR, n.d.

*Maelezo:* "Waliokaribishwa" hurejelea wale wakimbizi na waomba hifadhi kutoka nchi zingine ambao wanaishi katika nchi inayopokea (upande wa kulia wa kielelezo); "Nje ya nchi" hurejelea wakimbizi na waomba hifadhi wanaotoka kwa nchi hiyo ambao wako nje ya nchi yao ya asili. Nchi 10 za juu zinategemea data ya 2018 ambayo inakokotolewa kwa kuchanganya wakimbizi na waomba hifadhi ndani na kutoka nchi zingine.

Ufurushwaji mpya na mkubwa zaidi wa ndani barani Afrika katika mwaka wa 2018 ulifanyika Kusini mwa Jangwa la Sahara, huku wengi wakifurushwa kutoka kwa makazi yao na migogoro, si majanga. Hii ni tofauti na Asia, ambayo ilipitia idadi kubwa ya ufurushwaji kutoka kwa makazi yao uliosababishwa na majanga (tazama kielelezo cha 12). Ufurushwji unaotokana na migogoro ndani ya nchi ulikuwa mwingi sana nchini Ethiopia na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, ambao ulifanya matukio kama hayo kwingineko katika ukanda huu kuonekana kuwa madogo (kielelezo cha 6). Mwishoni mwa 2018, kulikuwa na visa vipya milioni

2.9 vya ufurushwaji uliotokana na migogoro nchini Ethiopia, idadi kubwa zaidi ulimwenguni, na kubwa zaidi kuliko idadi ya 2017, ambayo ilikuwa imezidi 700,000 kwa kiasi kidogo. Pamoja na hao waliofurushwa na migogoro, kulikuwa na ufurushwaji 290,000 mpya nchini Ethiopia kutokana na majanga. Katika mwaka wa 2018, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo ilikuwa na idadi kubwa ya pili ya ufurushwaji barani Afrika na ulimwenguni, huku idadi hiyo ikifikia milioni 1.8. Katika Jamuhuri ya Afrika ya Kati, ingawa kiwango cha ufurushwaji hakikuwa kibaya kama ilivyokuwa katika nchi kama Ethiopia, ulikuwa wa kiwango cha juu zaidi cha ufurushwaji wa ndani (11%). Kimsingi nchi kadhaa zilizo na idadi kubwa ya wafurushwaji wa ndani - kama vile Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Ethiopia na Somalia - pia zina wakimbizi wanaoishi pale au zinatoa idadi kubwa ya wakimbizi na waomba hifadhi (angalia kielelezo cha 5). Ni muhimu pia kutaja kwamba nchi kama Msumbiji, ambayo hivi karibuni ilipata ufurushwaji mkubwa kwa sababu ya vimbunga Idai na Kenneth, hazijajumuishwa kwenye kielelezo cha 6. Hii ni kwa sababu data iliyotumiwa inanasa tu idadi ya ufurushwaji mpya wa ndani katika mwaka wa 2018, si 2019. Hata hivyo, majadiliano kuhusu ufurushwaji kule Kusini mwa Afrika kwa sababu ya matukio yanayohusiana na hali ya hewa kama vile kimbunga Idai yanaweza kupatikana katika "Sifa muhimu na maendeleo barani Afrika" hapa chini.

### Kielelezo cha 6. Nchi 20 za juu za Kiafrika kulingana na ufurushwaji mpya wa ndani (janga na mgogoro), 2018




*Chanzo:* IDMC, n.d; UN DESA, 2017.

*Maelezo:* Neno "ufurushwaji mpya" linarejelea idadi ya harakati za ufurushwaji ambazo zilitokea katika mwaka wa 2018, si mkusanyiko wa jumla ya idadi ya IDPs unaotokana na ufurushwaji wa muda mrefu. Takwimu mpya za ufurushwaji zinajumuisha watu ambao wamefurushwa zaidi ya mara moja na hazilingani na idadi ya watu waliofurushwa katika mwaka husika.

Ukubwa wa idadi ya watu uliotumika kukokotoa asilimia ya ufurushwaji mpya unaotokana na majanga na migogoro unatokana na jumla ya idadi ya wakazi wa nchi kulingana na makadirio ya idadi ya watu ya mwaka 2017 ya UN DESA, na asilimia inatolewa kwa madhumuni ya kutoa ufafanuzi tu.

## Sifa muhimu na maendeleo barani Afrika

### *Mashariki na Kusini mwa Afrika*

**Migogoro isiyoweza kudhibitiwa kwa urahisi, vurugu za kisiasa na kijamii, na vizuizi vya ukuzaji wa amani vimesababisha kuhama kwa mamilioni katika Mashariki mwa Afrika, huku nchi nyingi katika ukanda huo zikiathiriwa.** Kwa mfano, mwishoni mwa 2018, kulikuwa na zaidi ya wakimbizi milioni 2.2 wa Sudan Kusini na karibu IDPs milioni 1.9.[8] Wakati idadi ya wakimbizi wa Sudan Kusini ilipungua kidogo, kutoka milioni 2.4 katika mwaka wa 2017, bado ilikuwa ya juu zaidi barani Afrika mnamo 2018.[9] Katika mwaka huo huo, Somalia ilikuwa asili ya karibu wakimbizi milioni 1 na ilikuwa na zaidi ya IDP milioni 2.6 waliofurushwa na migogoro na vurugu.[10] Wakati huo huo, ikiwa na IDP milioni 2.1, Ethiopia ilikuwa kati ya nchi 10 za juu zilizo na idadi kubwa zaidi ya watu waliofurushwa ndani ya nchi kutokana na migogoro na vurugu mwishoni mwa 2018.[11] Nchini Somalia, vita vya wenyewe kwa wenyewe vilivyoendelea kwa muda mrefu vimewasukuma watu kwenda nchi zingine katika ukanda huo mdogo, na pia kwenda mashariki kwa nchi kama Yemen; hata hivyo, mgogoro usioisha huko Yemen umesababisha hali isiyostahimilika, iliyolazimisha wahamiaji kurudi Mashariki mwa Afrika, huku waliowasili wakizalisha waomba hifadhi na wakimbizi wapya, waliojumuisha Wayemeni.[12] Maelfu ya Wayemeni wamekimbilia nchi za Afrika ya Mashariki kama Djibouti, ambayo, ikilinganishwa na idadi ya watu ilio nao, iliorodheshwa kati ya nchi 10 za juu zilizo wenyeji wa wakimbizi wengi ulimwenguni katika mwaka wa 2018.[13] Nchi zingine - pamoja na Uganda, Ethiopia, Kenya na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania - ziliendelea kuwa wenyeji wa idadi kubwa ya wakimbizi, hasa kutoka ukanda huo mdogo, kama ilivyofanya Sudan Kusini - licha ya mgogoro ambao umesababisha ufurushwaji wa kiwango kikubwa kutoka na ndani ya nchi hiyo.[14] Masuala changamano na yenye visababishi vingi yaliyochochea ufurushwaji na yanayozuia upatikanaji wa suluhisho yanamaanisha kwamba nchi hizi wenyeji - zikiwa baadhi ya zilizo na maendeleo duni ulimwenguni - zinaendelea kutoa hifadhi ya muda mrefu kwa sehemu ya waliofurushwa kutoka makao yao ulimwenguni isiyo uwiano.[15] Kwa kutambua changamoto ambazo nchi nyingi za Kiafrika zinakabiliwa nazo zinapokuwa wenyeji wa idadi kubwa ya watu waliokimbia makazi yao, na katika juhudi za kuonyesha uhusiano kati ya ufurushwaji, amani, usalama na mwelekeo wake wa maendeleo, Umoja wa Afrika ulitangaza mada yake kuu ya mwaka 2019 kuwa "Wakimbizi, Wanaorejea na Wakimbizi wa ndani ya Nchi: Kufikia Suluhisho za Kudumu za Ufurushwaji wa Lazima Barani Afrika".[16] Katika mwaka wa 2019, Umoja wa Afrika haulengi tu kuweka umakini zaidi kwenye changamoto za ufurushwaji barani Afrika, lakini pia unalenga kukuza mipango ya ubunifu na uthabiti ya kushughulikia vyanzo asili na kukuza suluhisho la kudumu kwa ufurushwaji barani.[17]

8 UNHCR, 2019a; IDMC, 2019.
9 UNHCR, 2018a, 2019a.
10 UNHCR, 2019a; IDMC, 2019.
11 IDMC, 2019.
12 UNHCR, 2019a; IOM, 2018a.
13 keshatajwa.
14 UNHCR, 2019a.
15 Kwa ufurushwaji wa ndani kwa ujumla, angalia pia Matriki ya Ufuatiliaji wa Ufurushwaji ya IOM, hasa kwa Burundi, Ethiopia, Kenya, Malawi, Msumbiji, Sudani Kusini, Uganda na Zimbabwe.
16 Umoja wa Afrika, 2019.
17 keshatajwa.

**Kwa muda mrefu Mashariki na Kusini mwa Afrika pamekuwa mahali pakuu walipokimbilia wahamiaji kutoka ndani ya Afrika na kanda zingine, wakati Mashariki mwa Afrika pia panazidi kuwa asili muhimu ya wafanyikazi wahamiaji wanaokwenda katika Mataifa ya Baraza la Ushirikiano wa Ghuba (GCC).**[18] Kihistoria, uhamiaji kutoka India umekuwa muhimu katika nchi kama Uganda, Kenya na Afrika Kusini,[19] wakati miaka ya hivi karibuni zimeshuhudia ongezeko la kasi katika idadi ya wafanyikazi wahamiaji wa Uchina wanaohamia nchi zilizo katika ukanda huo mdogo.[20] Kwa kuzingatia uchumi wake wa hali ya juu na utulivu wa kisiasa, Afrika Kusini pia imeshuhudia idadi kubwa ya wahamiaji katika miaka ya hivi karibuni, ikivutia wahamiaji, waomba hifadhi na wakimbizi kutoka ndani na nje ya Kusini mwa Afrika. Idadi ya wahamiaji wa kimataifa nchini Afrika Kusini iliongezeka kutoka karibu milioni 2 katika mwaka 2010 hadi zaidi ya milioni 4 katika mwaka 2019.[21] Wakati huo huo, Mashariki mwa Afrika inaendelea kushuhudia viwango vikubwa vya uhamiaji nje wa wafanyikazi, unaosababishwa na umasikini, mishahara midogo na ukosefu mkubwa wa ajira.[22] Hili linadhihirika zaidi katika idadi kubwa ya watu wa Afrika Mashariki wenye ujuzi wa chini na wenye ujuzi kiasi ambao katika miaka ya hivi karibuni wamehamia Mataifa ya GCC kwa mikataba ya kazi za muda. Hali ya kuwa Mataifa ya Ghuba yako karibu na Mashariki mwa Afrika na nafasi zao za ajira huyafanya kuwa kivutio cha kufikiwa na watu wengi wa Afrika Mashariki.[23]

**Katika Mashariki na Kusini mwa Afrika, uhamiaji wa ndani ya ukanda pia unachochewa na ongezeko la mahitaji ya wafanyikazi wenye ujuzi wa hali ya juu na wenye ujuzi mdogo.** Wakati uchumi wa nchi za Afrika Mashariki, kama Kenya na Rwanda, unazidi kukua wa mseto, mahitaji ya wafanyikazi katika tasnia ya huduma, kwa mfano, yamewavuta wafanyikazi wahamiaji kutoka nchi zingine za Afrika Mashariki, zikiwemo Uganda na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Hivi ndivyo hali ilivyo hasa kwa sekta ya teknolojia inayopanuka nchini Rwanda, ambayo inaendelea kuwavutia wafanyikazi kutoka ukanda huo mdogo.[24] Itifaki ya Soko la Pamoja la Afrika Mashariki, ambayo inaruhusu usafiri huru wa wafanyikazi, imesaidia kuwezesha uhamiaji wa wafanyikazi kote katika eneo hilo.[25] Nchi kadhaa zimeidhinisha Itifaki hiyo na tayari zingine zimefuta vibali vya kufanya kazi kwa raia wa Afrika Mashariki, na kurahisisha hali ya watu kufanya kazi popote katika ukanda huo mdogo. Wakati huo huo, uhamiaji wa ndani ya ukanda wa wafanyikazi umeimarika vyema Kusini mwa Afrika, ambapo idadi kubwa ya watu kwa kawaida wamehama kutoka nchi kama Eswatini, Lesotho, Malawi na Zimbabwe, kwenda kufanya kazi Afrika Kusini na Botswana.[26] Wakati sekta za jadi, kama vile uchimbaji madini, zinaendelea kuvutia wafanyikazi wahamiaji, sekta zingine - pamoja na fedha na teknolojia ya habari - zinazidi kuwavuta wahamiaji kwenda Afrika Kusini.[27]

**Uhamiaji Mashariki na Kusini mwa Afrika unaendelea kuhusisha idadi kubwa ya wahamiaji wasio halali, wanaotambuliwa na mtiririko wa uhamiaji mchanganyiko na unaoungwa mkono na vichocheo anuwai, pamoja na masuala ya kijamii na kiuchumi, migogoro na ukosefu wa utulivu wa kisiasa.**

---

18 Baraza la Ushirikiano wa Ghuba (GCC) ni shirika la kisiasa la kikanda ambalo linajumuisha nchi sita: Bahrain, Kuwait, Qatar, Oman, Saudi Arabia na Milki za Kiarabu.

19 Flahaux na de Haas, 2016.

20 Cook na wengine, 2016.

21 UN DESA, 2019a.

22 Manji, 2017.

23 Atong, Mayah na Odigie, 2018.

24 UNCTAD, 2018.

25 Jumuiya ya Afrika Mashariki, n.d.

26 Nshimbi na Fioramonti, 2013.

27 UNCTAD, 2018.

Magendo ya wahamiaji ni maarufu sana katika kanda ndogo zote mbili, huku watu wengi wakitumia huduma za wafanya magendo kufikia maeneo waliyokusudia. Mitandao mingi ya magendo ina makao yake katika Pembe ya Afrika, wakati nchi ambazo ni wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki - kama Kenya na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania - kwa kiasi kikubwa ni nchi za kupitia.[28] Mashariki ya Kati, Ulaya na Kusini mwa Afrika ni miongoni mwa sehemu kuu wanakokwenda wahamiaji kutoka Mashariki mwa Afrika, ambao hutumia njia kadhaa, pamoja na njia za Mashariki kuelekea Rasi ya Kiarabu na nchi zingine za Mashariki ya Kati, njia za kusini kwenda Kusini mwa Afrika, na njia za kaskazini kwenda Afrika Kaskazini, Ulaya na Amerika ya Kaskazini. Hata hivyo, njia za Pembe ya Afrika pia ni muhimu, kukiwa na idadi kubwa ya watu wanaosafiri kuelekea au ndani ya Pembe ya Afrika.[29] Kama ilivyo Mashariki mwa Afrika, uhamiaji usio halali umeenea Kusini mwa Afrika, na unahusisha wahamiaji wa ndani ya ukanda, kama vile wale wanaotoka Zimbabwe na Msumbiji, wanaohamia Afrika Kusini, na vilevile wale wanaotoka nje ya ukanda mdogo.[30] Mitandao ya magendo ya wahamiaji imeongezeka katika muda wa miongo kadhaa na imekuwa ya kupangwa na kitaaluma zaidi, kwa kuwa imekuwa vigumu zaidi kuvuka mipaka Kusini mwa Afrika.[31] Wakati idadi kubwa ya wahamiaji wanaoingizwa kimagendo Kusini mwa Afrika wanatoka katika ukanda huo mdogo, idadi kubwa pia hutoka nje ya Kusini mwa Afrika, hasa kutoka Pembe ya Afrika. Wahamiaji wengi mara nyingi hukumbana na hatari kubwa, huku wengi wakikabiliwa na vurugu na upokonywaji.[32]

**Mabadiliko ya mazingira na majanga katika Mashariki na Kusini mwa Afrika yameenea na yanaongezeka, na yanaathiri harakati za wanadamu na ufurushwaji.** Ukanda huo mdogo umekabiliwa na ongezeko la ubadilikaji wa mvua inayonyesha na matukio mengi ya ukame katika miongo ya hivi karibuni.[33] Mianzo hii ya polepole ya mabadiliko ya mazingira ina athari kubwa kwa usalama wa chakula, ikizingatiwa kuwa kilimo ni sekta kubwa ya uchumi katika Mashariki na Kusini mwa Afrika.[34] Ukame umekuwa tukio la kawaida katika nchi kama Somalia, na ni kichocheo kikuu cha ufurushwaji katika nchi hiyo. Katika mwaka wa 2018, kulikuwa na ufurushwaji mpya robo milioni nchini Somalia kwa sababu ya ukame.[35] Katika mwaka wa 2017, ufurushwaji unaotokana na ukame ulifikia zaidi ya watu 850,000 nchini Somalia.[36] Hali ya ukame imehusika na kuongezeka kwa utapiamlo, uhaba wa chakula na kuongezeka kwa ushindani wa rasilimali zilizopunguzwa tayari, hasa kati ya wakulima na wafugaji katika ukanda huo mdogo; takriban watoto milioni 1.2 nchini Somalia walikuwa na utapiamlo mkali katika mwaka wa 2017.[37] Nchi kadhaa Kusini mwa Afrika pia zilipitia ufurushwaji mkubwa kwa sababu ya hatari zinazoanza ghafla. Kuanzia Januari hadi Juni 2018, Mashariki mwa Afrika ilichangia visa vitano vikali zaidi duniani vya majangwa.[38] Na mnamo Machi 2019, Kusini mwa Afrika ilipata vimbunga viwili vilivyofuatana, Idai na Kenneth, ambavyo vilileta mvua nyingi sana na upepo, na kuacha uharibifu mwingi huko Msumbiji, Zimbabwe na Malawi. Kimbunga Idai, kilichosababisha maporomoko ya ardhi katikati mwa Msumbiji, kinachukuliwa kuwa moja ya majanga mabaya zaidi ya asili

28 UNODC, 2018.
29 IOM, 2019a.
30 Maher, 2018.
31 keshatajwa.
32 keshatajwa.
33 Climate and Development Knowledge Network, 2014a.
34 Tierney, Ummenhofer na deMenocal, 2015; USAID, n.d.
35 IDMC, 2019.
36 IOM, 2018a.
37 UN Environment, 2018a.
38 IDMC, 2018b.

yaliyotokea Kusini mwa Afrika kwa miongo mingi.[39] Kufikia Aprili, kimbunga hicho kilikuwa kimesababisha vifo vya karibu watu 600 na kuwahamisha zaidi ya watu 130,000 nchini Msumbiji pekee.[40]

**Mashambulizi ya chuki dhidi ya wageni wahamiaji na kuibuka kwa vikundi vipya vyenye silaha Kusini mwa Afrika vimechangia kuongezeka kwa ufurushwaji katika ukanda huo mdogo.** Katika kipindi cha miaka 10 iliyopita, wahamiaji katika nchi kama Afrika Kusini wamezidi kufanyiwa vurugu, na matokeo yake yamekuwa ni uharibifu wa mali, majeraha na wakati mwingine kupoteza maisha. Mashambulizi ya chuki dhidi ya wageni kote nchini, kama yale ambayo yalitokea katika mwaka wa 2008, yalifurusha maelfu ya wahamiaji na kusababisha zaidi ya vifo 60.[41] Hivi karibuni, mashambulizi ya chuki dhidi ya wageni katika mwaka wa 2018 yalisababisha vifo kadhaa, uporaji na uharibifu wa mali za raia wa kigeni; vurugu hizo zimeenea hadi mwaka 2019 na watu wengi zaidi wamekufa.[42] Mlipuko wa vurugu za chuki dhidi ya wageni ni jambo la kawaida katika miji ya Afrika Kusini na maeneo mengine jirani yaliyo maskini kiuchumi, ambapo wakazi mara nyingi huwalaumu raia wa kigeni kwa viwango vya juu vya uhalifu na upotezaji wa kazi. Katika sehemu za ukanda huo mdogo, vikundi vyenye silaha vinavyotisha jamii vinaendelea kufurusha watu kutoka kwa makazi yao. Kwa mfano, kaskazini mwa Msumbiji, kundi lenye silaha linalojulikana kama Al-Sunna wa Jama'a bado ni tishio kubwa na limewafukuza mamia ya watu kutoka nyumbani kwao.[43]

### *Afrika Magharibi na Kati*

**Uhamiaji wa ndani ya ukanda, ambao ni muhimu Afrika Magharibi na Kati, unabainishwa na mitiririko ya uhamiaji ambayo inashawishiwa na vichocheo kadhaa.** Ingawa kuna upungufu mkubwa wa data juu ya uhamaji, na ni vigumu kuthibitisha idadi sahihi, makadirio ya hivi karibuni yanaonyesha kwamba wahamiaji wengi wa kimataifa huko Afrika Magharibi na Kati huhamia ndani ya ukanda huo.[44] Uhamiaji wa ndani ya ukanda unatawala kwa sababu kadhaa, pamoja na usafiri usiohitaji viza kati ya nchi wanachama za Jumuiya ya Kiuchumi ya Nchi za Afrika Magharibi (ECOWAS), udogo wa nchi nyingi katika ukanda mdogo huo na mitandao imara kati ya makabila mengi yaliyotawanyika katika ukanda mdogo wote.[45] Muhimu zaidi ni kuwa uhamiaji wa ndani ya ukanda wa ECOWAS hutokea zaidi kwa sababu ya uhamaji wa wafanyikazi, huku kukiwa na wahamiaji wa msimu, wa muda na wa kudumu wanaohama hasa kutoka nchi kama Niger na Mali kuelekea Ghana na Côte d'Ivoire.[46] Idadi kubwa ya wafanyikazi wahamiaji wako katika sekta zenye ujuzi mdogo, ikiwa ni pamoja na kazi za nyumbani, biashara isiyo rasmi na kilimo.[47] Katika sehemu za Afrika Magharibi, wafanyikazi wa kilimo mara nyingi huhama wakati wa mavuno (Julai hadi Septemba), na vilevile katika msimu usio wa mavuno ambao unaendelea hadi Machi.[48] Baadhi ya wafanyikazi wahamiaji ni watoto, kama ilivyo katika uhamaji kati ya Côte d'Ivoire na Burkina Faso.[49] Tofauti na Afrika Magharibi, ambapo masuala

39 UNICEF, 2019.
40 IOM, 2019b.
41 Landau, 2018.
42 Amnesty International, 2018.
43 Human Rights Watch, 2018.
44 Adepoju, 2016.
45 Flahaux na de Haas, 2016.
46 Devillard, Bacchi na Noack, 2016.
47 UNCTAD, 2018.
48 ACAPS, 2018.
49 UNCTAD, 2018.

ya mazingira na uchumi ni vichocheo muhimu vya uhamiaji wa ndani ya ukanda, migogoro na ukosefu wa utulivu vimechangia kwa njia kubwa katika kuhamia nchi jirani za Afrika ya Kati.[50] Hata hivyo, uhamiaji wa wafanyikazi haukosekani Afrika ya Kati, huku Gabon, kwa mfano, ikiwa makao ya idadi kubwa ya wahamiaji wafanyikazi kutoka Afrika ya Kati wanaofanya kazi katika tasnia yake ya mafuta na mbao.[51]

**Uhamiaji usio halali bado umeenea Afrika Magharibi na Kati, ingawa makubaliano ya usafiri usio na vikwazo katika eneo hilo umewekwa ili kuwezesha uhamiaji na kupunguza uvunjaji kanuni.** Matumizi ya wafanya magendo kuvuka mipaka hata katika maeneo ya usafiri yasiyo na vikwazo kama vile ECOWAS yanaonekana pia, hasa katika hali ambazo watu hawana hati za utambulisho.[52] Hata hivyo, ni muhimu kusisitiza kwamba watu wa Afrika Magharibi wengi ambao walisafirishwa kimagendo kupitia nchi kavu huanza safari zao kama wahamiaji wa kawaida chini ya itifaki ya usafiri usio vikwazo na wanakiuka tu sheria za uhamiaji baada ya kutoka eneo la ECOWAS.[53] Zaidi ya hayo, mipaka kadhaa Afrika Magharibi inapitika kwa urahisi sana, ikiwezesha safari zisizoruhusiwa kati ya nchi, huku mipaka kadhaa ya ECOWAS ikiwa katika maeneo yasiyokuwa na utulivu wa kisiasa na yenye watu wachache, ambayo pia hayana usalama wa kutosha.[54] Kwa wahamiaji wengi wa Afrika Magharibi na Kati wanaojaribu kuvuka Bahari ya Mediterania kufika Ulaya, Niger ni nchi muhimu ya mpito na pia ni kitovu cha Magendo.[55] Uwezo dhaifu wa usimamizi wa mipaka ya Niger umezidishwa na ongezeko la mashambulizi ya vikundi vyenye silaha na vyenye msimamo mkali vinavyoendesha shughuli zake katika mipaka ya nchi hiyo. Mashambulizi mengi, pamoja na kutoka kwa Boko Haram, yanatokea hasa katika eneo la Diffa huko Niger, lililo kusini mashariki mwa nchi hiyo, inayopakana na Nigeria. Vurugu hiyo imekuwa na athari mbaya sana kwa huduma za afya na elimu, na imewafukuza maelfu ya watu kutoka nyumbani kwao.[56]

**Migogoro na vurugu zinazohusiana na machafuko ya kisiasa, mivutano ya kijamii na kikabila na msimamo mkali wa Boko Haram, vimemaanisha kuwa nchi nyingi za Afrika Magharibi na Kati zinaathiriwa na ufurushwaji wa ndani au unaovuka mipaka, ingawa ukubwa hutofautiana sana.** Kama ilivyo katika kanda ndogo zingine barani Afrika, nchi za Afrika Magharibi na Kati zina historia ndefu ya kuwa wenyeji na kuwa asili ya watu waliofurushwa makwao, mara nyingi kwa wakati mmoja. Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo ni mfano mmoja kama huo. Mwishoni mwa 2018, ilikuwa makazi ya wakimbizi zaidi ya nusu milioni, na wakati huo huo ilikuwa nchi ya asili ya wakimbizi zaidi ya 700,000, huku 300,000 kati yao wakiishi Uganda na idadi kubwa katika nchi zingine jirani, pamoja na Rwanda (77,000) na Burundi (71,000).[57] Hali ya kudumu kwa muda mrefu kwa mgogoro katika Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, ambayo inajumuisha vikundi vingi vyenye silaha, imekuwa na athari mbaya kwa nchi hiyo, na kusababisha moja ya mizozo mibaya zaidi ya kibinadamu ulimwenguni. Mwishoni mwa mwaka 2018, kulikuwa na IDP milioni 3 nchini humo, idadi ya tatu ya juu ya watu waliohamishwa kutokana na ghasia na migogoro ulimwenguni (tazama sura ya 2, kielelezo cha 11).[58] Wakati huo huo, huku maeneo makubwa ya nchi yakidhibitiwa na vikundi vyenye silaha, vita vya wenyewe kwa wenyewe katika Jamhuri ya Afrika ya Kati vilianzishwa tena

50 IOM, n.d.a.
51 keshatajwa.
52 Altai Consulting na IOM, 2015.
53 Carling, 2016.
54 keshatajwa.
55 Altai Consulting na IOM, 2015.
56 IFRC, 2018.
57 UNHCR, 2019a.
58 IDMC, 2019.

katika mwaka wa 2016 baada ya kipindi cha utulivu; mgogoro huo uliendelea hadi 2017 na 2018, ukisababisha uharibifu na kufurusha mamia ya maelfu ya watu kutoka nyumbani kwao. Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo na Jamhuri ya Afrika ya Kati zilikuwa kati ya nchi 10 za juu zilizo asili ya wakimbizi ulimwenguni katika mwaka wa 2018, huku Jamhuri ya Afrika ya Kati ikitoa karibu wakimbizi 600,000 na IDPs zaidi ya nusu milioni kutokana na migogoro.[59] Uasi wa Boko Haram, ambao ulianza katika mwaka wa 2009 huko Nigeria katika Jimbo la kaskazini la Borno, pamoja na operesheni za kupambana na uasi na mapigano ya jamii juu ya rasilimali chache, pia vimesababisha ufurushwaji mkubwa katika eneo la Ziwa Chad. Ikiwa na zaidi ya IDP milioni 2.2, Nigeria ilikuwa kati ya nchi 10 za juu zilizo na idadi kubwa zaidi ya watu waliokimbia makazi yao kwa sababu ya migogoro na vurugu kufikia mwishoni mwa 2018 (tazama sura ya 2, kielelezo cha 11).[60] Katika mwaka huo huo, kulikuwa na zaidi ya IDP 600,000 nchini Cameroon na zaidi ya 156,000 huko Niger.[61] Baadhi ya vurugu na ufurushwaji huko Afrika Magharibi huhusishwa na mgogoro kati ya wafugaji na wakulima juu ya ardhi na rasilimali, ingawa migogoro hii mara nyingi huwa na mielekeo ya kikabila na kidini pia.[62]

**Mabadiliko ya mazingira Afrika Magharibi na Kati yanaathiri jinsi binadamu anajichumia riziki na uhamaji.** Kwa mfano, ingawa matukio ya mvua katika Sahel[63] yanaongezeka polepole, yanazidi kutotabirika, na kusababisha utokeaji wa mara kwa mara wa ukame na mafuriko.[64] Huko Niger, takriban visa 40,000 vya ufurushwajiviulivyohusiana na majanga vilirekodiwa mwishoni mwa 2018, wakati huko Nigeria, kulikuwa na karibu visa 600,000 vya ufurushwaji kutokana na mafuriko katika mwaka huo huo.[65] Wakati huo huo, kuongezeka kwa kasi kwa idadi ya watu kumesababisha uzidishaji wa uzalishaji katika kilimo, uharibifu wa misitu na malisho kupita kiasi, na kuchangia uharibifu wa ardhi.[66] Licha ya kuongezeka kwa kiwango cha kilimo katika ukanda huo mdogo, uhaba wa chakula unabaki kuwa mkubwa.[67] Kwa mfano, mwishoni mwa 2018, zaidi ya watu milioni 3 waliathiriwa na uhaba wa chakula katika Bonde la Ziwa Chad.[68] Mamilioni ya watu katika Afrika Magharibi na Kati hutegemea Ziwa Chad; hata hivyo, ujazo wa ziwa umepungua kwa asilimia 90 katika eneo hilo katika miaka 40 iliyopita, kwa sababu ya kuongezeka kwa ukame na sababu zinazohusiana na wanadamu kama vile kuongezeka kwa maji yanayotumiwa katika unyunyizaji.[69] Kupungua kwa ziwa hakujaathiri tu njia za kujichumia riziki za mamilioni ya watu, lakini pia kumeathiri uhamishaji wa ng'ombe kwa misimu, na kunazidi kuwa chanzo cha mvutano na migogoro ya jamii;[70] Zaidi ya hayo, kuzorota kwa hali ya maisha, ambako kumefanya iwe vigumu kwa watu wanaoishi kando ya ziwa kuzoea hali ngumu, kumeunda mazingira bora kwa vikundi vyenye silaha kujitokeza.[71] Mabadiliko changamano na yaliyoingiliana ya kimazingira - kama vile ukame na mafuriko, utumiaji mwingi kuzidi kiasi wa rasilimali na mabadiliko ya tabianchi - ni sababu zinazochangia uhamaji kutoka vijijini hadi mijini na uhamaji wa kimzunguko ndani ya nchi tofauti na kuvuka mipaka ya ukanda huo mdogo. Uhamiaji ni mkakati mmoja unaotumiwa kuongeza

59 UNHCR, 2019a; IDMC, 2019.

60 IDMC, 2019.

61 keshatajwa.

62 UNOWAS, 2018.

63 Ukanda wa Sahel ni eneo la kiekolojia lenye ukame wa savanna ya kitropiki linalotanda katika nchi nyingi za Afrika Magharibi na Kati, ikiwa ni pamoja na Senegali, Mauritania, Mali, Burkina Faso, Niger, Nigeria, Chad na Sudan.

64 Hummel, Doevenspeck na Samimi, 2012.

65 IDMC, 2019.

66 keshatajwa.

67 UNEP, 2011.

68 European Commission, 2018a.

69 Gao et al., 2011.

70 UN Environment, 2b.

71 Rudincova, 2017.

njia za kujichumia riziki na kupunguza hatari katika Sahel ya Magharibi, hasa kutokana na mazao ya kilimo yasiyoridhisha.[72] Utafiti pia umeangazia uhusiano kati ya, kwa upande mmoja, athari za mabadiliko ya tabianchi kwa maisha ya kutegemea maliasili na ukosefu wa chakula na, kwa upande mwingine, mivutano, migogoro na uhamaji.[73]

## *Afrika Kaskazini*

**Uhamiaji wa watu wa Afrika Kaskazini kwenda Ulaya na Mataifa ya Ghuba unaendelea kuwa sifa ya mienendo ya uhamiaji wa ukanda huo mdogo, na ambao umekua kwa miongo kadhaa.** Uhamiaji wa watu wa Afrika Kaskazini kwenda nchi zilizo nje ya Afrika umekuwa, na unaendelea kuwa, wa juu sana kuliko uhamiaji kwenda nchi zingine ndani ya ukanda huo mdogo na ndani ya Afrika.[74] Mikondo miwili tofauti imeeleza uhamiaji kutoka Afrika Kaskazini: kihistoria, wahamiaji kutoka kaskazini magharibi (kama vile Moroko, Algeria na Tunisia) walihamia Ulaya, kwa sababu ya ukaribu wao wa kijiografia, makubaliano ya awali ya kuajiri wafanyikazi na uhusiano wa baada ya ukoloni,[75] wakati wale kutoka kaskazini mashariki (kama vile Misri na Sudan) mara nyingi wametafuta kazi ya muda katika nchi za GCC. Tofauti kubwa ya mapato kati ya nchi asili na wanakokwenda wahamiaji, na viwango vya juu vya ukosefu wa ajira katika Afrika Kaskazini, vinabaki kuwa vichocheo vikubwa vya uhamiaji. Kufikia mwaka 2019, karibu watu wa Afrika Kaskazini milioni 12 walikuwa wakiishi nje ya nchi zao za kuzaliwa, karibu nusu wakiwa Ulaya na milioni 3.3 wakiishi katika Mataifa ya Ghuba.[76]

**Mbali na kuwa eneo kuu la mpito la wahamiaji, Afrika Kaskazini pia ni mwenyeji wa idadi kubwa ya wahamiaji wa kimataifa, pamoja na wakimbizi.** Sudan ilikuwa na idadi kubwa zaidi ya wahamiaji wa kimataifa katika ukanda huo mdogo, zaidi ya milioni 1.2 katika mwaka wa 2019.[77] Sudan ilifuatwa na Libya, ikiwa na zaidi ya 800,000. Idadi ya wahamiaji wa kimataifa huko Misri iliongezeka kutoka 300,000 katika mwaka wa 2010 hadi zaidi ya 500,000 katika mwaka wa 2019, huku wahamiaji hasa wakitoka katika Jamuhuri ya Kiarabu ya Syria, Somalia, Sudan na Maeneo ya Palestina.[78] Wakati Moroko kwa kawaida imekuwa nchi ya wahamiaji wanaotoka nje, inazidi kuwa nchi wanakoelekea wahamiaji, pamoja na wahamiaji kutoka sehemu zingine barani Afrika, ambao hukaa huko kwa kipindi kisichojulikana wakati wanatafuta njia ya kuvuka kwenda Ulaya.[79]

**Migogoro na vurugu ndani ya Afrika Kaskazini, na katika kanda ndogo zinazoizunguka, vimechangia ufurushwaji.** Kufikia mwisho wa 2018, Sudan ilikuwa nchi ya sita kwa ukubwa wa asili ya wakimbizi ulimwenguni, ikiwa na wakimbizi karibu 700,000, ambao wengi wao waliishi katika nchi jirani za Chad, Sudan Kusini na Ethiopia.[80] Sudan pia ilikuwa na IDP takriban milioni 2.1 kwa sababu ya migogoro na vurugu.[81]

72 Hummel na Liehr, 2015.
73 UNEP, 2011.
74 Flahaux na de Haas, 2016.
75 Natter, 2014.
76 UN DESA, 2019a.
77 keshatajwa.
78 keshatajwa.
79 Reifeld, 2015.
80 UNHCR, 2019a.
81 IDMC, 2019.

Wakati huo huo, Sudan pia ni nchi inayojulikana iliyo mwenyeji wa wakimbizi, ikiwa na zaidi ya wakimbizi milioni 1 (idadi hii imekuwa zaidi ya maradufu tangu 2016), ambao wengi wao walikuwa kutoka Sudan Kusini, Eritrea na Jamhuri ya Kiarabu ya Syria.[82] Algeria pia ilikuwa mwenyeji wa wakimbizi zaidi ya 94,000 mwishoni mwa 2018,[83] wakati Misri ilikuwa mwenyeji wa zaidi ya wakimbizi 240,000, hasa wakitoka Jamhuri ya Kiarabu ya Syria, Maeneo ya Palestina na nchi na maeneo mengine ya Kiafrika.[84] Hali ya usalama na kisiasa inayobadilika kwa haraka nchini Libya ilikuwa imechangia idadi jumla ya IDP 221,000 kufikia mwisho wa 2018 (ikiwa imeteremka kutoka zaidi ya 300,000 katika mwaka wa 2016), huku pia ikiathiri zaidi ya wakimbizi na waomba hifadhi 56,000 wanaokaa Libya.[85]

**Kama kitovu muhimu cha shughuli za mpito kwa wahamiaji wanaotoka katika nchi nyingi zilizo kusini, kanda ndogo ya Afrika Kaskazini inakabiliwa na changamoto za ulinzi zinazohusiana na uhamiaji usio halali wa kwenda Ulaya.** Katika mwaka wa 2018, takriban wahamiaji 117,000 walifika Ulaya kwa njia ya bahari.[86] Hili ni poromoko kubwa ikilinganishwa na 2017 (karibu 172,000) na 2016, wakati idadi iliongezeka hadi 364,000.[87] Kumekuwepo pia na mabadiliko katika njia zinazotumiwa na wahamiaji wengi wa baharini wasio halali; wakati wengi kutoka Afrika walioingia Ulaya katika miaka ya 2016 na 2017 walitumia njia ya Mediterania ya Kati (kutoka Libya, hasa hadi Italia), wahamiaji wasio halali waliowasili Uropa kwa njia ya bahari walifuata njia ya Mediterania Magharibi (kutoka Moroko, hasa kwenda Uhispania).[88] Kulikuwa na karibu watu 59,000 waliowasili nchini Uhispania kwa bahari, tofauti na karibu 23,000 nchini Italia.[89] Mabadiliko katika njia kuu, kutoka Mediterania ya Kati hadi Magharibi, yanahusishwa na sababu kadhaa, pamoja na ushirikiano wa karibu kati ya Umoja wa Ulaya (EU) na nchi za asili na mpito, juhudi za kuzuia magendo, pamoja na kuongezeka kwa doria za usalama wa baharini karibu na upwa wa Libya.[90] Wahamiaji kutoka nchi za Kusini mwa Jangwa la Sahara walichangia idadi kubwa ya wahamiaji wasio halali waliowasili kwa bahari nchini Uhispania, wakifuatiwa na wale wa Moroko.[91] Watu waliopitia njia ya Mediterania ya Kati kwenda Italia hasa walikuwa kutoka Tunisia, wakifuatiwa na Waeritrea, Wairaq, Wasudan na Wapakistani.[92] Kuanzia Januari hadi Novemba 2018, inakadiriwa kuwa asilimia 15 ya watu wote waliofika kwa njia isiyo halali nchini Italia wakipitia baharini walikuwa watoto wasiosindikizwa.[93]

**Kuna njia kubwa kiasi za kusafirisha wahamiaji kimagendo kwenda, ndani ya na kutoka Afrika Kaskazini, huku usafirishaji kimagendo huu ukipatikana sana katika mitandao michache ya uhalifu.**[94] Kwa msaada wa wafanya magendo, wahamiaji kutoka nchi zilizo Kusini mwa Jangwa la Sahara, kwa mfano, mara nyingi huanza safari zilizo hatari kabisa. kwenda Afrika Kaskazini, pamoja na kupitia Jangwa la Sahara.[95] Moja ya njia kuu za usafirishaji kimagendo inajumuisha wahamiaji wanaohama kutoka Somalia, Sudan na

82 UNHCR, n.d.
83 UNHCR, 2019a.
84 keshatajwa.
85 IDMC, 2019, UNHCR, 2019a.
86 IOM, n.d.b. Hii ni pamoja na waliofika Bulgaria, Cyprus, Ugiriki, Italia, Malta na Uhispania.
87 keshatajwa.
88 Frontex, 2019; MacGregor, 2019.
89 IOM, n.d.b.
90 UNHCR, 2019b; Frontex, 2019; MacGregor, 2019.
91 UNHCR, 2019b.
92 keshatajwa.
93 keshatajwa.
94 UNODC, 2018.
95 keshatajwa.

Ethiopia, wakielekea Misri na Israeli.[96] Lakini kwa kuwa hali za kijamii na kiuchumi nchini Misri zimedorora katika miaka ya hivi karibuni, wasafirishaji kimagendo wamegeukia zaidi nchi kama Libya, ambayo kabla ya 2011 ilikuwa mahali muhimu walikokwenda wafanyikazi wahamiaji na, hivi karibuni, imekuwa kitovu kikubwa cha magendo na mahali pakuu pa kuanzia safari kwa wahamiaji wanaojaribu kufika Ulaya kupitia njia ya Mediterania ya Kati.[97] Ukanda huu mdogo unaendelea kupambana na ukiukaji mkubwa wa haki za binadamu na changamoto za ulinzi; wahamiaji wengi wanaopitia hapo hukabiliwa na unyanyasaji wa kijinsia na dhuluma zenye misingi ya kijinsia, kazi ya kulazimishwa, kuwekwa kizuizini kiholela, uporaji na unyonyaji, miongoni mwa dhuluma zingine. Hii hasa ndiyo hali iliyo nchini Libya, ambapo aghalabu usafirishaji binadamu kimagendo hubadilika taratibu na kuwa biashara haramu ya usafirishaji wa binadamu. Katika mwaka wa 2018, IOM ilisaidia wahamiaji zaidi ya 16,000 kurudi nyumbani baada ya kuzuiliwa au kukwama nchini Libya,[98] baadhi wakiwa mikononi mwa wafanya magendo na wafanya biashara haramu. Mgogoro wa wenyewe kwa wenyewe uliodumu muda mrefu nchini Libya umesababisha hali ya kutotii sheria, pamoja na kudhoofisha sana taasisi zake na kuharibu uchumi wake.[99]

## Asia[100]

Asia - makazi ya karibu watu bilioni 4.6 - ilikuwa asili ya zaidi ya asilimia 40 ya wahamiaji wa kimataifa ulimwenguni katika mwaka wa 2019 (milioni 111). Zaidi ya nusu (milioni 66) walikuwa wakiishi katika nchi zingine za Asia, ongezeko kubwa kutoka 2015, wakati ilikadiriwa kuwa karibu watu milioni 61 walikuwa wanaishi barani. Kama ilivyoonyeshwa katika safu ya katikati ya kielelezo cha 7, uhamiaji wa ndani ya Asia umeongezeka sana kwa muda mrefu, ukiongezeka kutoka milioni 35 katika mwaka wa 1990. Ukuaji mkubwa umetokea pia kwa idadi ya wahamiaji waliozaliwa Asia huko Kaskazini mwa Amerika na Ulaya katika miongo miwili iliyopita. Katika mwaka wa 2019, uhamiaji kutoka Asia kwenda Kaskazini mwa Amerika ulifikia milioni 17, ukiongezeka kutoka zaidi kidogo tu ya milioni 16 mnamo 2015, wakati huko Uropa, uhamiaji kutoka Asia ulikuwa karibu milioni 22 katika mwaka wa 2019. Uhamiaji kutoka Asia kwenda Kaskazini mwa Amerika na Ulaya ulisababisha ongezeko kubwa la idadi ya wahamiaji wa Asia walio nje ya ukanda huo, na kufikia jumla ya wahamiaji milioni 44.6 walioelekea kwenye kanda mbalimbali katika mwaka wa 2019, ongezeko la asilimia 11 kutoka milioni 40 katika mwaka wa 2015.

Idadi ya wahamiaji wasiozaliwa Asia walio huko Asia imebaki katika viwango vya chini tangu mwaka wa 1990. Wazungu wanajumuisha kundi kubwa zaidi la wahamiaji kutoka nje ya Asia katika ukanda huo. Idadi hizi zinajumuisha wahamiaji kutoka sehemu ya Uropa ya iliyokuwa Umoja wa Sovieti ambao sasa wanaoishi Asia ya Kati. Katika kipindi hicho hicho, idadi ya Waafrika - kikundi kingine kikubwa kiasi cha wahamiaji walio huko Asia - imeongezeka.

96 İçduygu, 2018.

97 keshatajwa.

98 IOM, 2018b.

99 UNSMIL na OHCHR, 2018.

100 Tazama kiambatisho cha A kwa maelezo juu ya vijenzi

Kielelezo cha 7. Wahamiaji kwenda, ndani ya na kutoka Asia, 1990–2019




*Chanzo:* UN DESA, 2019a.

*Maelezo:* "Wahamiaji kwenda Asia" hurejelea wahamiaji wanaoishi katika ukanda huo (yaani Asia) ambao walizaliwa katika mojawapo ya kanda zingine (kwa mfano Ulaya au Afrika). "Wahamiaji ndani ya Asia" hurejelea wahamiaji waliozaliwa katika ukanda huo (yaani Asia) na wanaoishi nje ya nchi yao ya kuzaliwa, lakini bado katika ukanda wa Asia. "Wahamiaji kutoka Asia" hurejelea watu waliozaliwa Asia ambao walikuwa wanaishi nje ya ukanda huo (kwa mfano, Ulaya au Kaskazini mwa Amerika).

Nchi kadhaa za Asia zimepitia mabadiliko makubwa katika wingi wa idadi ya watu katika miaka ya hivi karibuni. Mabadiliko haya yanaonyeshwa kwenye kielelezo cha 8, ambacho kinaorodhesha kidaraja nchi 20 za juu za Asia zilizo na kiwango kubwa zaidi cha idadi ya watu kutoka 2009 hadi 2019. Isipokuwa Jamhuri ya Kiarabu ya Syria, nchi zote 20 za juu zilipata ongezeko la idadi ya watu katika kipindi hiki. Nchi za GCC,

ambazo zote zinawakilishwa kati ya nchi 20 za juu, zilipitia mabadiliko makubwa zaidi ya idadi ya watu katika mwongo mmoja uliopita. Uhamiaji wa kimataifa umekuwa kiamuzi muhimu cha mabadiliko ya idadi ya watu huko Asia, na hasa katika Mataifa ya GCC, ambayo yanaendelea kuwa maeneo muhimu wanakokwenda wafanyikazi wahamiaji kutoka Asia na kutoka nje ya ukanda huo. Kama inavyoonyeshwa katika kielelezo cha 9, wahamiaji wa kimataifa huunda kiwango kikubwa cha idadi ya watu kitaifa katika Mataifa ya GCC, huku wahamiaji katika Milki za Kiarabu, kwa mfano, wakichangia asilimia 88 ya idadi ya watu katika nchi hiyo.[101]

## Kielelezo cha 8. Nchi 20 kuu zilizo na mabadiliko makubwa zaidi ya kiwango cha idadi ya watu barani Asia, 2009-2019




*Chanzo:* UN DESA, 2019c.

*Maelezo:* Ni muhimu kutambua kwamba kiwango kikubwa zaidi cha mabadiliko ya idadi ya watu kutoka 2009 hadi 2019 kilikuwa na uwezekano mkubwa wa kutokea katika nchi zilizo na idadi ndogo ya watu.

Nchi mbili za Asia "zenye idadi kubwa zaidi ya watu", India na Uchina, zina idadi kubwa kabisa ya wahamiaji wanaoishi nje ya nchi (kielelezo cha 9). Ni muhimu kuongeza kuwa hii idadi kubwa kabisa ya wahamiaji wanaoenda nje ya nchi ni sehemu ndogo ya jumla ya idadi ya watu wa India na Uchina. Wahamiaji kutoka Uchina walichangia idadi kubwa ya tatu ulimwenguni ya wahamiaji waliozaliwa nje ya nchi baada ya India na Meksiko. Karibu wahamiaji milioni 3 wa Kichina walioenda nje waliishi Marekani, ambayo pia yalikuwa makazi ya vikundi vingine vikubwa vya wahamiaji wa Asia kutoka India, Ufilipino na Vietnamu. Nchi zingine zilizo na wahamiaji wengi wanaoishi nje ya nchi ni pamoja na Bangladeshi na Jamhuri ya Kiarabu ya Syria.

101 UN DESA, 2019a.

Katika nchi za GCC, wahamiaji huchangia kiwango kikubwa cha jumla ya idadi ya watu kitaifa (kielelezo cha 9). Kwa mfano, katika mwaka wa 2019, wahamiaji walikuwa asilimia 88 ya idadi ya watu katika Milki za Kiarabu; asilimia 72 nchini Kuwait; karibu asilimia 79 nchini Qatar; na asilimia 45 nchini Bahrain.[102] Wahamiaji wengi walitoka Afrika, Asia Kusini (kwa mfano, India, Pakistani, Bangladeshi na Nepal), na Asia ya Kusini-Mashariki (kwa mfano, Indonesia na Ufilipino).

Pia ni muhimu kutambua kwamba data ya sasa juu ya wahamiaji waliozaliwa nje ya nchi pia kwa kiasi fulani inaangazia matukio muhimu ya kihistoria, kama vile Mgawanyo wa 1947, uliosababisha uhamishaji mkubwa wa watu kutoka na kwenda India na Pakistani. Hii linadhihirika katika data ya 2019, ambayo inaonyesha kuwa zaidi ya wahamiaji milioni 5 na milioni 3 waliozaliwa nje, mtawalia, waliishi katika nchi hizo mbili.

## Kielelezo cha 9. Nchi 20 za juu za wahamiaji barani Asia katika mwaka wa 2019




*Chanzo:* UN DESA, 2019a.

*Maelezo ya 1:* Wingi wa idadi ya watu uliotumika kukokotoa asilimia ya wahamiaji na wahamaji unategemea idadi ya wakazi wa nchi hiyo ya UN DESA, ambayo inajumuisha wazaliwa wa kigeni.

*Maelezo ya 2:* "Mhamiaji" hurejelea wahamiaji walio wazaliwa wa kigeni wanaokaa nchini. "Mhamaji" hurejelea watu waliozaliwa nchini ambao walikuwa wakiishi nje ya nchi yao ya kuzaliwa katika mwaka wa 2019.

102 UN DESA, 2019a.

Kielelezo cha 10 kinaonyesha njia 20 kuu za uhamiaji kutoka nchi za Asia, huku zaidi ya nusu yazo - 13 kati ya 20 - zikitokea ndani ya ukanda huo. Njia hizi za uhamiaji zinawakilisha mkusanyiko wa harakati za wahamaji kwa muda mrefu na hutoa picha ya jinsi mikondo ya uhamiaji imebadilika na kuwa idadi kubwa ya wazaliwa wa kigeni katika nchi mahususi walikokwenda. Njia kubwa zaidi inaanzia Jamhuri ya Kiarabu ya Syria hadi Uturuki, ambapo zaidi ya Wasyria milioni 3.7 walikuwa wanaishi katika mwaka wa 2019. Haya ni mabadiliko kutoka miaka ya 2015 na 2017 wakati ambapo njia kubwa zaidi barani Asia ilikuwa ya India hadi Milki za Kiarabu.

Kielelezo cha 10. Njia 20 kuu za uhamiaji kutoka nchi za Asia, 2019




*Chanzo:* UN DESA, 2019a.

*Maelezo:* Njia za uhamiaji zinawakilisha mkusanyiko wa harakati za wahamaji kwa muda mrefu na hutoa picha ya jinsi mikondo ya uhamiaji imebadilika na kuwa idadi kubwa ya wazaliwa wa kigeni katika nchi mahususi walikokwenda.

Ufurushwaji wa kimataifa ndani na kutoka Asia ni sifa kuu ya ukanda huo, kama inavyoonyeshwa katika kielelezo cha 11. Jamhuri ya Kiarabu ya Syria na Afuganistani zilikuwa nchi kuu za asili ya wakimbizi ulimwenguni. Athari ya mgogoro wa Syria kuhusu ufurushwaji inaweza kuonekana wazi kwenye kielelezo cha 11, huku wakimbizi na waomba hifadhi kutoka Jamuhuri ya Kiarabu ya Syria wakiwa wengi zaidi kushinda wale wa Afuganistani. Katika mwaka wa 2018, idadi kubwa ya wakimbizi kutoka nchi za Asia waliishi katika nchi jirani. Kwa mfano, wengi wa wakimbizi kutoka Jamuhuri ya Kiarabu ya Syria walikaribishwa kukaa Uturuki, Lebanon na Jordan, wakati wengi wa wakimbizi kutoka Afuganistani, ambao idadi yao iliongezeka kutoka milioni 2.6 katika mwaka wa 2017 hadi milioni 2.7 katika mwaka wa 2018 (hasa kutokana na uzazi katika mwaka huo), walikaribishwa kukaa Pakistani na Jamhuri ya Kiislamu ya Iran. Kwa sababu ya vurugu na mateso dhidi ya Rohingya, Myanmar ilizalisha idadi kubwa ya tatu ya wakimbizi katika ukanda huo na ya nne kwa ukubwa ulimwenguni mnamo 2018, huku wakimbizi wengi wakikaribishwa kukaa nchini Bangladeshi. Kama inavyoonyeshwa katika kielelezo cha 11, ni muhimu pia kutambua kwamba nchi za asili kama Pakistani, Jamhuri ya Kiislamu ya Iran na Iraq pia ni wenyeji wa wakimbizi.

## Kielelezo cha 11. Nchi 10 kuu za Asia kulingana na jumla ya wakimbizi na waomba hifadhi, 2018




*Chanzo:* UNHCR, n.d.

*Maelezo:* "Waliokaribishwa" hurejelea wale wakimbizi na waomba hifadhi kutoka nchi zingine ambao wanaishi katika nchi inayopokea (upande wa kulia wa kielelezo); "Nje ya nchi" hurejelea wakimbizi na waomba hifadhi wanaotoka kwa nchi hiyo ambao wako nje ya nchi yao ya asili. Nchi 10 za juu zinategemea data ya 2018 ambayo inakokotolewa kwa kuchanganya wakimbizi na waomba hifadhi ndani na kutoka nchi zingine.

Ufurushwaji mkubwa na mpya zaidi wa ndani huko Asia ulitokana na majanga (kielelezo cha 12). Ufilipino, ambayo ilikuwa na ufurushwaji mpya wa watu milioni 3.8 uliotokana na majanga mwishoni mwa 2018, ilirekodi idadi kubwa zaidi ulimwenguni. Majanga yaliyosababisha ufurushwaji ni pamoja na milipuko ya volkano, na mafuriko yaliyosababishwa na masika na maporomoko ya ardhi. Kukiwa na karibu visa milioni 3.7 vya ufurushwaji, Uchina ilirekodi visa vya ufurushwaji mpya vilivyokaribia idadi ya vile vya Ufilipino. Uchina ilifuatiwa na India (milioni 2.7) na Indonesia (853,000). Mgogoro pia ulichangia idadi kubwa ya ufurushwaji mpya huko Asia, huku Jamhuri ya Kiarabu ya Syria ikiwa na idadi kubwa zaidi (milioni 1.6), karibu asilimia 9 ya idadi yake ya watu. Nchi zingine ambako mgogoro ulisababisha ufurushwaji mkubwa wa ndani ni pamoja na Afuganistain (372,000), Yemen (252,000) na Ufilipino (188,000).

## Kielelezo cha 12. Nchi 20 za juu za Asia kulingana na ufurushwaji mpya wa ndani (janga na mgogoro), 2018




*Chanzo:* IDMC, n.d .; UN DESA, 2017.

*Maelezo:* Ufurushwaji mpya unarejelea idadi ya harakati za kufurushwa ambazo zilitokea katika mwaka wa 2018, si jumla ya idadi ya mkusanyiko wa IDP inayotokana na ufurushwaji unaotokea kwa muda mrefu. Tarakimu mpya za ufurushwaji zinajumuisha watu ambao wamefurushwa zaidi ya mara moja na hazilingani na idadi ya watu waliofurushwa katika mwaka husika.

Wingi wa idadi ya watu uliotumika kukokotoa asilimia ya ufurushwaji mpya unaotokana na maafa na migogoro unatokana na jumla ya idadi ya wakazi wa nchi kulingana na makadirio ya idadi ya watu ya mwaka 2017 ya UN DESA, na asilimia inatolewa kwa madhumuni ya kutoa ufafanuzi tu.

# Sifa muhimu na maendeleo barani Asia

### *Asia ya Kusini-Mashariki*

**Kwa nchi nyingi za Asia ya Kusini-Mashariki, uhamiaji unajumuisha viwango muhimu vya uhamaji na uhamiaji, na pia uhamiaji wa mpito.** Tofauti kubwa ya mapato katika ukanda huu mdogo ni jambo kuu linaloimarisha mwenendo madhubuti wa watu kuhama kutoka nchi zenye mapato ya chini kwenda nchi zenye mapato ya juu katika (na nje ya) ukanda huu mdogo. Kuna zaidi kidogo ya wahamiaji milioni 10 wa kimataifa katika ukanda huo mdogo na zaidi kidogo ya wahamiaji milioni 21.8 kutoka ukanda huo mdogo, milioni 6.8 kati yao walihamia nchi zingine ndani ya Asia ya Kusini-Mashariki.[103] Nchi zenye uchumi ulioendelea za Malaysia na Singapore zinatambulika kwa wahamiaji wengi wanaokwenda huko. Jitihada za Chama cha Mataifa ya Asia ya Kusini-Mashariki (ASEAN) kuelekea uunganishaji mkubwa wa kikanda zimechangia ongezeko la uhamiaji wa ndani ya ukanda. Pia kuna kipengele madhubuti cha kijiografia kwa uhamiaji, huku viwango vya juu vya uhamiaji vikitokea kati ya nchi zinazoshiriki mipaka, hasa kwenye mipaka ya Tailandi na majirani wa Cambodia, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Watu wa Lao na Myanmar.[104] Njia za uhamiaji za muda mrefu katika ukanda zinabainika, ambazo zinatumiwa sana na uhamiaji wa wafanyikazi wa muda, na sehemu ndogo za uhamiaji wa kudumu (wenye ujuzi na wa familia), uhamiaji wa wanafunzi na uhamiaji wa kulazimishwa.[105]

**Uhamiaji wa wafanyikazi, sifa inayojitokeza Asia ya Kusini-Mashariki na kichocheo muhimu cha ukuaji wa uchumi na maendeleo, pia unahusishwa na matendo ya haki za binadamu yasiyofuata utaratibu.** Kwa muda mrefu wahamiaji wafanyikazi wamekuwa muhimu kwa uchumi wa nchi kuu walikokwenda katika ukanda huo - kama vile Malaysia, Singapore na Tailandi - ambapo wanasaidia kujaza mapengo katika masoko ya ajira. Hili ni jambo linalotokea hasa kwa sekta zinazohitaji ujuzi wa chini kama vile uvuvi, kazi za nyumbani na ujenzi.[106] Wakati huo huo, uwezekano wa kupata ajira na mshahara wa juu mara nyingi huwalazimisha watu kutoka nchi kama Ufilipino na Indonesia kuhamia kwenye nchi zenye uchumi uliostawi zaidi katika ukanda huo.[107] Wahamiaji wengi hutuma sehemu kubwa ya mapato yao kwa familia zao nyumbani, huku Ufilipino, kwa mfano, kila mara ikiorodheshwa kati ya nchi zinazopokea pesa nyingi zaidi zilizotumwa duniani. Katika mwaka wa 2018, pesa ambazo zinazotumwa kimataifa kuingia Ufilipino zilikuwa dola bilioni 34 za Marekani, na ilikuwa mpokeaji mkubwa wa nne ulimwenguni wa pesa zilizotumwa baada ya India, Uchina na Meksiko.[108] Lakini hata wakati uhamiaji wa wafanyikazi umesaidia kupunguza uhaba wa wafanyikazi katika nchi wanazokwenda, wahamiaji wengi wafanyikazi wanaendelea kukabili hali ya unyonyaji. Wafanyakazi walioajiriwa katika sekta zinazohitaji ujuzi wa chini, zenye wafanyikazi wengi, zisizojali hali yao ya kisheria, huathiriwa zaidi, huku unyanyasaji unaohusiana na mshahara ukiwa jambo la kawaida kabisa.[109] Wahamiaji wengi wafanyikazi huhitajika kufanya kazi kwa muda mrefu sana kwa mshahara wa chini zaidi, matokeo ya ulinzi duni unaotolewa kwa wahamiaji wafanyikazi wakati wa kuajiri na ajira.[110]

---

103 UN DESA, 2019a.

104 Hugo, 2014; Hatsukano, 2015.

105 Hugo, 2014.

106 Harkins, Lindgren na Suravoranon, 2017.

107 Pholphirul, 2018.

108 Benki ya Dunia, 2019a.

109 Harkins, Lindgren na Suravoranon, 2017.

110 keshatajwa.

**Uhamiaji unahusisha kiwango kikubwa cha uhamiaji usio halali, hasa kuhusiana na masuala ya kiuchumi kama vile umaskini na ukosefu wa kazi.** Uhamiaji usio halali kama vile kutoka Cambodia na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Watu wa Lao hadi maeneo yanayojumuisha Tailandi na Malaysia mara nyingi huwezeshwa na wafanya magendo. Wafanya magendo pia hutekeleza jukumu kubwa katika uhamiaji usio halali kutoka nje ya ukanda huo, huku wahamiaji wa Kivietnamu wakienda Ulaya, kwa mfano, mara nyingi wakitumia wafanya magendo kufikia maeneo yao.[111] Mitiririko ya uhamiaji mchanganyiko ipo (ikihusisha harakati za watu walio na wasio na mahitaji ya ulinzi wa kimataifa), kama ilivyo mitiririko ya uhamiaji unaongozwa na motisha mchanganyiko. Wahamiaji wengi wanakabiliwa na unyonyaji huko Asia ya Kusini-Mashariki, kutokana na hali yao isiyo halali. Wafanyikazi wahamiaji katika tasnia mahususi pia hukabiliwa na kazi ya kulazimishwa, unyonyaji na dhuluma kubwa (kwa mfano, katika tasnia ya uvuvi, kilimo, ujenzi na utengenezaji).[112] Mbali na ufanyaji magendo, usafirishaji haramu wa watu unaendelea kuwa changamoto huko Asia ya Kusini-Mashariki, na karibu nusu ya waathiriwa wote huko Asia (46%) wakisafirishwa katika ukanda huo mdogo.[113] Idadi kubwa ya watu husafirishwa kwa njia haramu kwa ajili ya unyanyasaji wa kijinsia na kazi ya kulazimishwa, huku idadi kubwa ya wanawake wakisafirishwa kwa njia haramu kwa ajili ya unyonyaji wa kijinsia mnamo 2016.[114] Nchi kama Malaysia na Tailandi zilikuwa na waathiriwa wengi wa kazi za kulazimishwa kuliko unyonyaji wa kijinsia mnamo 2016.[115]

**Kumekuwepo na ongezeko la ufurushwaji katika ukanda huo mdogo kwa sababu ya vurugu, mateso yaliyoenea na kutengwa.** Hali ya wakimbizi wa Rohingya ni mbaya sana, na inabaki kuwa moja ya matatizo changamano zaidi ya wakimbizi ulimwenguni. Kufikia mwisho wa 2018, kulikuwa na zaidi ya Rohingya 900,000 huko Cox Bazar, Bangladeshi, na zaidi ya watu milioni 1 wanaohitaji usaidizi wa kibinadamu.[116] Eneo la Kutupalong-Balukhali huko Cox's Bazar linaendelea kuwa makazi makubwa na yenye wahamiaji wengi zaidi ulimwenguni; wakimbizi kutoka Myanmar walikuwa idadi kubwa ya nne ya wakimbizi ulimwenguni katika mwaka wa 2018.[117] Kutokana na ongezeko la mauaji ya kimakusudi na ukiukaji wa haki za binadamu mnamo Agosti 2017, idadi kubwa ya Rohingya walifurushwa kutoka Jimbo la Rakhine la Myanmar, wengi wakitafuta ulinzi nchini Bangladeshi. Ingawa hii haikuwa mara ya kwanza ambapo Rohingya walitoroka Myanmar kwa sababu ya vurugu, vurugu za Agosti 2017 zilisababisha mojawapo ya mawimbi makubwa zaidi ya ufurushwaji katika miongo kadhaa. Wakati huo huo, ndani ya Asia ya Kusini-Mashariki, Malaysia iliendelea na mwenendo wa muda mrefu wa kuwa mwenyeji wa idadi kubwa ya wakimbizi na watu walio katika hali kama za wakimbizi (zaidi ya 120,000 katika mwaka wa 2018), hasa kama matokeo ya ufurushwaji uliosababishwa na migogoro ya wenyewe kwa wenyewe huko Myanmar kwa miaka mingi.[118] Utoaji wa makazi mapya kwa wakimbizi wanaotoka ukanda huo mdogo unafanywa hasa na nchi ambazo "kidesturi" zimekuwa zikitoa makazi hayo (kama vile Marekani, Canada na Australia), na kuna "miundombinu ya ulinzi" michache sana katika ukanda huu mdogo.[119] Pia kuna idadi kubwa ya IDP na watu wasio na utaifa katika eneo hilo, huku nchi nane katika ukanda mdogo huo zikiwa wenyeji wa watu wasio na utaifa (idadi kubwa zaidi iko Myanmar, ambayo ilikuwa mwenyeji wa zaidi ya watu 600,000 mwishoni mwa 2018).[120]

111 UNODC, 2018.
112 Gois, 2015.
113 IOM, n.d.c.
114 UNODC, 2018.
115 keshatajwa.
116 IOM, 2018c.
117 UNHCR, 2019a.
118 keshatajwa.
119 McAuliffe, 2016. "Miundombinu ya ulinzi" inajumuisha sheria za ndani, sera za kitaifa pamoja na desturi za kiutawala juu ya ulinzi; tazama Sitaropoulos, 2000.
120 Southwick, 2015; UNHCR, 2019a.

## *Kusini mwa Asia*

**Uhamiaji kutoka Kusini mwa Asia kwenda kwa kanda zingine ndogo ni sifa muhimu, huku wafanyikazi wahamiaji wengi wa muda katika nchi za GCC wakitoka katika ukanda huu mdogo.** Matarajio ya mshahara wa juu na upatikanaji wa fursa za ajira ni mambo yaliyosababisha ongezeko kubwa la idadi ya watu wanaoondoka katika eneo hili dogo katika miaka ya hivi karibuni.[121] Kwa nchi zilizo katika ukanda huo mdogo zilizo na ziada kubwa ya wafanyikazi, uhamiaji umepunguza shinikizo la wafanyikazi, huku ukisaidia kupunguza umaskini kupitia fedha zinazotumwa. Kutokana na hilo, Kusini mwa Asia ni kati ya wapokeaji wakubwa wa pesa zinazotumwa kutoka nje. Katika mwaka wa 2018, pesa zilizotumwa kimataifa kuingia India zilikuwa dola bilioni 79 za Marekani, kiasi kubwa zaidi ulimwenguni; na katika nchi kama vile Pakistani, Sri Lanka na Bangladeshi, pesa zilizotumwa zilizidi asilimia 5 ya jumla ya pato la ndani (GDP) mwaka huo huo.[122]

**Uhamiaji ndani ya ukanda huu mdogo ni sifa kubwa katika Asia ya Kusini, inayoongozwa na tofauti za kiuchumi na soko la wafanyikazi.**[123] Harakati za ndani ya ukanda, za kawaida na zisizo halali, zinahusiana na mizizi ya pamoja na thabiti ya kihistoria, ukaribu wa kijiografia, na uhusiano wa kiutamaduni na kijamaa kati ya nchi.[124] Katika mwaka wa 2019, chini ya asilimia 80 tu ya wahamiaji milioni 14 wa kimataifa walio Asia ya Kusini walitoka nchi zingine katika ukanda huo mdogo.[125] Njia kuu za uhamiaji ni pamoja na Bangladeshi-India, Afuganistani-Pakistani, India-Pakistani na Nepal-India; Hata hivyo, ni muhimu kutambua kwamba njia hizi zote ni tofauti kabisa, zikiakisi masuala mengi ya kihistoria na ya kisasa ya kiuchumi, kiusalama na kitamaduni. Kuna mamilioni ya wahamiaji wafanyikazi wa Bangladeshi na Nepal wanaofanya kazi sasa nchini India, kwa mfano, hasa katika sekta isiyo rasmi kama wafanyikazi wa ujenzi na wafanyikazi wa nyumbani, wakati ambapo njia ya India-Pakistani kwa kiasi inaonyesha ufurushwaji wa watu wengi kufuatia Mgawanyo wa 1947 wa India na Pakistani.[126] Zaidi ya hayo, wahamiaji wengi wa kimataifa wa Afuganistani milioni 3.9 ambao wanaishi katika eneo hilo (hasa katika Jamuhuri ya Kiislamu ya Iran na Pakistani) wamefurushwa pande zote mbili za mpaka kwa sababu ya migogoro na vurugu ndani ya Afuganistani ambayo imekuwa ikiongezeka na kupungua tangu miaka ya 1970.[127] Uhamiaji wa ndani katika nchi za Asia Kusini ni mpana na mkubwa kwa kiwango kuliko uhamiaji wa kimataifa, unaohusiana kimsingi na uhamiaji wa muda na msimu kutoka vijijini kwenda mijini.[128] Kuanzia mwaka 2001 hadi 2011, idadi ya watu wa mijini Kusini mwa Asia ilikua kwa watu milioni 130.[129] Hata hivyo, wakati uhamiaji wa vijijini-mijini umechangia ukuaji huu, umesababishwa sana na uainishaji upya wa makazi ya vijijini na ongezeko asili la idadi ya watu.[130]

**Uhamiaji usio halali ndani na kutoka kwenye ukanda huo mdogo ni jambo la kawaida Kusini mwa Asia, na mara nyingi husaidiwa na mitandao huru ya magendo.** Wakati idadi kamili ya watu wanaojihusisha na uhamiaji usio halali katika ukanda huo mdogo haijulikani, inakadiriwa kuwa kuna idadi kubwa ya wahamiaji

121 Doherty et al., 2014.
122 Benki ya Dunia, 2019a
123 Srivastava na Pandey, 2017.
124 keshatajwa.
125 UN DESA, 2019a.
126 Srivastava na Pandey, 2017.
127 Schmeidl, 2016; UNHCR, 2016.
128 keshatajwa.
129 Ellis na Roberts, 2016.
130 keshatajwa.

wasio halali katika ukanda huo mdogo.[131] Kwa mfano, India ni mwenyeji wa idadi kubwa ya wahamiaji wasio halali kutoka Bangladeshi, Nepal na, kwa kiwango kidogo, Sri Lanka.[132] Kanda mbalimbali zikiwemo Ulaya, Kaskazini mwa Amerika na Oceania ni miongoni mwa maeneo yanayopendelewa zaidi ya wahamiaji wasiofuata njia halali kutoka Kusini mwa Asia.[133]1Sababu za kijamii na kiuchumi na ukosefu wa usalama katika nchi za asili, pamoja na mshahara bora na fursa za ajira katika nchi wananazokwenda, ni miongoni mwa sababu zinazohusiana na uhamiaji usio halali na usafirishaji wa wahamiaji kimagendo.[134] Wahamiaji kutoka Kusini mwa Asia wakielekea Magharibi mwa Ulaya husafirishwa kimagendo kupitia Asia ya Kati na Shirikisho la Urusi, na pia kupitia Mashariki ya Kati kwenda Magharibi mwa Balkan.[135] Wahamiaji wengine wasio halali husafirishwa kimagendo hadi Malaysia, Tailandi na Indonesia kufanya kazi.[136] Kumekuwepo na visa vingi vilivyoarekodiwa vya wahamiaji wanaonyonywa na kudhulumiwa na wafanya magendo wanaowasafirisha Kusini mwa Asia.[137] Biashara ya magendo ya kusafirisha watu ni jambo linaloleta wasiwasi mkubwa Kusini mwa Asia, ingawa data na habari za nchi nyingi katika ukanda huo ni chache. Ripoti ya UNODC ya 2018 inakadiria kuwa karibu asilimia 60 ya waathiriwa wa bishara haramu ya usafirishaji waliotambuliwa katika ukanda huo katika mwaka wa 2016 walikuwa wanawake, kulingana na habari inayopatikana kuhusu nchi nne, ambazo ni Bangladeshi, Maldives, Nepal na Pakistani.[138] Huko Nepal, kulikuwa na waathiriwa watoto wengi kuliko waathiriwa watu wazima.[139]

**Migogoro, kutokuwa na utulivu wa kisiasa, vurugu na ukandamizaji wa muda mrefu vimefanya Kusini mwa Asia kuwa chanzo muhimu cha ufurushwaji; ukanda huu mdogo pia ni makazi ya idadi kubwa ya watu waliofurushwa.** Katika miaka ya hivi karibuni, kila nchi katika ukanda huu mdogo (isipokuwa Maldives) imekuwa chanzo au mwenyeji wa watu waliofurushwa makwao. Hasa, mwishoni mwa 2018, kulikuwa na wakimbizi milioni 2.7 wa Afuganistani, idadi ya pili kwa wingi wa wakimbizi ulimwenguni baada ya Jamhuri ya Kiarabu ya Syria, na IDP milioni 2.6 wa Afuganistani.[140] Nchi jirani za Pakistani na Jamhuri ya Kiislamu ya Iran zilikuwa na wakimbizi wengi zaidi kutoka Afuganistani na, hivyo, zilikuwa kati ya nchi wenyeji zinazoongoza ulimwenguni.[141] Pakistani, na mipaka yake inayopitika kwa urahisi na uhusiano wa karibu wa kikabila, lugha, dini na uchumi, imekuwa mwenyeji mkuu kwa miongo kadhaa, ikiwa na wakimbizi karibu milioni 1.4 mwishoni mwa 2018, karibu wote wakiwa Waafghani;[142] karibu wakimbizi 60,000 walirudishwa nchini Afuganistani mnamo 2017, wengi wao kutoka Pakistan.[143] Mwishoni mwa 2018, Jamhuri ya Kiislamu ya Iran ilikuwa mwenyeji wa wakimbizi karibu milioni 1,[144] na kuifanya kuwa nchi ya sita kwa wingi wa wakimbizi ulimwenguni, wakati India na Bangladeshi ziliendelea kutoa makazi kwa idadi kubwa ya IDP.[145]

131 Srivastava na Pandey, 2017.
132 Jayasuriya na Sunam, 2016.
133 McAuliffe na Jayasuriya, 2016.
134 keshatajwa.
135 Sengupta, 2018.
136 Gallagher na McAuliffe, 2016.
137 UNHCR, 2018.
138 keshatajwa.
139 keshatajwa.
140 UNHCR, 2019a; IDMC, 2019.
141 UNHCR, 2019a.
142 keshatajwa.
143 IOM na UNHCR, 2018.
144 UNHCR, 2019a.
145 IDMC, 2019. Kwa ufurushwaji wa ndani kwa ujumla, angalia pia Matriki ya Ufuatiliaji wa Ufurushwaji ya IOM, hasa kwa Afuganistani, India, Jamhuri ya Kiislami ya Iran, Pakistani na Sri Lanka.

**Watu wa Asia ya Kusini wako katika hatari zaidi ya kukumbwa na majanga yanayoanza polepole na yanayoanza mara moja yanayohusiana na hatari za asili na mabadiliko ya tabianchi.** Isipokuwa kwa Afuganistani, ambapo migogoro na vurugu ilichangia kwa kiasi kikubwa katika kufurusha watu kutoka nyumbani kwao, majanga yalihusika katika ufurushwaji mwingi huko Asia ya Kusini katika mwaka wa 2018.[146] Kulikuwa na ufurushwaji mpya uliokadiriwa kuwa milioni 3.3 kule Kusini mwa Asia uliotokana na hatari zilizoanza mara moja katika mwaka wa 2018, huku wengi wa wale walioathiriwa wakiwa nchini India, Afuganistani, Sri Lanka na Bangladeshi. Kuhusiana na wingi wa idadi ya watu, Kusini mwa Asia ina idadi kubwa zaidi ya watu walio katika hatari ya kufurushwa kutoka kwa makazi yao kutokana na hatari za ghafla, huku Bangladeshi, India na Pakistani zikiwa na hatari kubwa zaidi yinayotokana na majanga.[147] India ndiyo iliyoathiriwa zaidi na majanga katika ukanda huo mdogo, ikiwa na zaidi ya wakimbizi milioni 2.7 waliofurushwa kutokana na dhoruba za tropiki na mafuriko.[148] Afuganistani ilikuwa na idadi ya pili kubwa ya wakimbizi waliofurushwa na majanga katika ukanda huo mdogo, ikiwa na ufurushwaji mpya 371,000, hasa kutokana na hali ya ukame. Maelfu ya watu pia walihama makazi yao huko Sri Lanka na Bangladeshi kwa sababu ya masika.[149] Kiwango cha uharibifu unaohusiana na majanga na ufurushwaji Kusini mwa Asia katika miaka ya hivi karibuni kimesababishwa na mipango mibovu na ukosefu wa utayari katika ukanda huo.[150] Uhamiaji na mwendo ni mikakati muhimu sana ya kukabiliana na mambo na kama kiitikio cha matukio ya mabadiliko ya mazingira katika Asia ya Kusini - pamoja na kuongezeka kwa kiwango cha bahari, mmomonyoko wa pwani, mafuriko na kumaliza maji yaliyo chini ya ardhi - yote ambayo yanaleta changamoto kubwa katika ukanda huo.[151]

### *Mashariki mwa Asia*

**Mashariki mwa Asia inakabiliwa na mabadiliko makubwa ya idadi ya watu, huku nchi kadhaa zikikabiliwa na viwango vya chini vya uzazi na watu wanaozeeka, na hili linasababisha marekebisho ya sera za uhamiaji.** Nchi kama Japani tayari zinakabiliwa na ongezeko hasi la idadi ya watu, wakati kiwango cha uzazi cha Jamhuri ya Korea kiko chini sana ya kiwango cha ubadili cha 2.1 kinachohitajika ili kudumisha idadi ya watu.[152] Katika mwaka wa 2019, Japani ilikuwa na uwiano wa chini kabisa wa msaada kote ulimwenguni (idadi ya wafanyikazi kwa kila mstaafu) na, pamoja na Uchina, ilikuwa kati ya nchi 10 za juu zilizo na idadi kubwa ya watu zilizo na viwango vya kuzaa ambavyo viko chini ya ubadili.[153] Mabadiliko haya ya idadi ya watu yana athari kubwa kwa deni la umma, hali za huduma za jamii bila malipo na masoko ya wafanyikazi. Kwa mfano, Japani inakabiliwa na uhaba mkubwa wa wafanyikazi.[154] Uhalisia huu unawashawishi watunga sera kutathmini tena njia finyu za kihistoria kuhusu uhamiaji, ambazo zimehusishwa na kiwango cha juu cha usawa wa kitamaduni katika nchi zingine, uzoefu mdogo katika sera ya uhamiaji ikilinganishwa na kanda na kanda ndogo zingine, na hali ya kutopendwa kwa uhamiaji katika nchi nyingi.[155]

---

146 IDMC, 2019.

147 keshatajwa.

148 keshatajwa.

149 keshatajwa.

150 IDMC, 2018a.

151 Climate and Development Knowledge Network, 2014b. Tazama pia Ionesco, Mokhnacheva na Gemenne, 2017.

152 UN DESA, 2019c.

153 keshatajwa.

154 Nye, 2019.

155 Staedicke, Batalova na Zong, 2016.

**Kadiri nchi muhimu za Asia ya Mashariki zinavyoshuhudia kupungua kwa idadi ya watu, nchi kadhaa zimepitisha sheria mpya za uhamiaji au zimetekeleza mipango inayokusudia kuwavutia wafanyikazi wa kigeni.** Mnamo Desemba 2018, Bunge la Japani liliidhinisha sheria mpya ya uhamiaji iliyopunguza vizuizi kwa wafanyikazi wa kigeni katika tasnia zinazokabiliwa na uhaba wa wafanyikazi, huku mabadiliko hayo yakitarajiwa kuvutia zaidi ya wafanyikazi 300,000.[156] Mabadiliko ya hivi karibuni katika sheria za uhamiaji za Japani pia ni sehemu ya majibu ya kuongezeka kwa mahitaji ya wafanyikazi katika maeneo kama vile ujenzi, wakati nchi inajitayarisha kuandaa Michezo ya Olimpiki ya 2020 huko Tokyo.[157] Wakati huo huo, kupitia Mfumo wa Kibali cha Ajira, ambao unaruhusu uingiaji wa wafanyikazi wa kigeni kutoka nchi za Asia wanazoshirikiana nazo[158] ambazo zimetia sahihi hati za makubaliano, Jamhuri ya Korea inatarajiwa kupokea wafanyikazi wa kigeni 56,000 katika mwaka wa 2019, katika juhudi za kukabiliana na upungufu wa wafanyikazi.[159] Uchina, kimsingi ikiwa ni nchi ya asili ya wafanyikazi wahamiaji, pia hivi karibuni imejaribu kuvutia wafanyikazi katika sekta zenye ujuzi wa hali ya juu na ujuzi wa chini, kwa njia ya kubadilisha sera zake za uhamiaji na kutia sahihi makubaliano ya nchi mbili. Kuvutia idadi inayoongezeka ya wafanyikazi wa kigeni hakujapangwa tu ili kushughulikia upungufu wa ujuzi, lakini pia ni sehemu ya juhudi za nchi kuelekea kwenye uwazi zaidi wa kiuchumi na ujumuishaji. Kwa mfano, katika mwaka wa 2018, Uchina ililegeza mahitaji yake ya viza kwa wataalamu na wafanyikazi wenye ujuzi wa hali ya juu, kwa nia ya kuvutia wageni wenye vipaji vya juu[160] ili wajiunge na uchumi ambao unabadilika taratibu kutoka kwa utengenezaji hadi kwa huduma. Katika mwaka huo huo, nchi ilianzisha, kwa mara ya kwanza, Utawala wa Uhamiaji wa Taifa. Ofisi mpya ya uhamiaji ni itikio kwa ukuaji wa idadi ya wahamiaji wa kimataifa nchini Uchina na hitaji la kuleta ufanisi kwa kurahisisha na kusimamia vyema uhamiaji.[161] Pia, Uchina na Ufilipino zilitia sahihi makubaliano katika mwaka wa 2018 ambayo yataruhusu wafanyikazi 300,000 wa Ufilipino, pamoja na walimu 100,000 wa Kiingereza, kufanya kazi nchini Uchina.[162]

**Uhamiaji katika Mashariki mwa Asia unazidi kutambuliwa na uhamaji mkubwa wa wanafunzi wanaotoka nje na wanaoingia ndani.** Idadi ya wanafunzi wa kimataifa kutoka Mashariki mwa Asia, hasa katika kiwango cha elimu ya juu, imeongezeka haraka katika miaka ya hivi karibuni, wakati idadi ya wanafunzi wa kigeni katika kanda ndogo pia inaendelea kuongezeka. Wakisukumwa na matarajio ya elimu ya kiwango bora, idadi kubwa ya wanafunzi wa kimataifa kutoka Mashariki mwa Asia husoma katika nchi kama Marekani, Canada na Uingereza. Uchina iliendelea kuwa chanzo kikuu cha wanafunzi wa kimataifa ulimwenguni katika mwaka wa 2018, huku zaidi ya nusu milioni ya wanafunzi wake wakianza masomo ya juu nje ya nchi, ongezeko la zaidi ya asilimia 8 kutoka mwaka wa 2017.[163] Hata hivyo, Mashariki mwa Asia si tu chanzo kubwa cha wanafunzi wa kimataifa, bali pia polepole inakuwa kivutio muhimu kwa wanafunzi wa kigeni, wengi wao wakitoka katika ukanda huo mdogo. Idadi ya wanafunzi wa kimataifa katika taasisi za elimu ya juu nchini Uchina ilikuwa zaidi ya 490,000 katika mwaka wa 2018.[164] Wanafunzi kutoka Jamuhuri ya Korea walichangia idadi kubwa zaidi ya

156 McCurry, 2019; BBC, 2018.

157 Tian na Chung, 2018.

158 Nchi washirika wa Mfumo wa Kibali cha Ajira wa 2019 ni pamoja na Bangladeshi, Cambodia, Uchina, Timor-Leste, Indonesia, Kyrgyzstan, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Watu wa Lao, Mongolia, Myanmar, Nepal, Pakistani, Sri Lanka, Tailandi, Ufilipino, Uzbekistan na Vietnamu.

159 Ju-Young, 2018.

160 Ning, 2018.

161 The State Council, the People’s Republic of China, 2018.

162 Jennings, 2018.

163 Ministry of Education of the People’s Republic of China, 2019a; Shuo, 2019.

164 Ministry of Education of the People’s Republic of China, 2019b.

wanafunzi wa kimataifa nchini Uchina katika mwaka wa 2018.[165] Walifuatwa na wanafunzi kutoka Tailandi, Pakistani na India.[166]

**Uhamiaji wa nje wa wafanyikazi, hasa kutoka Uchina, unamaanisha kuwa ukanda huo mdogo ni mojawapo ya wapokeaji wakubwa wa pesa zilizotumwa kimataifa ulimwenguni.** Katika mwaka wa 2019, wahamiaji wa kimataifa waliozaliwa Uchina walikuwa watu waliozaliwa nchi za kigeni, wa tatu kwa wingi ulimwenguni baada ya Wahindi na Wameksiko, huku karibu wahamiaji milioni 11 wa Kichina wakiishi nje ya Uchina.[167] Katika mwaka wa 2018, mtiririko wa pesa zinazotumwa ulimwenguni ulifikia karibu Dola bilioni 690 za Marekani, huku Uchina ikipokea zaidi ya Dola bilioni 67 za Marekani, mgao mkubwa wa pili wa pesa zinazotumwa kimataifa ulimwenguni baada ya India.[168]

**Ingawa sura hii inazingatia hasa uhamiaji wa kimataifa, ni muhimu kutambua kwamba, katika muktadha huu, uhamiaji wa ndani umekuwa jambo muhimu katika nchi za Mashariki mwa Asia, ukijumuisha hali isiyokuwa ya kawaida ya watu kutoka maeneo ya vijijini kwenda kwenye vituo vya mijini.** Wakati kasi ya ukuaji wa miji imepungua na hata kufifia katika sehemu za bara kama Magharibi mwa Asia, Mashariki mwa Asia imepitia moja ya viwango vya haraka zaidi vya ukuaji wa miji katika miongo michache iliyopita.[169] Kufikia mwaka wa 2015, sehemu ya idadi ya watu wa mijini katika ukanda mdogo huo ilikuwa imeongezeka hadi asilimia 60, zaidi ya mara tatu tangu mwaka wa 1950.[170] Hii imetambulika kuwa hali iliyoko Uchina, ambapo mageuzi ya kiuchumi na kijamii ya miaka ya 1980 yalianzisha moja ya uhamiaji mkubwa wa kibinadamu katika historia. Miongoni mwa mageuzi hayo kulikuwa na ulegezaji wa mfumo wa Hukou, uliobuniwa kurekodi na kudhibiti uhamiaji wa ndani, ambao uliunganisha ufikiaji wa huduma na hadhi ya makazi ya watu. Matokeo yake ni kuwa, mamia ya mamilioni ya wafanyikazi, wakisukumwa na matarajio ya ajira na mshahara wa juu, waliondoka mashambani kuelekea mijini, ambapo shughuli nyingi za kiuchumi zilikuwa zinapatikana na zinahitaji wahamiaji wafanyikazi wasio na ujuzi na wenye ujuzi.[171] Watu wengi wamehama kutoka mikoa ya magharibi ya China kwenda mikoa yake ya mashariki. Mienendo ya kijamiii na kiuchumi kati ya magharibi na mashariki mwa China ni masuala muhimu, huku magharibi ikijulikana kwa viwango vya juu vya ukuaji wa idadi ya watu, wafanyikazi wa ziada na mapato ya chini, wakati mashariki inakabiliwa na uhaba wa wafanyikazi katika maeneo ya miji mikubwa na inarekodi mapato ya juu na elimu ya viwango vya juu.[172]

**Kipengele kipya (kisicho cha kawaida) katika mienendo ya uhamiaji ya Mashariki mwa Asia kilikuwa ni kuwasili kwa mamia ya waomba hifadhi kutoka nchi zilizoharibiwa na migogoro na vurugu.** Katika mwaka wa 2018, zaidi ya waomba hifadhi 500 wa Yemen waliwasili kwenye Kisiwa cha Jeju cha Jamuhuri ya Korea, wakaingia kupitia sera ya viza huru ya kisiwa hicho iliyokusudiwa kuvutia watalii.[173] Kuwasili kwa Wayemeni kulizusha mjadala mkali wa umma na hisia dhidi ya wahamiaji, katika nchi ambayo maombi ya hifadhi yamekuwa ya chini kihistoria. Hapo awali, Jamhuri ya Korea haikuwa nchi wanakokwenda watu wanaotafuta ulinzi (isipokuwa wale kutoka Jamuhuri ya Watu wa Kidemokrasia ya Korea).[174] Kufikia mwisho wa 2017, Uchina na Jamhuri ya Korea zilikuwa na waomba hifadhi 600 na karibu 20,000, mtawaliwa.[175]

165 keshatajwa.
166 keshatajwa.
167 UN DESA, 2019a.
168 Benki ya Dunia, 2019a.
169 UN DESA, 2018.
170 keshatajwa.
171 Hu, 2012; Qin et al., 2016.
172 Hugo, 2015.
173 Kwon, 2019.
174 Watu kutoka Jamhuri ya Kidemokrasia ya Watu wa Korea ambao huhamia Jamhuri ya Korea wakitafuta ulinzi hawachukuliwi kuwa waomba hifadhi, lakini wanatambuliwa kama raia chini ya Katiba ya Jamhuri ya Korea.
175 UNHCR, 2019a.

## *Asia ya Kati*

**Harakati za uhamiaji katika Asia ya Kati hufanyika kwa kiasi kikubwa kutoka kwenye ukanda huo mdogo, na hasa kuelekea kaskazini hadi kwenye Shirikisho la Urusi.** Kwa mfano, katika mwaka wa 2019, kulikuwa na wahamiaji wasiotimia milioni 5 waliozaliwa Asia ya Kati ambao walikuwa wakiishi katika Shirikisho la Urusi.[176] Kukiwa na mishahara mikubwa zaidi na nafasi bora za ajira,[177] kwa muda mrefu Shirikisho la Urusi limekuwa mahali pa kwenda panapoongoza kwa wahamiaji wafanyikazi kutoka Asia ya Kati.[178] Kwa watu wa Kyrgyzstan vijijini, kwa mfano, uhamiaji wa wafanyikazi umekuwa mkakati wa kujitafutia riziki, huku wafanyikazi wahamiaji wengi wa Kyrgyz wakitafuta ajira katika Shirikisho la Urusi, na mikoa kama Siberia ikizidi kupendwa.[179] Shirikisho la Urusi pia linavutia kwa sababu ya idadi kubwa ya Wakyrgyz ambao tayari wameimarika nchini na wanatoa msaada kwa njia ya kutafuta makazi yanayofaa na kazi kwa wageni waliofika.[180] Lakini si wahamiaji wote kutoka Asia ya Kati kwenda Shirikisho la Urusi ni wahamiaji wafanyikazi wenye ujuzi mdogo; wahamiaji kutoka Kazakhstan, kwa mfano, wanajumuisha kwa kiasi kikubwa wanafunzi na wataalamu wenye ujuzi wa juu.[181] Watu kutoka Asia ya Kati pia huhamia sehemu zingine za Uropa na Uchina, ambapo uhusiano kati ya kazi na familia ni thabiti kiasi. Idadi inayoongezeka ya Waasia wa Kati pia inahamia maeneo kama Uturuki na Jamhuri ya Korea kutafuta kazi; uhamaji kwenda Jamuhuri ya Korea umewezeshwa na makubaliano ya wafanyikazi baina ya nchi mbili kama vile Uzbekistan na Kyrgyzstan.[182]

**Uhamiaji wa ndani ya ukanda ni sifa muhimu katika ukanda huo mdogo na inaungwa mkono na viungo vya kijiografia, kitamaduni, kiuchumi, kisiasa na kijamii ambavyo ni vya kihistoria.** Asia ya Kati ni makazi ya mamilioni ya wahamiaji wa kimataifa, hasa kutoka katika eneo hilo dogo, lakini pia kutoka ukanda mdogo mwingine. Kimsingi wahamiaji hutoka katika nchi za Umoja wa Kisovieti wa zamani, ambao wengi wao ni wanachama wa sasa wa Umoja wa Nchi Huru za Madola ya Kisovieti.[183] Katika mwaka wa 2019, Kazakhstan, kwa mfano, ilikuwa na idadi kubwa ya watu waliozaliwa nje (milioni 3.7), ambao milioni 2.4 walizaliwa katika Shirikisho la Urusi.[184] Sasa hivi Kazakhstan ni nchi ya mpito na ya uhamiaji, ikivutia wafanyikazi wenye ujuzi kutoka nchi anuwai na, inazidi kuwa mahali wanapokwenda wafanyikazi wahamiaji wenye ujuzi wa chini kutoka Kyrgyzstan, Tajikistan na Uzbekistan. Katika miaka ya hivi karibuni, nchi za Asia ya Kati zimerekebisha sera zinazosimamia uhamiaji wa ndani ya ukanda, ikiwa ni pamoja na kuhitimishwa kwa makubaliano ya nchi mbili juu ya kuingia na kukubaliwa tena.[185] Kwa mfano, kuanzishwa kwa Jumuiya ya Uchumi ya Eurasia katika mwaka wa 2015 kumeruhusu watu kutoka nchi wanachama - ikiwa ni pamoja na Kazakhstan na Kyrgyzstan kuvuka, kutoka nchi moja hadi nyingine bila vizuizi, kuishi, kufanya kazi na kusoma katika nchi zingine wanachama wa Umoja huo.[186] Kwa sasa ushirikiano zaidi unatokea katika ukanda huo wa kuimarisha usimamizi wa mtiririko mchanganyiko, ikiwa ni pamoja na mambo yanayohusiana na usimamizi wa mpaka, haki na ulinzi wa wahamiaji, na uhamiaji usio halali.[187] Kuna utambuzi unaokua wa umuhimu wa kutekeleza sera imara za uhamiaji na mipango ili kulinda haki na hadhi ya wahamiaji, pamoja

176 UN DESA, 2019a.
177 Sengupta, 2018.
178 Turaeva, 2018.
179 Sengupta, 2018.
180 keshatajwa.
181 Nikiforova na Brednikova, 2018.
182 Eurasianet, 2019; Matusevich, 2019.
183 keshatajwa.
184 UN DESA, 2019a.
185 OSCE, 2016.
186 Eurasian Economic Union, n.d.
187 IOM, 2016a.

na familia na jamii zao. Wafanyakazi wahamiaji wa kiume na wa kike kutoka Asia ya Kati wanaweza kuwa katika hatari ya unyonyaji na dhuluma, hasa katika ajira isiyo rasmi, kama vile ujenzi, kilimo na kazi za nyumbani.[188]

**Pesa zinazotumwa kimataifa hutekeleza jukumu muhimu katika uchumi wa nchi za Asia ya Kati, hasa kwa nchi ambazo hazijaendelea sana katika ukanda huo mdogo.** Nchi mbili kati ya 10 za juu duniani zinazopokea pesa zilizotumwa zinapohusishwa na Jumla ya Pato la Ndani ziko katika ukanda huu mdogo - Kyrgyzstan na Tajikistan.[189] Nchini Kyrgyzstan, pesa zinazotumwa zinakadiriwa kupunguza kiwango cha umaskini kitaifa kwa asilimia 6-7.[190] Mtiririko wa pesa zinazotumwa kuingia nchi za Asia ya Kati kwa kiasi kikubwa huakisi mikondo ya uhamiaji ndani na kutoka kwa ukanda huo mdogo, ambayo inahusiana sana na kazi na uzalishaji mali. Pesa zinazotumwa kutoka Shirikisho la Urusi, kwa mfano, zimekuwa kiasi kubwa kwa muda, zikisaidiwa na gharama ndogo za uhawilishaji kutoka Shirikisho la Urusi kwenda nchi za Asia ya Kati. Baada ya miaka michache ya kushuka mfululizo, ikisababishwa na kushuka kwa uchumi na mabadiliko ya sera katika Shirikisho la Urusi, utumaji wa pesa kwenda Ulaya na Asia ya Kati uliimarika katika mwaka wa 2017, ikikua kwa asilimia 21 na kufikia Dola bilioni 48 za Marekani katika mwaka wa 2017.[191] Takwimu hii iliongezeka hadi dola bilioni 59 katika mwaka wa 2018.[192] Miongoni mwa mambo yaliyosababisha ukuaji huu ni kuendelea kufufuka kwa shughuli za kiuchumi katika Shirikisho la Urusi.[193]

**Uhamiaji usio halali ni sifa inayopatikana Asia ya Kati, ingawa ni vigumu kutambua idadi halisi.** Mara nyingi, wahamiaji wasio halali hutoka ndani na nje ya ukanda huo mdogo, huku wale wanaopitia Asia ya Kati huelekea Ulaya Magharibi. Kwa wahamiaji wengi, sehemu za kwanza za kuingilia ni Kyrgyzstan na Tajikistan kabla ya kusafirishwa kimagendo kupitia Kazakhstan na Shirikisho la Urusi hadi Ulaya Magharibi.[194] Masuala kama vile usimamizi dhaifu wa mipaka, pamoja na mipaka iliyotengwa, vimechangia uhamiaji usio halali katika ukanda mdogo wote.[195] Usafirishaji kimagendo wa wahamiaji katika Asia ya Kati ni mchakato changamano, na unahusisha mipango rasmi na isiyo rasmi katika maeneo anuwai ya mpaka katika ukanda huo mdogo, pamoja na shughuli zinazovuka mipaka ambazo husaidia kuwezesha usafiri wa watu kupita Asia ya Kati.[196]

### *Mashariki ya Kati*

**Nchi za Ghuba zina idadi kubwa zaidi ya wahamiaji wafanyikazi wa muda mfupi ulimwenguni.** Zikiendeshwa na utajiri wa mafuta, nchi za GCC zimepitia maendeleo ya kiuchumi ya kiwango cha juu katika miongo michache iliyopita, zikiwavutia wafanyikazi wenye ujuzi na wenye ujuzi kiasi kwa sekta mbalimbali, pamoja na ujenzi na matengenezo, huduma ya rejareja na huduma za nyumbani. Katika nchi kama Qatar, ongezeko la mahitaji ya hivi karibuni ya wafanyikazi katika maeneo kama vile ujenzi kunachochewa kwa kiasi na maandalizi ya nchi kwa Kombe la Dunia la 2022.[197] Ongezeko la uhamiaji wa wafanyikazi kwenda Mataifa ya GCC kumesababisha mabadiliko makubwa ya idadi ya watu. Katika mwaka wa 2019, wahamiaji walichangia

188 IOM, 2016b.
189 Benki ya Dunia, 2019a.
190 UNDP, n.d.
191 Benki ya Dunia, 2018a, 2018b.
192 Benki ya Dunia, 2019a.
193 keshatajwa.
194 Sengupta, 2018.
195 keshatajwa.
196 keshatajwa.
197 Buckley et al., 2016.

idadi kubwa ya watu katika nusu ya nchi za GCC - wakiwa ni asilimia 88 ya idadi ya watu katika Milki za Kiarabu, karibu asilimia 79 nchini Qatar na asilimia 72 nchini Kuwait.[198] Wahamiaji wafanyikazi katika nchi za GCC kimsingi hutoka Asia na Afrika. Tofauti za mapato kati ya nchi za asili na nchi wanazokwenda wahamiaji ni kichocheo muhimu cha uhamiaji, huku nchi za Ghuba zikitoa mshahara wa juu na nafasi za ajira kwa wahamiaji wafanyikazi.[199] Licha ya maendeleo fulani, udhibiti na ulinzi wa haki za wahamiaji vinabaki kuwa changamoto katika ukanda huu mdogo. Mfumo wa ufadhili wa Kafala,[200] ambao unawafunga wafanyikazi wahamiaji na waajiri wao na unatekelezwa katika Mataifa kadhaa ya GCC, umefanyiwa uchunguzi makini. Ingawa Mataifa kadhaa ya Ghuba yametekeleza mageuzi katika mfumo wa Kafala, mabadiliko yamekuwa madogo na yamekuwa na athari chanya ndogo sana kwa wahamiaji.[201] Mfumo wa ufadhili bado umeenea na unazidi kuchangia katika hali ya kuweza kudhuruwa ya wahamiaji wafanyikazi katika Ghuba, pamoja na hali ya kulazimishwa kufanya kazi na kudhulumiwa kimalipo.[202]

**Migogoro ya wenyewe kwa wenyewe, kuongezeka kwa vurugu za kimadhehebu na kuenea kwa ugaidi (hasa na Daesh) kumesababisha viwango kubwa vya ufurushwaji wa ndani na wa kimataifa katika ukanda huo mdogo katika miaka ya hivi karibuni.** Nchi mbili katika ukanda huo mdogo - Jamhuri ya Kiarabu ya Syria na Yemen - zinakabiliwa na dharura ya "ngazi ya 3" (uainishaji wa mfumo wa misaada ya kibinadamu ulimwenguni kwa migogoro ya kibinadamu mikali, na mikubwa zaidi) na ni wachangiaji wakuu wa takwimu jumla za watu waliofurushwa kwao ulimwenguni.[203] Mgogoro katika Jamhuri ya Kiarabu ya Syria, unaotokea sasa kwa zaidi ya miaka saba, umehamisha zaidi ya nusu ya idadi ya watu wa nchi hiyo, ukiwa na zaidi ya wakimbizi milioni 6.6 na IDP zaidi ya milioni 6.1, na ulikuwa umetoa karibu waomba hifadhi 140,000 kufikia mwisho wa 2018.[204] Mawimbi mfululizo ya ufurushwaji nchini Iraq - sifa iliyobainika tangu mwanzo wa karne - yaliendelea na kuongezeka katika mwaka wa 2016 na pia 2017. Hili lilitokea katika muktadha wa juhudi za kulitwaa tena eneo na kukabiliana na Daesh. Ingawa Wairaq zaidi ya milioni 1.9 walibaki wakimbizi wa ndani kufikia mwisho wa 2018, hii ilikuwa mara ya kwanza kwa karibu zaidi ya miaka minne ambapo idadi hii ilipungua na kuwa chini ya milioni 2.[205] Idadi inaendelea kuongezeka ya Wairaq ambao pia wamerudi nyumbani, kwani Daesh imezidi kurudishwa nyuma na kupoteza eneo huko Iraq na katika Jamhuri ya Kiarabu ya Syria; kundi hili la wapiganaji limepoteza zaidi ya asilimia 90 ya maeneo ambayo lilidhibiti katika nchi zote mbili.[206] Hali ya kisiasa na kiusalama ya Yemen iliendelea kuzorota, na vurugu na hali isiyotabirika iliyotokea iliiacha nchi na zaidi ya IDP milioni 2.3 mwishoni mwa 2018.[207] Kufikia mwisho wa 2018, zaidi ya asilimia 8 ya watu wa Yemen walikuwa wakimbizi wa ndani.

**Mashariki ya Kati inaendelea kuwa mwenyeji wa sehemu kubwa ya wakimbizi ulimwenguni.** Kufikia mwisho wa 2018, ukanda mdogo wa Mashariki ya Kati ulikuwa mwenyeji wa idadi kubwa zaidi ya wakimbizi ulimwenguni, pamoja na wakimbizi waliosajiliwa na Shirika la Usaidizi na Kazi la Umoja wa Mataifa kwa Wakimbizi wa Palestina katika Mashariki ya Karibu (UNRWA).[208] Nchi jirani haziepuki kushiriki mzigo mkubwa wakati wa kuwakaribisha watu wanaotafuta hifadhi katika nchi zingine, na uwezo huu ni sifa muhimu ya

198 UN DESA, 2019a.

199 Jacobsen na Valenta, 2016.

200 "Mfumo wa Kafala unazuia kuungana kwa familia kwa wahamiaji wasio na ujuzi, unawafunga kwa mwajiri mmoja, unawazuia kuoa wenyeji, na kutekeleza vikwazo vingine juu ya haki na mwendo ili wahamiaji wakae kama wafanyikazi wa muda mfupi katika nchi za Ghuba" (Rahman, 2013).

201 Diop, Johnston na Le, 2018.

202 keshatajwa.

203 OCHA, n.d.

204 UNHCR, 2019a; IDMC, 2019.

205 IDMC, 2019; IOM, 2018d.

206 Seligman, 2018.

207 IDMC, 2019.

208 UNHCR, 2019b.

mikondo ya kisasa ya ufurushwaji katika ukanda huo mdogo. Kama nchi zinazopakana na Jamhuri ya Kiarabu ya Syria na wenyeji wakuu wa wakimbizi wa Syria, Uturuki, Lebanon na Jordan zote zilikuwa kati ya nchi 10 zinazoongoza ulimwenguni katika kuwakaribisha wakimbizi katika mwaka wa 2018 (Uturuki ni ya kwanza, Lebanon ya saba na Jordan ya kumi).[209] Kina cha uwajibikaji wao ni dhahiri wakati idadi ya wakimbizi katika kila nchi inalinganishwa na idadi ya watu kitaifa - nchini Lebanon, kulikuwa na wakimbizi 156 kwa kila wakazi 1,000; nchini Jordan, 72 kwa kila 1,000; na Uturuki, 45 kwa kila 1,000.[210] Nchi zingine katika ukanda huu mdogo, pamoja na zile zilizoathiriwa na migogoro, pia zinahifadhi wakimbizi wengi, zikiwa ni pamoja na Yemen na Iraq, na hata Jamhuri ya Kiarabu ya Syria.[211] Wakimbizi karibu milioni 5.5 waliosajiliwa na UNWRA pia wanakaa katika ukanda huu mdogo.[212]

**Uhamiaji usio halali ndani na kutoka kwa ukanda huu mdogo unaendelea kuwa changamoto kwa wahamiaji na Mataifa.** Kukosekana kwa utulivu wa kisiasa na migogoro ya muda mrefu katika Mashariki ya Kati ni vichocheo vikuu vya uhamiaji usio halali na usafirishaji wa wahamiaji kimagendo katika ukanda huu mdogo.[213] Wahamiaji wengi wanaosafirishwa kimagendo katika ukanda huu mdogo ni watu wanaokimbia migogoro na vurugu. Usafirishaji wa wahamiaji kimagendo na uhamiaji usio halali mara nyingi huenda sambamba na harakati za wakimbizi na hifadhi.[214] Kwa kuwa migogoro imeongezeka katika ukanda wote mdogo, ndivyo ilivyo pia kwa idadi ya wahamiaji wanaosafirishwa kimagendo na nchi zilizoathiriwa na mitandao ya magendo. Zaidi ya hayo, mitandao ya magendo imekuwa ya mseto zaidi na changamano.[215] Idadi kubwa sana ya wakimbizi wa Syria waliokaribishwa katika nchi jirani, pamoja na mgogoro ulioendelea kwa muda mrefu na uwezekano mdogo wa kurudi katika Jamuhuri ya Kiarabu ya Syria, umesababisha wakimbizi kujiingiza katika uhamiaji usio halali hadi kwa nchi zingine, hasa zile za Ulaya kupitia njia ya Mediterania ya Mashariki.

## Ulaya[216]

Zaidi ya wahamiaji wa kimataifa milioni 82 waliishi Ulaya katika mwaka wa 2019, ongezeko la karibu asilimia 10 tangu mwaka wa 2015, wakati wahamiaji milioni 75 wa kimataifa waliishi katika ukanda huo. Zaidi kidogo ya nusu ya hawa (milioni 42) walizaliwa Ulaya lakini walikuwa wakiishi mahali pengine katika ukanda huo; wakati idadi hii imeongezeka kwa wastani tu tangu 2015, ilikuwa ya chini sana mnamo 1990, karibu milioni 28 (kielelezo cha 13). Kuanzia mwaka 2015 hadi 2019, idadi ya wahamiaji ambao si Wazungu huko Ulaya iliongezeka kutoka zaidi ya milioni 35 hadi kama milioni 38.

Katika mwaka wa 1990, kulikuwa na kiasi sawa cha Wazungu wanaoishi nje ya Ulaya kama wasio Wazungu wanaoishi Ulaya. Hata hivyo, tofauti na ukuaji wa uhamiaji kwenda Ulaya, idadi ya Wazungu wanaoishi nje ya Ulaya ilipungua zaidi wakati wa miaka 30 iliyopita, na ilirudi tu kwa viwango vya 1990 katika miaka ya hivi karibuni. Katika mwaka wa 2019, wahamiaji waliozaliwa Ulaya waliokaa nje ya bara hilo walikuwa kimsingi wakikaa Kaskazini mwa Amerika (milioni 7.4). Kulikuwa na ukuaji taratibu wa wahamiaji wa Uropa huko Asia na Oceania kutoka 2010 hadi 2019.

---

209 keshatajwa.

210 UNHCR, 2019a.

211 keshatajwa.

212 UNRWA, n.d.

213 İçduygu, 2018.

214 keshatajwa.

215 keshatajwa.

216 Tazama kiambatisho cha A kwa maelezo juu ya vijenzi vya Ulaya.

Kielelezo cha 13. Wahamiaji kwenda, ndani ya na kutoka Ulaya, 1990–2019




*Chanzo:* UN DESA, 2019a.

*Maelezo:* “Wahamiaji kwenda Ulaya” hurejelea wahamiaji wanaoishi katika ukanda huo (yaani Ulaya) ambao walizaliwa katika moja ya kanda zingine (kwa mfano, Afrika au Asia). “Wahamiaji ndani ya Ulaya” hurejelea wahamiaji waliozaliwa katika ukanda huo (yaani Ulaya) na wanaoishi nje ya nchi yao ya kuzaliwa, lakini bado katika ukanda wa Ulaya. “Wahamiaji kutoka Ulaya” hurejelea watu waliozaliwa Ulaya ambao walikuwa wanaishi nje ya ukanda huo (kwa mfano, Amerika ya Kusini na Karibiani au Kaskazini mwa Amerika).

Nchi kadhaa za Ulaya zimepitia mabadiliko makubwa katika wingi wa idadi ya watu katika mwongo uliopita. Kielelezo cha 14 kinapanga kidaraja nchi 20 za juu za Uropa zilizo na mabadiliko makubwa zaidi ya kiwango cha idadi ya watu kutoka 2009 hadi 2019. Wakati nchi zingine, kama vile Luxemburg, Norway na Uswisi zilishuhudia ukuaji wa idadi ya watu, zingine zilipata punguzo kubwa la idadi ya watu katika miaka 10 iliyopita. Lithuania, Bosnia na Herzegovina na Latvia zilipata punguzo kubwa zaidi la idadi ya watu (zaidi ya 10%). Viwango vya chini vya uzazi ni vichocheo muhimu zaidi vya mabadiliko hasi ya watu katika sehemu za Ulaya. Hata hivyo, uhamiaji halisi hasi, ambapo idadi ya wahamaji inazidi idadi ya wahamiaji, pia umechangia

kupungua kwa idadi ya watu barani, hasa katika nchi kama Lithuania na Latvia. Majadiliano juu ya mabadiliko ya idadi ya watu huko Ulaya, na uhusiano wake na uhamiaji, yanaweza kusomwa hapo chini kwenye "Sifa muhimu na maendeleo huko Ulaya".

Kielelezo cha 14. Nchi 20 za juu zilizo na mabadiliko makubwa zaidi ya kiwango cha idadi ya watu Ulaya, 2009-2019




*Chanzo:* UN DESA, 2019c.

*Maelezo:* Ni muhimu kutambua kwamba kiwango kikubwa zaidi cha mabadiliko ya idadi ya watu kutoka 2009 hadi 2019 kina uwezekano mkubwa wa kutokea katika nchi zilizo na idadi ndogo ya watu.

Nchi nyingi mashariki mwa Ulaya - kama Shirikisho la Urusi, Ukraine, Poland na Romania - zina idadi kubwa zaidi ya wahamaji katika ukanda huo (kielelezo cha 15). Ikiwa na zaidi ya wahamaji zaidi ya milioni 10 katika mwaka wa 2019, Shirikisho la Urusi lilikuwa na idadi kubwa zaidi ya raia wake wanaoishi nje ya nchi huko Ulaya. Baada ya Shirikisho la Urusi na Ukraine, Poland na Uingereza zilikuwa za tatu na nne kwa idadi kubwa ya wahamaji huko Ulaya (milioni 4.4 na milioni 4.3 mtawalia). Bosnia na Herzegovina zilikuwa na sehemu kubwa zaidi ya wahamaji ikilinganishwa na idadi ya wakazi katika mwaka wa 2019, ambao wengi wao waliondoka wakati Yugoslavia ya zamani iliporomoka. Ureno na Bulgaria, nchi mbili ambazo zina historia ndefu ya uhamaji, pia zilikuwa na sehemu kubwa ya idadi ya watu nje ya nchi.

Ikiwa na wahamiaji zaidi ya milioni 13 katika mwaka wa 2019, Ujerumani ilikuwa na idadi kubwa zaidi ya watu waliozaliwa nje ya nchi kuliko nchi yoyote huko Ulaa; idadi ya wahamiaji katika nchi hiyo iliongezeka kwa karibu milioni 3 kati ya 2015 na 2019. Vikundi vikubwa zaidi vilitoka Poland, Uturuki, Shirikisho la Urusi, Kazakhstan na Jamhuri ya Kiarabu ya Syria. Kila moja ya idadi ya watu wa Uingereza na Ufaransa ilijumuisha zaidi ya watu milioni 9.5 na karibu milioni 8 waliozaliwa nje, mtawalia, katika mwaka wa 2019. Wahamiaji waliozaliwa katika nchi za Afrika Kaskazini zinazozungumza Kifaransa walichangia idadi kubwa

zaidi ya watu nchini Ufaransa waliozaliwa nje ya nchi. Huko Uingereza, idadi kubwa zaidi ya wahamiaji ilikuwa kutoka India, Poland na Pakistani. Zikiwa na idadi ya watu waliozaliwa nje ya nchi karibu milioni 6, Italia na Uhispania zilishika nafasi ya tano na sita kwa sehemu walikopenda kwenda wahamiaji huko Ulaya katika mwaka wa 2019; nchi zote mbili zilipata ongezeko dogo la idadi ya wahamiaji waliozaliwa nje ya nchi tangu mwaka wa 2015. Watu wengi waliozaliwa nje katika nchi hizi walitoka sehemu zingine Ulaya - kama vile Romania, Albania na Ujerumani - au kutoka nchi za Afrika Kaskazini kama vile Moroko. Uhamaji wa watu kutoka nchi za Muungano wa Kisovieti wa zamani - kama vile Ukraine, Kazakhstan na Uzbekistan - ulichangia baadhi ya njia kuu zaidi za uhamiaji za Ulaya (angalia kielelezi cha 16). Kama inavyoonyeshwa kwenye kielelezo cha 15, kati ya nchi 20 kuu za uhamiaji katika ukanda huo, Uswisi ilikuwa na sehemu kubwa zaidi ya wahamiaji katika idadi yake ya watu (29.9%) ikifuatiwa na Uswidi (20%), Austria (19.9%) na Ubelgiji (17.2%).

## Kielelezo cha 15. Nchi 20 za juu za wahamiaji wa Ulaya katika mwaka wa 2019




*Chanzo:* UN DESA, 2019a.

*Maelezo ya 1:* Wingi wa idadi ya watu uliotumika kukokotoa asilimia ya wahamiaji na wahamaji unategemea idadi jumla ya wakazi wa nchi hiyo kulingana na UN DESA, ambayo inajumuisha watu waliozaliwa nje ya nchi.

*Maelezo ya 2:* "Mhamiaji" hurejelea wahamiaji walio wazaliwa wa kigeni wanaokaa nchini. "Mhamaji" hurejelea watu waliozaliwa nchini ambao walikuwa wakiishi nje ya nchi yao ya kuzaliwa katika mwaka wa 2019.

Kielelezo cha 16 kinaonyesha njia 20 kuu za uhamiaji zinazojumuisha nchi za Ulaya, zinazowakilisha mkusanyiko wa harakati za uhamaji kwa muda mrefu, na kutoa picha ya jinsi mikondo ya uhamiaji imebadilika kuwa idadi kubwa ya watu waliozaliwa nje ya nchi katika nchi mahususi walizokwenda. Moja ya sifa za kuvutia za njia kuu za uhamiaji zinazohusisha nchi za Ulaya ni kwamba nyingi ni njia za ndani ya ukanda. Shirikisho la Urusi linaangaziwa sana katika njia kuu. Watu waliozaliwa Urusi walio katika mataifa ya awali yaliyounda Muungano wa Kisovieti ya zamani - kama vile Ukraine, Kazakhstan na Uzbekistan - walichangia baadhi ya njia kuu zaidi za uhamiaji za Ulaya katika mwaka wa 2019. Hata hivyo, ni muhimu kutambua kwamba watu hawa waliozaliwa Urusi walikuwa wahamiaji wa kimataifa tu baada ya kutanguliwa kwa Muungano wa Kisovyeti mnamo 1991; kabla ya hapo, walikuwa wahamiaji wa ndani katika Muungano wa Kisovieti. Shirikisho la Urusi pia lilikuwa eneo la pili kubwa walikokwenda wahamiaji huko Ulaya baada ya Ujerumani.

Kielelezo cha 16. Njia 20 kuu za uhamiaji zinazohusisha nchi za Ulaya, 2019




*Chanzo:* UN DESA, 2019a.

*Maelezo:* Njia za uhamiaji zinawakilisha mkusanyiko wa harakati za wahamaji kwa muda mrefu na hutoa picha ya jinsi mikondo ya uhamiaji imebadilika na kuwa idadi kubwa ya wazaliwa wa kigeni katika nchi mahususi walikokwenda.

Katika mwaka wa 2018, Ujerumani iliendelea kuwa mwenyeji wa idadi kubwa zaidi ya wakimbizi na waomba hifadhi huko Ulaya na ya tano kwa ukubwa ulimwenguni (kielelezo cha 17). Idadi kubwa zaidi ya wakimbizi nchini Ujerumani walitoka Jamhuri ya Kiarabu ya Syria, Iraq na Afuganistani. Ufaransa na Uswidi zilikuwa za pili na tatu kwa nchi wenyeji zenye wakimbizi wengi barani Ulaya, zikiwa na zaidi ya 368,000 na zaidi ya 248,000, mtawalia. Ukraine na Shirikisho la Urusi zilizalisha idadi kubwa ya wakimbizi barani Ulaya mwishoni mwa 2018, karibu 93,000 na 61,000 mtawalia.

Kielelezo cha 17. Nchi 10 kuu za Ulaya kulingana na jumla ya wakimbizi na waomba hifadhi, 2018




*Chanzo:* UNHCR, n.d.

*Maelezo:* "Waliokaribishwa" hurejelea wale wakimbizi na waomba hifadhi kutoka nchi zingine ambao wanaishi katika nchi inayopokea (upande wa kulia wa kielelezo); "Nje ya nchi" hurejelea wakimbizi na waomba hifadhi wanaotoka kwa nchi hiyo ambao wako nje ya nchi yao ya asili. Nchi 10 za juu zinategemea data ya 2018 ambayo inakokotolewa kwa kuchanganya wakimbizi na waomba hifadhi walio ndani na kutoka nchi zingine.

Ufurushwaji mpya wa ndani katika mwaka wa 2018 huko Ulaya ulikuwa ni matokeo ya majanga, si migogoro (kielelezo cha 18). Ukraine ilikuwa nchi pekee barani Ulaya iliyo na ufurushwaji uliohusiana na migogoro mipya ya ndani ya nchi katika mwaka wa 2018, ikiwa na makadirio ya watu 12,000 wapya waliofurushwa kwa sababu ya migogoro na vurugu katika mwaka huo. Ufurushwaji mwingine mpya wa ndani uliobakia ulisababishwa na majanga, huku Ugiriki ikirekodi idadi kubwa zaidi ya ufurushwaji uliosababishwa na majanga (9,200) ikifuatiwa na Ufaransa (6,300). Nchi zote mbili zilikumbwa na mafuriko na dhoruba kubwa. Shirikisho la Urusi, Uhispania na Italia zilirekodi zaidi ya ufurushwaji mpya 3,000 uliotokana na majanga katika mwaka wa 2018.

Kielelezo cha 18. Nchi 20 kuu za Ulaya kulingana na ufurushwaji mpya wa ndani (janga na mgogoro), 2018




*Chanzo:* IDMC, n.d; UN DESA, 2017.

*Maelezo:* Ufurushwaji mpya unarejelea idadi ya harakati za kufurushwa ambazo zilitokea mwaka wa 2018, si jumla ya idadi ya mkusanyiko wa IDP inayotokana na ufurushwaji unaotokea kwa muda mrefu. Takwimu mpya za ufurushwaji zinajumuisha watu ambao wamefurushwa zaidi ya mara moja na hazilingani na idadi ya watu waliofurushwa katika mwaka husika.

Wingi wa idadi ya watu uliotumika kukokotoa asilimia ya ufurushwaji mpya unaotokana na majanga na migogoro inayotokana na jumla ya idadi ya wakazi wa nchi kulingana na makadirio ya idadi ya watu ya mwaka 2017 ya UN DESA, na asilimia inatolewa kwa madhumuni ya kutoa ufafanuzi tu.

## Sifa muhimu na maendeleo barani Ulaya

### *Kusini-Mashariki na Mashariki mwa Ulaya*

**Kwa nchi nyingi za Kusini-Mashariki na Mashariki mwa Ulaya, uhamaji wala si uhamiaji ndio umekuwa jambo muhimu katika miaka na miongo ya hivi karibuni, huku kukiwa na viwango vya chini vya uhamiaji ikilinganishwa na sehemu zingine za Ulaya.** Kwa sababu hii na sababu zingine, inakadiriwa kuwa nchi kadhaa barani Ulaya zitashuhudia upungufu mkubwa wa idadi ya watu ifikapo mwaka 2050 (ikiwa ni pamoja na Bosnia na Herzegovina, Bulgaria, Romania, Jamhuri ya Moldova na Ukraine).[217] Uhamaji kutoka nchi za Mashariki mwa Ulaya kwenda Magharibi mwa Ulaya umekuwa mtindo unaokua, hasa tangu kupanuliwa kwa EU mnamo 2004 na 2007 ili kujumuisha nchi zaidi zilizo wanachama Mashariki mwa Ulaya, wakati ikipanua mipaka ya nje ya EU hadi kwa nchi zisizo wanachama huko Mashariki.[218] Uhamaji kutoka Mashariki na Kusini mwa Ulaya kwa kiasi kikubwa unajumuisha wahamiaji wafanyikazi katika kazi zinazohitaji ujuzi wa hali ya juu na wa hali ya chini. Miaka ya hivi karibuni, kwa mfano, imekuwa na ongezeko kubwa la idadi ya wataalamu wa matibabu wanaohamia Ulaya Magharibi. Wakivutiwa na mishahara ya juu, idadi kubwa ya wataalamu wa matibabu kutoka nchi kama vile Romania, Poland na Slovakia wameacha nchi zao na kwenda kufanya kazi Magharibi mwa Ulaya.[219] Inakadiriwa kuwa, kufikia mwaka 2015, Romania ilikuwa imepoteza nusu ya madaktari wake.[220] Uhamaji wa wataalamu wenye ujuzi wa hali ya juu, pamoja na idadi ya watu inayopungua, vimesababisha upungufu mkubwa wa wafanyikazi katika baadhi ya sekta katika nchi kadhaa za Mashariki mwa Ulaya.

**Licha ya kupungua kwa idadi ya watu kote Ulaya kunakotarajiwa, huku Mashariki mwa Ulaya inakabiliwa na mabadiliko makubwa zaidi ya idadi ya watu, nchi zingine zinapinga uhamiaji kama sehemu ya suluhisho pana la tatizo hilo.** Huku viwango vya uzazi huko Ulaya vikipungua, idadi ya wazee inaendelea kuongezeka. Watu zaidi wanaishi kwa muda mrefu na miaka ambayo mtu anatarajiwa kuishi huko Ulaya na Kaskazini mwa Amerika ilifika miaka 78.7 katika mwaka wa 2019 na inakadiriwa kuwa itaongezeka hadi miaka 83.2 ifikapo 2050.[221] Kote ulimwenguni, watu wanaokadiriwa kuwa milioni 962 walikuwa na umri uliozidi miaka 60 katika mwaka wa 2017, huku Ulaya ikiwa na asilimia kubwa zaidi (25%).[222] Kadiri idadi ya wazee inavyopanuka, ndivyo mifumo ya ulinzi wa kijamii katika nchi za Ulaya Mashariki itakavyokuwa na shinikizo kubwa, huku matumizi ya umma kwenye huduma ya afya na pensheni yakitarajiwa kuongezeka sana[223] Wakati huo huo, kupungua kwa idadi ya watu wa umri wa kufanya kazi kutakuwa na athari kubwa kwa wafanyikazi wa Ulaya, huku wastani wa umri wa watu wanaoshiriki katika nguvukazi ukifikia miaka 42.6 ifikapo 2030.[224] Hata wakati watu wa Mashariki mwa Ulaya wanaendelea kuzeeka, nchi nyingi katika ukanda mdogo huo zinasita kukumbatia uhamiaji kama sehemu moja ya suluhisho la muda mrefu kwa mizozo ya idadi ya watu inayokaribia. Tayari nchi kama vile Hungary zimeanza kuhisi athari hasi za kupungua kwa nguvukazi. Kama njia ya kukabiliana na uhaba wa wafanyikazi na athari yake kwa uchumi wa nchi, katika mwaka wa 2018 Serikali ya Hungary ilipitisha sheria yenye utata ambayo ilizusha malalamiko ya umma; ilivyoitwa “sheria ya watumwa” iliweza kuwahitaji watu kufanya kazi hadi saa 400 za ovataimu ya

217 UN DESA, 2015.
218 Kahanec na Zimmermann, 2009.
219 Hervey, 2017.
220 keshatajwa.
221 UN DESA, 2019c.
222 keshatajwa.
223 ILO, 2018.
224 keshatajwa.

lazima.[225] Mnamo Februari 2019, Hungary pia ilitangaza faida mpya za mikopo na ushuru zilizolenga kuongeza kiwango cha chini cha uzazi nchini humo, wakati ikibaki kupinga waziwazi uhamiaji.[226] Hata hivyo, wakati mielekeo na mazungumzo ya kisiasa kuhusu uhamiaji yakibaki hasi kote Mashariki mwa Ulaya, nchi kama vile Poland zimekuwa zikiajiri wafanyikazi wa kigeni, hasa wale waliotoka Ukraine, ili kushughulikia upungufu wa wafanyikazi. Idadi ya watu wa Ukraine nchini Poland imeongezeka sana tangu mapigano yalipoanza Mashariki mwa Ukraine katika mwaka wa 2014. Katika mwaka wa 2017, Poland ilitoa vibali vya makazi zaidi ya 660,000 kwa wageni, huku vingi (zaidi ya 85%) vikipewa watu wa Ukraine.[227]

**Shirikisho la Urusi linabaki kuwa nchi kuu wanayoenda wakimbizi katika ukanda huo mdogo (na moja kati ya nchi muhimu zaidi ulimwenguni).** Katika mwaka wa 2019, nchi hii ilikuwa mwenyeji wa wahamiaji wa kimataifa karibu milioni 11.6.[228] Wahamiaji wengi wametoka nchi jirani, hasa wanachama wa Umoja wa Nchi Huru za Madola ya Kisovieti.[229] Wahamiaji kutoka Ukraine walichangia idadi kubwa zaidi ya watu waliozaliwa katika nchi za kigeni walio katika Shirikisho la Urusi (zaidi ya milioni 3), wakifuatwa na Kazakhstan (karibu milioni 2.5) na Uzbekistan (milioni 1.1).[230] Idadi kubwa ya wahamiaji wa Shirikisho la Urusi, ambao wengi wao ni wahamiaji wafanyikazi, inamaanisha kuwa nchi hiyo pia ni mojawapo ya chimbuko kubwa la utumaji pesa ulimwenguni. Katika mwaka wa 2018, pesa zilizotumwa kutoka Shirikisho la Urusi zilifikia Dola bilioni 21 za Marekani, kutokana na kasi ndogo lakini thabiti ya kufufuka kwa uchumi wa nchi hiyo, ambayo inaendelea kuvutia wahamiaji wafanyikazi.[231] Katika mwaka wa 2019, Ukraine pia ilikuwa na idadi kubwa ya watu waliozaliwa nje ya nchi wakiwa karibu milioni 5, kukiwa na wahamiaji waliotoka kwa kiasi kikubwa Belarusi, Kazakhstan, Jamhuri ya Moldova, Shirikisho la Urusi na Uzbekistan.[232]

**Ukanda huo mdogo umeshuhudia ongezeko la ufurushwaji katika miaka ya hivi karibuni, hasa kutokana na mgogoro wa muda mrefu huko Mashariki mwa Ukraine.** Mgogoro huo, ambao sasa uko katika mwaka wake wa tano, umesababisha ufurushwaji mkubwa wa ndani na kusababisha wakimbizi na wahamiaji kukimbilia Mataifa jirani. Kufikia mwisho wa 2018, Ukraine ilikuwa chanzo cha karibu wakimbizi 93,000 na karibu IDP 800,000.[233] Katika mwaka wa 2018 pekee, kulikuwa na ufurushwji mpya wa watu 12,000 uliosababishwa na migogoro/vurugu huko Ukraine (angalia kielelezo cha 18).[234] Idadi kubwa ya wakimbizi kutoka Ukraine walikuwa wanaishi katika Shirikisho la Urusi. Tangu kuanza kwa mgogoro huko Mashariki mwa Ukraine katika mwaka wa 2014, watu wanaokadiriwa kuwa 400,000 walihamia Shirikisho la Urusi, huku idadi kubwa ikiwa imepata hadhi ya ukimbizi au hifadhi ya muda.[235]

## *Kaskazini, Magharibi na Kusini mwa Ulaya*

**Uhamiaji wa ndani ya kanda huko Ulaya una nguvu sana, na unaendelea kuongezeka muda unavyosonga.** Kufikia 1 Januari 2017, kulikuwa na watu milioni 22 walioishi katika moja ya nchi wanachama ya EU wakiwa na uraia wa nchi nyingine mwanachama, likiwa ongezeko la kutoka milioni 16 mwaka uliopita.[236] Kiwango

225 Karasz na Kingsley, 2018; Peto, 2019.

226 Szakacs, 2019; Walker, 2019.

227 Eurostat, 2018.

228 UN DESA, 2019a.

229 Umoja wa Nchi Huru za Madola ya Kisovieti una nchi tisa wanachama: Armenia, Azabajani, Belarusi, Kazakhstan, Kyrgyzstan, Jamhuri ya Moldova, Shirikisho la Urusi, Tajikistan na Uzbekistan; pamoja na nchi mbili shiriki: Turkmenistan na Ukraine.

230 UN DESA, 2019a.

231 Benki ya Dunia, 2019a; Hickey, 2019; Benki ya Dunia 2018a.

232 UN DESA, 2019a.

233 UNHCR, 2019a; IDMC, 2019.

234 UNHCR, 2019.

235 UNHCR, 2019c.

236 Eurostat, 2019.

hicho cha juu cha uhamiaji wa ndani ya ukanda kinawezeshwa na mipango ya usafiri bila vizuizi ambao unawawezesha raia kuvuka mipaka bila kufanyiwa ukaguzi mipakani. Eneo la Schengen, ambalo linajumuisha nchi 22 wanachama wa EU na nchi 4 zisizo wanachama wa EU, huhakikishia zaidi ya raia milioni 400 usafiri huru wa ndani.[237] Katika mwaka wa 2017 Romania, Poland, Italia, Ureno na Bulgaria zilikuwa na idadi kubwa zaidi ya raia wao walioishi katika nchi zingine wanachama wa EU.[238] Hata hivyo, usafiri usio vikwazo huko Ulaya unakabiliwa na changamoto. Katika mwaka wa 2015, kuwasili kwa idadi kubwa ya wahamiaji na wakimbizi Ulaya kupitia Mediterania kuliweka shinikizo kwenye mfumo wa kawaida wa hifadhi ya Ulaya na kukaathiri utendakazi wa sheria za Schengen. Hili lilisababisha kusimamishwa kwa muda kwa mfumo wa Dublin na kuanzishwa kwa ukaguzi wa mipaka ya nchi kadhaa wanachama.[239] Pia kuna kiwango cha kutokuwa na uhakika, hasa kwa wafanyikazi wahamiaji, kufuatia kura ya maoni ya wanachama wa EU mnamo Juni 2016 nchini Uingereza kuhusu mipangilio ya uhamiaji wa siku zijazo inayotokana na mashauriano ya "Brexit". Hata hivyo, suala kubwa zaidi ni kukamilika kwa Brexit yenyewe, na ikiwa / ni vipi itatekelezwa.

**Uhamiaji unaendelea kuwa suala lenye ubishani huko Ulaya na linabaki la kwanza kwenye ajenda ya kisiasa katika ukanda wote.** Wakati mijadala yenye usawa kuhusu suala hilo haipo, kauli za kisiasa na mazungumzo ya umma juu ya uhamiaji wakati mwingine yametawaliwa na maoni ya wale wanaopingaji uhamiaji. Katika kipindi cha 2017 na 2018, vikundi vya mrengo wa kulia kote Ulaya vilikuza hadithi za uwongo au "habari ghushi" juu ya uhamiaji.[240] Hili lilionekana wazi katika kampeni zilizoratibiwa mtandaoni dhidi ya Mkataba wa Uhamiaji Duniani na wanaharakati wa mrengo wa kulia, pamoja na kupitia mitandao ya kijamii, maombi ya mtandaoni na video. Kampeni hizo hasi zilitekeleza jukumu kubwa katika kuibusha upinzani dhidi ya Mkataba wa Uhamiaji Duniani katika nchi kadhaa za Ulaya, na kusababisha serikali zingine kujiondoa kwenye makubaliano ya uhamiaji.[241] Mitazamo ya kijumla kuhusu uhamiaji pia inabaki imegawanyika, wakati kauli hasi za kisiasa dhidi ya uhamiaji zinaendelea kupewa nafasi kuu katika chaguzi kadhaa za kitaifa kote Ulaya.[242] Utafiti wa Tume ya Ulaya ya 2018 uligundua kuwa Wazungu wanne kati ya kumi huona uhamiaji kama shida zaidi kuliko fursa.[243] Katika savei tofauti iliyofanywa katika nchi 10 za EU[244] na Kituo cha Utafiti cha Pew, zaidi ya nusu walisema kuwa wanataka wahamiaji wachache katika nchi zao.[245]

**Uhamiaji usio halali unaendelea kuleta changamoto kwa ukanda huo, na unabaki juu kwenye ajenda za Ulaya mnamo 2017 na 2018.** Kufikia mwisho wa 2018, idadi kubwa zaidi ya waliowasili kwa njia isiyo halali Ulaya kupitia baharini walitumia njia ya Magharibi mwa Mediterania, inayoelekea Uhispania.[246] Hii ilikuwa tofauti na 2016 na 2017, wakati wahamiaji wasio halali waliopitia baharini walifika Ulaya kwa idadi kubwa kupitia njia ya Mediterania ya Kati kutoka Libya (hasa wakielekea Italia) au kutoka Uturuki hadi Ugiriki kwenye njia ya Mashariki mwa Mediterania. Katika mwaka wa 2018, zaidi ya wahamiaji 117,000 na 26,000 waliwasili Ulaya kwa njia ya bahari na nchi kavu, mtawalia.[247] Kulikuwa na karibu watu 59,000 waliowasili kwa bahari nchini Uhispania na 23,370 nchini Italia mwaka huo huo.[248] Zaidi ya wahamiaji 2,000 walifariki katika Mediterania katika mwaka wa 2018, huku njia ya Mediterania ya Kati ikiwa mbaya zaidi kwa

237 European Commission, n.d.

238 Eurostat, 2019.

239 keshatajwa.

240 McAuliffe, 2018.

241 keshatajwa.

242 Diamant na Starr, 2018.

243 European Commission, 2018b.

244 Nchi 10 za EU zilizofanyiwa savei ni pamoja na Ugiriki, Hungary, Italia, Ujerumani, Uswidi, Poland, Ufaransa, Uholanzi, Uingereza na Uhispania.

245 Connor na Krogstad, 2018.

246 Frontex, 2019; MacGregor, 2019.

247 IOM, n.d.b.

248 keshatajwa.

wahamiaji wasio halali mnamo 2018 (zaidi ya vifo 1,300).[249] Ingawa idadi ya wahamiaji waliokufa baharini wakijaribu kufika Ulaya ilipungua katika mwaka wa 2018 kwa sababu ya watu wachache kwaa jumla kujaribu kuvuka, kiwango cha vifo katika njia ya Mediterania ya Kati kiliongezeka kutoka 2.6% mnamo 2017 hadi 3.5% mnamo 2018 na, kufikia Aprili 2019, ilikuwa imefikia asilimia 10.[250] Idadi kubwa ya waliowasili kwa bahari katika mwaka wa 2018 walitoka nchi ambazo zinaendelea kuathiriwa na vurugu na migogoro, ikiwa ni pamoja na Afuganistani, Jamhuri ya Kiarabu ya Syria na Iraq, hasa kwenda Ugiriki. Waafrika wa Kaskazini na Kusini mwa Jangwa la Sahara pia waliendelea kuwa sehemu kubwa ya mtiririko wa wahamiaji kwenda Ulaya, hasa kwenda Italia na Uhispania.

**Bado biashara haramu ya usafirishaji wa binadamu ni changamoto kubwa barani Ulaya, na ukanda huo umeshuhudia ongezeko la usafirishaji haramu wa wafanyikazi na unyonyaji wa kijinsia.** Usafirishaji haramu wa binadamu kwa ajili ya unyonyaji wa kijinsia unabaki kuwa aina kuu ya biashara haramu ya binadamu huko Ulaya (56%), ikifuatwa na unyonyaji wa wafanyikazi (26%) na aina zingine za unyonyaji, kama vile kuombaomba kwa kulazimishwa au kutolewa kwa viungo (18%).[251] Wanawake na wasichana wanaendelea kuwa kundi lililo hatarini zaidi (68% ya waathiriwa), mara nyingi hutumika katika huduma na kazi za nyumbani na ukahaba wa kulazimishwa.[252] Mienendo miwili muhimu uliyoripotiwa na Mataifa wanachama wa EU ni ongezeko kubwa la usafirishaji haramu wa watoto (23% ya waathiriwa wote) na ukuaji wa usafirishaji haramu ndani ya EU (44% ya waathiriwa ni raia wa EU).[253] Maelezo mafupi ya wafanyabiashara wa magendo na mbinu za utendaji zimebadilika, kukiwa na ongezeko katika idadi ya wanawake na wahalifu wenye umri mdogo, na jukumu linaloongezeka la mtandao na mitandao ya kijamii katika uandikishaji na usambazaji wa nyenzo za unyonyaji. Licha ya kuongezeka kwa utambuzi na ufahamu wa vitendo vya biashara haramu ya usafirishaji, mashtaka na viwango vya kupatikana na hatia bado viko chini. Wahamiaji wasio halali wako katika hatari zaidi, kwa kuwa wafanyabiashara wa magendo mara nyingi hutumia hadhi yao kuwafunga katika mzunguko wa unyonyaji. Katika mwaka wa 2018, kisa cha wavuvi wahamiaji waliokuwa wanafanya kazi kwenye vyombo vya kuvulia samaki vilivyosajiliwa Ireland walifikishwa kwenye Mahakama Kuu ya Jamhuri ya Ireland; iliaminika kuwa baadhi ya wahamiaji walikuwa wamesafirishwa kwa njia isiyo halali na walifanya kazi katika hali ngumu, pamoja na kunyanyaswa kwa sababu ya rangi yao, kulipwa mshahara mdogo na kufanyishwa kazi kupita kiasi[254]

## Amerika ya Kusini na Karibiani[255]

Uhamiaji kwenda Kaskazini mwa Amerika ni jambo muhimu katika Amerika ya Kusini na eneo la Karibiani. Katika mwaka wa 2019, zaidi ya wahamiaji milioni 26 walikuwa wameshasafari kaskazini na walikuwa wakiishi Kaskazini mwa Amerika ya. Kama inavyoonyeshwa kwenye kielelezo cha 19, watu wa Amerika ya Kusini na Karibiani wanaoishi Kaskazini mwa Amerika wameongezeka sana kwa muda mrefu, kutoka takribani milioni 10 mnamo 1990 na milioni 25.5 mnamo 2015 hadi milioni 26.6 mnamo 2019. Wengine milioni 5 walikuwa Ulaya katika mwaka wa 2019; wakati idadi hii imeongezeka kidogo tu tangu 2015, idadi ya wahamiaji kutoka Amerika ya Kusini na Karibiani wanaoishi Ulaya imekuwa zaidi ya mara nne tangu 1990. Kanda zingine, kama

249 IOM, n.d.d.
250 IOM, 2019c.
251 European Commission, 2018c.
252 keshatajwa.
253 keshatajwa.
254 O'Faolain, 2018.
255 Tazama kiambatisho cha A kwa maelezo juu ya vijenzi vya America ya Kusini na Karibiani.

Asia na Oceania, zilikuwa makazi ya idadi ndogo sana ya wahamiaji kutoka Amerika ya Kusini na Karibiani mwaka wa 2019 (wahamiaji 400,000 na 200,000, mtawalia).

Idadi jumla ya wahamiaji kutoka kanda zingine wanaoishi Amerika ya Kusini na Karibiani haijabadilika, ikiwa karibu milioni 3 katika miaka 30 iliyopita. Hizi zilijumuisha zaidi Wazungu (ambao idadi yao imepungua kidogo katika kipindi hicho) na Wamarekani wa Kaskazini, ambao idadi yao imeongezeka. Katika mwaka wa 2019, idadi ya Wazungu na Wamarekani wa Kaskazini walioishi Amerika ya Kusini na Karibiani ilikuwa milioni 1.4 na milioni 1.2, mtawalia.

Kielelezo cha 19. Wahamiaji kwenda, ndani ya na kutoka Amerika ya Kusini na Karibiani, 1990–2019




*Chanzo:* UN DESA, 2019a.

*Maelezo:* "Wahamiaji kwenda Amerika ya Kusini na Karibiani" hurejelea wahamiaji wanaoishi katika ukanda huo (yaani Amerika Kusini na Karibiani) ambao walizaliwa katika mojawapo ya kanda zingine (kwa mfano Ulaya au Asia). "Wahamiaji ndani ya Amerika ya Kusini na Karibiani" hurejelea wahamiaji waliozaliwa katika ukanda huo (yaani Amerika ya Kusini na Karibiani) na wanaoishi nje ya nchi yao ya kuzaliwa, lakini bado ndani ya Amerika ya Kusini na ukanda wa Karibiani. "Wahamiaji kutoka Amerika ya Kusini na Karibiani" hurejelea watu waliozaliwa Amerika ya Kusini na Karibia ambao walikuwa wanaishi nje ya ukanda huo (kwa mfano, Ulaya au Kaskazini mwa Amerika).

Nchi kadhaa katika Amerika ya Kusini na Karibiani zimepitia mabadiliko makubwa ya idadi ya watu katika mwongo mmoja uliopita. Kielelezo cha 20 kinaonyesha nchi 20 za juu za Amerika ya Kusini na Karibiani ambazo zimeshuhudia mabadiliko makubwa zaidi ya kiwango cha idadi ya watu kutoka 2009 hadi 2019. Nchi zote 20 za juu zilishuhudia ongezeko la idadi ya watu katika kipindi hiki, huku kiwango kikubwa zaidi cha mabadiliko ya idadi ya watu kikitokea Amerika ya Kati. Belize ilikuwa na mabadiliko makubwa zaidi ya asilimia, huku idadi ya watu ikiongezeka kwa asilimia 24 kutoka 2009 hadi 2019. Ilifuatiwa na Guatemala na Honduras, ambazo idadi yao iliongezeka kwa karibu asilimia 23 na 20 mtawalia.

Kielelezo cha 20. Nchi 20 kuu zilizo na mabadiliko makubwa zaidi ya kiwango cha idadi ya watu huko Amerika ya Kusini na Karibiani, 2009-2019




*Chanzo:* UN DESA, 2019c.

*Maelezo:* Ni muhimu kutambua kwamba kiwango kikubwa zaidi cha mabadiliko ya idadi ya watu kutoka 2009 hadi 2019 kina uwezekano mkubwa wa kutokea katika nchi zilizo na idadi ndogo ya watu.

Kwa kiasi kikubwa, Meksio ilikuwa nchi kubwa zaidi ya uhamaji katika Amerika ya Kusini na Karibiani (kielelezo cha 21). Karibu watu milioni 12 wa Meksiko waliishi nje ya nchi hiyo katika mwaka wa 2019. Pia Meksiko ni nchi ya pili ya asili ya wahamaji wengi ulimwenguni baada ya India. Wahamaji wengi wa Meksiko waliishi Marekani, ambayo inaendelea kuwa njia kubwa zaidi wa uhamiaji kutoka nchi hadi nchi ulimwenguni kote (kielelezo cha 22). Nchi zingine nyingi za Amerika ya Kati - kama El Salvador, Guatemala na Honduras - pia zina idadi kubwa ya wahamiaji nchini Marekani, kama zilizvyo nchi za Amerika ya Kusini kama vile Colombia, Ecuador, Brazil na Peru. Idadi kubwa ya wahamiaji wa Amerika ya Kusini waliishi mahali pengine katika ukanda huo. Colombia na Jamuhuri ya Bolivaria ya Venezuela zilikuwa na idadi kubwa ya pili na ya tatu ya wahamaji katika ukanda huo katika mwaka wa 2019 (milioni 2.9 na milioni 2.5 mtawalia). Karibu Wavenezuela milioni 1 waliishi Colombia, ikionyesha ufurushwaji unaovuka mipaka wa hivi karibuni kutoka Jamuhuri ya Bolivaria ya Venezuela.

Katika mwaka wa 2019, Argentina ilikuwa mwenyeji wa idadi kubwa zaidi ya watu waliozaliwa nje ya nchi katika ukanda huo (ikiwa na zaidi ya wahamiaji milioni 2), hasa kutoka nchi jirani kama Paraguay na Taifa la Bolivia. Jamhuri ya Bolivara ya Venezuela ilifuata na idadi kubwa zaidi ya wahamiaji, kisha Colombia na Meksiko. Katika mwaka wa 2019, Meksiko ilikuwa na wahamiaji zaidi ya 760,000 waliozaliwa Marekani. Kama inavyoonyeshwa katika kielelezo cha 21, kati ya nchi 20 kuu za uhamiaji katika ukanda huo, Costa Rica ilikuwa na sehemu kubwa zaidi ya wahamiaji katika idadi ya watu wake wote (8%), kwa sababu ya uhamaji wa muda mrefu kutoka nchi jirani ya Nicaragua. Nchi zingine katika ukanda huu zilizo nje ya 20 kuu zilikuwa na idadi kubwa ya wahamiaji kama sehemu ya idadi ya watu wote, kama Belize iliyokuwa na asilimia 15.

## Kielelezo cha 21. Nchi 20 za juu za wahamiaji katika Amerika ya Kusini na Karibiani katika mwaka wa 2019




*Chanzo:* UN DESA, 2019a.

*Maelezo ya 1:* Wingi wa idadi ya watu uliotumika kukokotoa asilimia ya wahamiaji na wahamaji unategemea idadi jumla ya wakazi wa nchi hiyo kulingana na UN DESA, ambayo inajumuisha watu waliozaliwa nje ya nchi.

*Maelezo ya 2:* "Mhamiaji" hurejelea wahamiaji walio wazaliwa wa kigeni wanaokaa nchini humo. "Mhamaji" hurejelea watu waliozaliwa nchini ambao walikuwa wakiishi nje ya nchi yao ya kuzaliwa katika mwaka wa 2019.

Jamhuri ya Bolivara ya Venezuela kwenda Colombia). Njia hizi za uhamiaji zinawakilisha mkusanyiko wa harakati za wahamaji zinazohusisha nchi za Amerika ya Kusini na Karibiani kwa muda mrefu na zinatoa picha ya jinsi mikondo ya uhamiaji imebadilika na kuwa idadi kubwa ya wazaliwa wa kigeni katika nchi mahususi walikokwenda.

Kielelezo cha 22. Njia 10 kuu za uhamiaji zinazohusisha nchi za Amerika ya Kusini na Karibiani, 2019




*Chanzo:* UN DESA, 2019a.

*Maelezo:* Njia za uhamiaji zinawakilisha mkusanyiko wa harakati za wahamaji kwa muda mrefu na hutoa picha ya jinsi mikondo ya uhamiaji imebadilika na kuwa idadi kubwa ya wazaliwa wa kigeni katika nchi mahususi walikokwenda.

Katika mwaka wa 2018, Jamhuri ya Bolivara ya Venezuela ilikuwa nchi kubwa ya chanzo cha madai ya hifadhi duniani, ikiwa na madai ya hifadhi zaidi ya 340,000 yaliyowasilishwa kufikia mwishoni mwa mwaka. Hili ni ongezeko kubwa kutoka mwaka wa 2017, wakati madai mapya ya hifadhi yalizidi 100,000 kidogo tu. Inakadiriwa kuwa raia wa Venezuela milioni 3 walikuwa wameondoka nchini mwao mwishoni mwa 2018 kwa sababu kadhaa, ikiwa ni pamoja na vurugu, mateso na mzozo wa kiuchumi/kisiasa. Idadi kubwa ya watu wa Venezuela waliofurushwa nje ya nchi waliishi Colombia (karibu milioni 1). Colombia ilikuwa nchi kubwa zaidi ya asili ya wakimbizi katika ukanda wa Amerika ya Kusini na Karibiani. Wakimbizi wengi kutoka Colombia walipewa makazi katika nchi jirani za Jamuhuri ya Bolivara ya Venezuela na Ecuador. El Salvador ilikuwa nchi kubwa ya pili ya asili ya wakimbizi na chanzo kikubwa cha pili cha madai mapya ya hifadhi katika ukanda huo, baada ya Jamhuri ya Bolivaria ya Venezuela. El Salvador ilifuatwa na Haiti, ambayo ilikuwa asili kuu ya tatu ya wakimbizi katika Amerika ya Kusini na Karibiani mwishoni mwa 2018.

## Kielelezo cha 23. Nchi 10 kuu za Amerika ya Kusini na Karibiani kulingana na jumla ya wakimbizi na waomba hifadhi, 2018




*Chanzo:* UNHCR, n.d.

*Maelezo:* "Waliokaribishwa" hurejelea wale wakimbizi na waomba hifadhi kutoka nchi zingine ambao wanaishi katika nchi inayopokea (upande wa kulia wa kielelezo); "Nje ya nchi" hurejelea wakimbizi na waomba hifadhi wanaotoka kwa nchi hiyo ambao wako nje ya nchi yao ya asili. Nchi 10 za juu zinategemea data ya 2018 ambayo inakokotolewa kwa kuchanganya wakimbizi na waomba hifadhi ndani na kutoka nchi zingine.

Wafurushwaji wengi wapya wa ndani wa Amerika ya Kusini na Karibiani walijipata katika hali hiyo kutokana na vurugu na migogoro, si majanga. Kielelezo cha 24 kinaonyesha nchi 20 kuu katika ukanda huo zilizo na ufurushwaji mpya mkubwa wa ndani uliosababishwa na migogoro na vurugu na majanga. El Salvador na Colombia zilirekodi idadi kubwa zaidi ya wakimbizi wapya wa ndani huko Amerika ya Kusini na Karibiani mnamo 2018, huku ufurushwaji mwingi ukichochewa na vurugu na migogoro katika nchi zote mbili. Kulikuwa na visa vipya 246,000 vya ufurushwaji vilivyohusiana na migogoro nchini El Salvador (karibu 4% ya idadi ya watu wa nchi hiyo), wakati Colombia ilirekodi 145,000. Ikiwa na visa vipya 11,000 vya ufurushwaji kutokana na vurugu na migogoro, Meksiko ilirekodi idadi kubwa zaidi ya tatu katika ukanda huo. Visa vingine vya ufurushwaji mkubwa wa ndani katika ukanda huo vilisababishwa na majanga, huku Brazil ikipata idadi kubwa zaidi (86,000), ikifuatwa na Colombia (67,000) na Cuba (52,000). Wakati idadi ya visa vya ufurushwaji mpya wa ndani katika Amerika ya Kusini na Karibiani ni vya chini sana ikilinganishwa na Afrika, hizi ndizo kanda mbili tu ambapo idadi ya wakimbizi wapya kutokana na vurugu na migogoro ni kubwa kuliko ile inayosababishwa na majanga.

## Kielelezo cha 24. Nchi 20 kuu za Amerika ya Kusini na Karibiani kulingana na ufurushwaji mpya wa ndani (janga na mgogoro), 2018




*Chanzo:* IDMC, n.d; UN DESA, 2017.

*Maelezo:* Ufurushwaji mpya unarejelea idadi ya harakati za kufurushwa ambazo zilitokea mwaka wa 2018, si jumla ya idadi ya mkusanyiko wa IDP inayotokana na ufurushwaji unaotokea kwa muda mrefu. Takwimu mpya za ufurushwaji zinajumuisha watu ambao wamefurushwa zaidi ya mara moja na hazilingani na idadi ya watu waliofurushwa katika mwaka husika.

Ukubwa wa idadi ya watu uliotumika kukokotoa asilimia ya ufurushwaji mpya unaotokana na maafa na migogoro unatokana na jumla ya idadi ya wakazi wa nchi kulingana na makadirio ya idadi ya watu ya mwaka 2017 ya UN DESA, na asilimia inatolewa kwa madhumuni ya kutoa ufafanuzi tu.

## Sifa muhimu na maendeleo katika Amerika ya Kusini na Karibiani

### *Amerika Kusini*

**Machafuko ya kisiasa na kiuchumi katika Jamuhuri ya Bolivaria ya Venezuela yamesababisha moja ya mzozo mbaya zaidi wa kibinadamu ulimwenguni, ikihamisha mamilioni ya watu kutoka nchi hiyo.** Kufikia mwisho wa 2018, idadi ya Wavenezuela waliokimbia makazi yao ulimwenguni ilikuwa imezidi milioni 3;[256] kufikia katikati ya 2019, idadi hii ilikuwa imeongezeka hadi milioni 4.[257] Idadi kubwa ilikaribishwa katika nchi jirani kama vile Colombia, Peru, Ecuador, Argentina, Chile na Brazil, ingawa idadi inayoongezeka ya wananchi wa Venezuela pia inahamia nchi za Amerika ya Kati na Karibiani.[258] Colombia na Peru zilikuwa wenyeji wa idadi kubwa zaidi ya Wavenezuela mwishoni mwa 2018, zaidi ya watu milioni 1 na 500,000, mtawalia.[259] Huku uchumi ukiporomoka, mgogoro mbaya wa kiuchumi umeacha mamilioni ya watu wakishindwa kumudu mahitaji ya msingi kama chakula, dawa na vifaa vya matibabu. Hali mbaya ya mfumo wa huduma ya afya na ongezeko la viwango vya utapiamlo kati ya watoto kulisababisha vifo vingi katika mwaka wa 2018.[260] Shirika la Fedha Duniani lilikadiria kuwa mfumuko wa bei katika Jamuhuri ya Bolivaria ya Venezuela ungefikia zaidi ya asilimia milioni 1 katika mwaka wa 2018, na ungeongezeka hadi asilimia milioni 10 katika mwaka wa 2019.[261] Mbali na shida ya uchumi, Jamhuri ya Bolivaria ya Venezuela inakabiliwa na hali ya kisiasa inayoendelea kuwa mbaya, ambayo inahusisha kuwanyanyasa wapinzani wa kisiasa na kukamatwa kwa maelfu ya waandamanaji.[262]. Kuongezeka kwa uhalifu unaohusisha vurugu nchini humo pia kunaendelea kuwalazimisha watu zaidi kutafuta ulinzi katika nchi zingine. Maombi ya hifadhi yaliyowasilishwa na Wavenezuela wanaofika Marekani, kwa mfano, yalifikia karibu 28,000 mwishoni mwa Juni 2018.[263]

**Uhamiaji ndani ya ukanda huko Amerika ya Kusini ni muhimu sana, huku idadi kubwa ya wahamiaji wa kimataifa wanahama ndani ya eneo hilo.** Wahamiaji wengi katika nchi kama vile Argentina na Jamuhuri ya Bolivaria ya Venezuela, nchi mbili zilizo na idadi kubwa zaidi ya wahamiaji wa kimataifa huko Amerika Kusini katika mwaka wa 2019, walikuwa wanatoka katika ukanda huo.[264] Wahamiaji wa kimataifa wa Argentina walikuwa hasa kutoka Paraguay, Taifa la Wingi-utaifa la Bolivia na Chile, wakati wale wa Jamhuri ya Bolivaria ya Venezuela walikuwa hasa kutoka Kolombia.[265]Idadi kubwa ya watu waliozaliwa nje nchini Chile pia inajumuisha wahamiaji kutoka nchi za Amerika Kusini kama vile Peru, Argentina na Taifa la Wingi-taifa la Bolivia.[266] Mikataba ya Makazi iliyopitishwa na Soko la Pamoja la Kusini (MERCOSUR) - taasisi ya kiuchumi na kisiasa iliyoundwa na Argentina, Brazil, Paraguay, Uruguay na Jamhuri ya Bolivaria ya Venezuela[267] - imetekeleza jukumu kubwa katika kuimarisha uhamiaji wa wafanyikazi ndani ya ukanda, na wakati kwa wakati huo kupunguza uhamiaji usio halali ndani ya ukanda huo.[268] Makubaliano haya yanaruhusu raia wa MERCOSUR kukaa na kufanya kazi katika Nchi wanachama kwa kipindi cha miaka miwili, mradi hawana

256 IOM, 2018e.
257 UNHCR, 2019d.
258 UNHCR, 2019a.
259 keshatajwa.
260 OHCHR, 2018a.
261 Werner, 2018; Reuters, 2018.
262 Human Rights Watch, 2019
263 UNHCR, 2019a.
264 UN DESA, 2019a.
265 keshatajwa.
266 keshatajwa.
267 Chatzky, 2019.
268 Acosta, 2016; Aimsiranun, 2018.

rekodi ya jinai na wanaweza kuthibitisha uraia wao.[269] Kutokana na hayo, wahamiaji wenye ujuzi wa chini na wenye ujuzi kiasi katika sekta kama vile kilimo, uvuvi na kazi za nyumbani, ambao ndio wahamiaji wengi wafanyikazi huko Amerika Kusini,[270] wameweza kusafiri na kufanya kazi kwa uhuru zaidi katika ukanda huu mdogo.

**Mamilioni ya watu wa Amerika Kusini wanaendelea kuishi nje ya ukanda huo, na wakati huo huo idadi ya wahamiaji kutoka nje ya ukanda huo inakua polepole.** Uhamaji kutoka Amerika Kusini unahusiana sana na kazi, ukichochewa na mizozo ya kiuchumi na ukosefu wa utulivu wa kisiasa katika nchi asili.[271] Nchi ya Marekani ndiyo nchi wanakokwenda wahamiaji wengi zaidi kutoka Amerika Kusini, ikiwa na wahamiaji milioni 3.4.[272] Nchi zilizo na idadi kubwa zaidi ya wahamaji wanaoishi nje ya Amerika Kusini katika mwaka wa 2019 zilikuwa Kolombia (karibu milioni 1.57), ikifuatiwa na Brazil (milioni 1.5) na Ecuador (karibu milioni 1).[273] Wakati huo huo, kupunguzwa kwa fursa katika masoko ya ajira nje ya nchi, na pia kuboreshwa kwa hali ya uchumi katika ukanda huo mdogo, kunachangia kurudi kwa wahamiaji wengi wa Amerika Kusini na kupungua kwa kiwango cha uhamiaji wa kanda nyingi.[274] Idadi ya wahamiaji huko Amerika Kusini kutoka nje ya ukanda huo pia inaongezeka. Kwa mfano, tangu 2010, kwa jumla watu wengi wamehama kutoka EU kwenda Amerika ya Kusini na Karibia, kuliko kutoka Amerika ya Kusini na Karibia kwenda EU.[275] Wengi wa watu hawa si wahamiaji wanaorejea, lakini ni raia wa EU, hasa kutoka Uhispania, Italia na Ureno.[276] Wahamiaji kutoka nchi hizi tatu asili kwa pamoja waliwakilisha idadi ya zaidi ya watu 800,000 huko Amerika Kusini katika mwaka wa 2019.[277] Wahaiti, Wacuba na Wadominika wengi zaidi pia wamehamia Amerika Kusini.[278]

**Ingawa ni mahususi kwa nchi fulani, migogoro na vurugu huchangia ufurushwaji wa watu na uhamiaji katika ukanda huo mdogo.** Huko Kolombia, zaidi ya watu milioni 5.7 walibaki wakimbizi wa ndani kufikia mwisho wa 2018 - idadi kubwa ya pili ya IDP ulimwenguni.[279] Katika mwaka huo huo, karibu Wakolombia 139,000 walikuwa wakiishi kama wakimbizi au katika hali kama za wakimbizi nje ya nchi, idadi ikiwa imepungua kutoka zaidi ya 190,000 mnamo 2017 na karibu 300,000 mnamo 2016.[280] Kulikuwa na Wakolombia karibu milioni 1 katika Jamuhuri ya Bolivaria ya Venezuela na Ecuador katika mwaka wa 2019. Hata hivyo, wakati Colombia inapoanza kubadilika kutoka kwa miongo mitano ya vurugu kwa kuwa mazungumzo ya amani mwishoni mwa 2016 na 2017, kuzorota kwa hali za kiuchumi na kijamii katika Jamuhuri ya Bolivaria ya Venezuela kunawafanya Wakolombia wengi kurudi nyumbani.[281]

### *Amerika ya Kati na Karibiani*

**Uhamiaji kuelekea kaskazini unaendelea kuwa mwenendo unaotawala katika Amerika ya Kati, Meksiko na Karibiani.** Meksiko inabaki kuwa nchi asili ya wahamiaji inayojulikana, huku maelfu wakihama hasa kwenda Marekani kila mwaka. Pia ni nchi muhimu ya mpito kwa wahamiaji wanaosafiri kuelekea

269 keshatajwa.
270 Aimsiranun, 2018.
271 IOM, 2017.
272 UN DESA, 2019a.
273 keshatajwa.
274 IOM, n.d.e.
275 IOM, 2015.
276 keshatajwa.
277 UN DESA, 2019a.
278 IOM, 2017.
279 IDMC, 2019.
280 UNHCR, 2018a, 2019a.
281 UNHCR, 2019a.

kaskazini kwenye mpaka wa kusini wa Marekani. Hata hivyo, katika muktadha wa kuboresha hali ya uchumi na kuongezeka kwa viwango vya elimu nchini, pamoja na utekelezaji mkali wa uhamiaji nchini Marekani, Meksiko ni nchi inayozidi kuwa muhimu wanakofika wahamiaji wa kimataifa, baadhi wakiwa wale ambao walishindwa kuingia Marekani kama walivyopanga hapo awali.[282] Idadi ya watu waliozaliwa nje ya nchi huko Meksiko iliongezeka kutoka karibu 970,000 katika mwaka wa 2010 hadi zaidi kidogo ya milioni 1 katika mwaka wa 2019 - wengi wao wakitoka Amerika Kaskazini, lakini pia sehemu kubwa zaidi walikuwa wahamiaji kutoka nchi zingine za Amerika ya Kusini na Karibiani.[283] Hata hivyo, Marekani ndipo mahali panapopendwa sana na wahamiaji wa Amerika ya Kati, huku zaidi ya asilimia 90 ya wahamiaji wa Amerika ya Kati wakiishi Marekani katika mwaka wa 2017.[284] Vurugu na ukosefu wa usalama, umaskini na kuungana kwa familia bado ni vichocheo muhimu vya uhamaji kutoka Amerika ya Kati.[285] Njia mashuhuri zaidi za uhamiaji ndani ya ukanda zinahusisha watu wa Nicaragua, Panama na wengine wa Amerika ya Kati wanaohamia Costa Rica kwa kazi ya muda au ya kudumu, na watu wa Amerika ya Kati (hasa kutoka Honduras, Guatemala na El Salvador) wanahamia Belize kwa sababu ya ukosefu wa utulivu na ukosefu wa nafasi za ajira.[286] Katika Karibiani, njia maarufu zaidi za wahamiaji ndani ya ukanda zinajumuisha Wahaiti wanaohamia Jamhuri ya Dominika.[287] Pia kuna idadi inayoongezeka ya wahamiaji kutoka kanda zingine, pamoja na wale kutoka Afrika, wanaopitia Amerika ya Kati kuelekea Marekani.[288]

**Mtiririko wa uhamiaji usio halali katika eneo hilo ni wenye nguvu, ukizidi kuwa changamano na anuwai.** Wameksiko waliwakilisha idadi kubwa ya wahamiaji wasio halali ambao kwa miaka mingi wanakamatwa wanapojaribu kuvuka mpaka wa Marekani- Meksiko. Hata hivyo, katika miaka ya hivi karibuni, wasiwasi wa watu wa Amerika ya Kati unaotokana na eneo la "Pembetatu ya Kaskazini" la Guatemala, Honduras na El Salvador ulizidi ule wa Wameksiko katika mpaka wa Marekani na Meksiko.[289] Wakitoroka vurugu, mateso na umaskini, maelfu ya wahamiaji kutoka Amerika ya Kati walitembea maelfu ya maili kuelekea kwenye mpaka wa Meksiko na Marekani. Kama unavyoitwa, "msafara wa wahamiaji" wa hivi karibuni ilianzia Honduras mnamo Oktoba 2018. Wakati wahamiaji wa Honduras walipokuwa wakielekea kwenye mpaka wa Marekani na Meksiko, maelfu zaidi ya wahamiaji kutoka nchi kama El Salvador na Guatemala walijiunga na kikundi hicho. Kufikia mwisho wa 2018, msafara wa wahamiaji ulikuwa umetuna kwa maelfu ya wahamiaji, wengi wao wakiwa watoto.[290] Mambo kadhaa yaliwasukuma watu kujiunga na msafara huo, ikiwa ni pamoja na kutoroka vurugu katika nchi kama Honduras, kukimbia umaskini uliokithiri na kutafuta nafasi bora za kiuchumi. Msafara wa wahamiaji ulisababisha mjadala mkali wa kisiasa huko Marekani na kuichochea Serikali kupeleka zaidi ya maafisa wa jeshi 7,000 wa kudumu kwenye mpaka na Meksiko.[291] Mwanzoni mwa 2019, wahamiaji elfu chache waliofanikiwa kufikia mpaka wa Marekani walikuwa wamekamatwa. Wengine walipokea viza za kibinadamu za Meksiko, wakati wengine walifukuzwa nchini au walichagua kurudi katika nchi zao za asili.[292] Mamia ya wahamiaji wamebaki Tijuana, Meksiko. Mnamo Februari 2019, msafara wa Wacuba na Wahaiti, pamoja na baadhi ya Waafrika na Waasia, uliingia Panama kutoka Colombia na baadaye ukafika Meksiko. Katika mabadiliko kutoka kwa sera yake wazi zaidi iliyotangazwa mwanzoni mwa 2019, Meksiko ilianza kuwazuia wahamiaji kutoka Amerika ya Kati mnamo Aprili 2019.[293]

282 Dominguez-Villegas, 2019.
283 UN DESA, 2019a.
284 keshatajwa.
285 FAO, 2018a; CEPAL, 2019.
286 ILO, 2016.
287 keshatajwa.
288 Solomon, 2019.
289 Bialik, 2019.
290 UNICEF, 2018.
291 Meissner, 2018.
292 Dominguez-Villegas, 2019; BBC, 2019.
293 Cullell, 2019.

**Usafirishaji haramu wa wahamiaji pia ni sifa kuu ya ukanda huo mdogo, watu wanapojaribu kukwepaa udhibiti wa mpakani katika Amerika ya Kati na Meksiko.** Kwenye mpaka wa Marekani na Meksiko, mitandao ya magendo ni tasnia yenye faida inayosimamiwa na vikundi vya uhalifu wa kimataifa.[294] Inajulikana kuwa wahamiaji wanaosafirishwa kimagendo mara nyingi huathiriwa na vitendo vya kiulafi kuanzia madai ya hongo hadi utekaji nyara wa watu wengi na kughusubiwa.[295] Wahamiaji pia wamekuwa wakiuawa, kunyanyaswa kimwili na kingono, kuteswa na kutoweka; hivi ndivyo hali ilivyo hasa huko Meksiko, ambapo imeripotiwa kuwa baadhi ya mitandao ya magendo mara nyingi husimamiwa na mashirika ya biashara ya dawa za kulevya.[296] Usafirishaji kimagendo wa wahamiaji pia umewezesha uhamiaji usio halali ndani na kupitia nchi za Amerika ya Kati kama vile Guatemala, hasa na wahamiaji wanaoelekea Marekani. Kihistoria, raia wa Guatemala na wahamiaji wa kimataifa wanaopitia Guatemala walitegemea magendo sana, yanayojulikana katika eneo hilo kama Coyoterismo, ili kufika walikokuwa wakienda.[297] Kuna wasiwasi unaoongezeka huko Amerika ya Kusini kwamba utaratibu wa viza unatumiwa kuwezesha wahamiaji kuingia katika nchi za ukanda huo kabla ya kusafirishwa kimagendo kwenda kwingineko.[298] Zaidi ya hayo, idadi kubwa ya watu wamekufa wakati wakifanya safari za uhamiaji zisizo halali katika Amerika ya Kati.[299]

**Hali za kijamii na kiuchumi na vurugu jumla katika kiwango cha jamii katika nchi kadhaa za Amerika ya Kati huchangia uhamiaji, hasa wa idadi kubwa ya wanawake na watoto.** Kumekuwepo na ongezeko kubwa la idadi ya madai ya hifadhi kutoka Amerika ya Kati. Maombi kutoka Amerika ya Kati na Meksiko yalichangia asilimia 54 ya madai yote ya hifadhi nchini Marekani katika mwaka wa 2017.[300] Wahamiaji kutoka El Salvador walikuwa waombaji wengi (zaidi ya 33,000), wakifuatwa na wale kutoka Guatemala (karibu 33,000) na Jamuhuri ya Bolivaria ya Venezuela (27,500).[301] Kumekuwepo na ongezeko la idadi ya vitengo vya familia vilivyokamatwa katika mpaka wa Marekani na Meksiko; katika mwaka wa 2018, karibu wanafamilia 163,000 walikamatwa, wakichangia asilimia 35 ya watu wote waliokamatwa mpakani na zaidi ya mara tatu ya idadi ya familia zilizoshikwa katika mwaka wa 2017.[302] Watoto wasiosindikizwa wanabaki kuwa sehemu muhimu ya mtiririko wa uhamiaji usio halali, kukiwa na karibu watoto 54,000 wasiosindikizwa waliokamatwa mpakani katika mwaka wa 2018.[303]

**Mabadiliko ya tabianchi yanaonekana kuathiri usafiri wa binadamu katika Amerika ya Kati na Karibiani, ingawa kutenga vichocheo vya kimazingira vya uhamiaji bado ni kazi ngumu.** Kulingana na Jopo la Serikali Mbalimbali kuhusu Mabadiliko ya Tabianchi (IPCC), kuongezeka kwa joto ulimwenguni kunahusishwa na uhamiaji katika jamii zinazotegemea kilimo.[304] Katika mwaka wa 2018, hali ya ukame huko Amerika ya Kati ilichangia upotezaji wa asilimia 82 ya mihindi na miharagwe huko Honduras, na kuwaweka karibu watu milioni 3 katika hatari ya ukosefu wa chakula.[305] Katika nchi kama El Salvador, Guatemala na Honduras, idadi kubwa ya watu huishi vijijini na hutegemea sana kilimo kujichumia riziki, hali inayowafanya wawe katika hatari zaidi ya kuathiriwa na mabadiliko ya mazingira kama vile ukame.[306] Huenda athari za mabadiliko ya tabianchi zilihusika katika mienendo ya hivi karibuni ya uhamiaji huko Amerika ya Kati,

294 Sanchez, 2018.
295 keshatajwa.
296 keshatajwa.
297 Velasco, 2018; Sanchez, 2018.
298 keshatajwa.
299 IOM, n.d.d.
300 UNHCR, 2019a
301 keshatajwa.
302 Bialik, 2019.
303 keshatajwa
304 IPCC, 2018.
305 Palencia, 2014; FAO, 2018b.
306 CEPAL, 2019.

huku idadi kubwa ya watu ambao walikuwa sehemu ya msafara, kwa mfano, wakihusika na shughuli kama vile kilimo, misitu, ufugaji wa ng'ombe na uvuvi kabla ya kuanza safari ya kuelekea kaskazini.[307] Wakati huo huo, Karibiani iko katika eneo linalokabiliwa mara kwa mara na mitetemeko ya ardhi na hatari za majanga yanayohusiana na tabianchi. Nchi za Karibiani ni miongoni mwa zile zilizo katika hatari zaidi ya kupatwa na majanga ya asili na mabadiliko ya tabianchi. Huku sehemu kubwa ya watu wa Karibiani wakiwa wanaishi katika maeneo yasiyokingwa kutokana na ongezeka la usawa wa bahari, majanga ya hivi karibuni yamesababisha watu wengi kuhama makwao na vifo. Kimbunga Irma, kwa mfano, ambacho kilikumba sehemu za Karibiani na Kaskazini mwa Amerika, kilikuwa janga kubwa zaidi ulimwenguni katika mwaka wa 2017, na kilihamisha zaidi ya watu milioni 2 katika kanda zote mbili.[308] Mbali na kupoteza maisha, kimbunga hicho kiliacha uharibifu wa mali na miundombinu katika maeneo kadhaa ya Karibiani, pamoja na Puerto Rico, Cuba na Visiwa vya Virgin vya Marekani.[309] Pia visiwa vingi vya Karibiani hutegemea sana sekta kama vile kilimo na utalii, na majanga yameathiri sana uchumi wao. Jinsi idadi na ukali wa majanga haya unavyoongezeka kutokana na mabadiliko ya tabianchi, inatarajiwa kwamba hatari za kiafya na ukosefu wa chakula vitakithiri, pamoja na kuongezeka kwa uharibifu wa bioanuwai.[310]

**Uhamaji kwenda Marekani ni sifa muhimu ya Karibiani, huku wahamiaji waliozaliwa Karibia wakiwa kati ya vikundi vikubwa zaidi nchini humo.** Mahusiano ya kihistoria kati ya Karibiani na Marekani, na pia siasa za kijiografia, vimeathiri sana uhamiaji kuelekea kaskazini. Katika mwaka wa 2017, asilimia 10 ya wahamiaji wote nchini Marekani walikuwa kutoka Karibiani, na kuifanya kuwa kituo kikubwa zaidi cha wahamiaji kutoka Karibiani nje ya ukanda huo mdogo.[311] Vituo vingine vikuu ni pamoja na CKanada, Uhispania na Uingereza. Zaidi ya asilimia 65 ya wahamiaji wa Karibiani waliokuwa nchini Marekani katika mwaka wa 2019 walitoka nchi tano tu (Haiti, Trinidad na Tobago, Cuba, Jamaika na Jamhuri ya Dominika), huku wengi wao wakitoka Cuba.[312] Ongezeko la idadi ya Wacuba huko Marekani baada ya miaka ya katikati ya 1960 lilitokana kimsingi na sheria mbili ambazo zilitoa hadhi ya kipekee kwa wahamiaji kutoka Cuba: Sheria ya Marekebisho ya Cuba ya 1966 na Mkataba wa Uhamiaji wa Marekani na Cuba wa 1994 na 1995, ambayo iliwawezesha Wacuba (ambao walikuwa wamewasili Marekani kwa barabara) kupata makazi ya kudumu baada ya kuishi nchini humo kwa mwaka mmoja. Hii ilijulikana kama sera ya "wa baharini hawakubaliwi, wa nchi kavu wanakubaliwa".[313]

## Kaskazini mwa Amerika[314]

Uhamiaji huko Kaskazini mwa Amerika unatawaliwa na uhamiaji kuingia katika ukanda huo. Kama inavyoonyeshwa kwenye kielelzo cha 25, zaidi ya wahamiaji milioni 58.6 walikuwa wakiishi Kaskazini mwa Amerika kutoka maeneo anuwai katika mwaka wa 2019. Idadi hii imeongezeka kwa karibu milioni 3 tangu 2015, wakati karibu wahamiaji milioni 55.6 walikuwa wakiishi katika ukanda huo. Kundi kubwa zaidi lilikuwa kutoka Amerika ya Kusini na Karibiani (milioni 26.6), likifuatiwa na Asia (milioni 17.4) na Ulaya (milioni 7). Katika kipindi cha miaka 30 iliyopita, idadi ya wahamiaji huko Kaskazini mwa Amerika imeongezeka zaidi ya maradufu, ikisukumwa na uhamaji kutoka Amerika ya Kusini na Karibiani, na Asia, na pia ukuaji wa uchumi na utulivu wa kisiasa huko Kaskazini mwa Amerika.

307 IOM, 2018f.
308 IDMC, 2018a.
309 keshatajwa.
310 Otker-Robe, 2019.
311 Zong na Batalova, 2019.
312 UN DESA, 2019a.
313 CEPAL, United Nations na IOM, 2017; Zong na Batalova, 2019.
314 Tazama kiambatisho cha A kwa maelezo juu ya vijenzi vya Kaskazini mwa Amerika.

Idadi ya wahamiaji wa Kaskazini mwa Amerika wanaoishi katika ukanda huo au kwingineko ilikuwa ndogo sana ikilinganishwa na idadi ya watu waliozaliwa nje katika ukanda huo. Kinyume na kanda kama Asia na Afrika ambapo uhamiaji wa ndani ya ukanda unatawala, wahamiaji zaidi waliozaliwa Kaskazini mwa Amerika waliishi nje ya ukanda huo (karibu milioni 3) kuliko waliohamia kwingineko katika ukanda huo. (milioni 1.4).

Kielelezo cha 25. Wahamiaji kwenda, ndani ya na kutoka Kaskazini mwa Amerika, 1990–2019




*Chanzo:* UN DESA , 2019a.

*Maelezo:* "Wahamiaji kwenda Kaskazini mwa Amerika" hurejelea wahamiaji wanaoishi katika ukanda huo (yaani Kaskazini mwa Amerika) ambao walizaliwa katika moja ya kanda zingine (kwa mfano, Ulaya au Asia). "Wahamiaji ndani ya Amerika ya Kaskazini" hurejeleaa wahamiaji waliozaliwa katika ukanda huo (yaani Kaskazini mwa Amerika) na wanaoishi nje ya nchi yao ya kuzaliwa, lakini bado katika ukanda wa Kaskazini mwa Amerika. "Wahamiaji kutoka Kaskazini mwa Amerika" hurejelea watu waliozaliwa Kaskazini mwa Amerika ambao walikuwa wanaishi nje ya ukanda huo (kwa mfano, Ulaya au Afrika).

Kielelezo cha 26 kinaonyesha nchi zilizo na kiwango kikubwa zaidi cha mabadiliko ya idadi ya watu huko Kaskazini mwa Amerika kati ya 2009 hadi 2019. Mabadiliko ya idadi ya watu nchini Canada na Marekani yalikuwa katika ukuaji, huku Canada ikipata mabadiliko makubwa zaidi kwa wingi wa idadi ya watu katika mwongo mmoja uliopita (11%). Idadi ya watu wa Marekani pia ilipanuka wakati huo huo, ikiongezeka kwa karibu asilimia 7. Huko Canada, mabadiliko ya hivi karibuni ya idadi ya watu yamechochewa kwa kiasi kikubwa na uhamiaji, ambao unabaki kuwa kichocheo kikuu cha ukuaji wa idadi ya watu humo chini.

Kielelezo cha 26. Nchi zilizo na mabadiliko makubwa zaidi ya kiwango cha idadi ya watu huko Kaskazini mwa Amerika, 2009-2019




*Chanzo:* UN DESA, 2019a.

*Maelezo:* Ni muhimu kutambua kwamba kiwango kikubwa zaidi cha mabadiliko ya idadi ya watu kutoka 2007 hadi 2019 kina uwezekano mkubwa wa kutokea katika nchi zilizo na idadi ndogo ya watu.

Katika mwaka wa 2019, Marekani ilikuwa na idadi kubwa zaidi ya watu waliozaliwa nje ya nchi hiyo ulimwenguni, wakati Canada ilikuwa na idadi kubwa ya nane. Zaidi ya asilimia 86 ya idadi ya watu waliozaliwa nje katika ukanda huo waliishi Marekani. Kama inavyoonyeshwa kwenye kielelezo cha 27, sehemu ya idadi jumla ya watu wa Canada ambayo ilizaliwa nje ya nchi hiyo (ikiwa zaidi ya 21%) ilikuwa kubwa zaidi kuliko ile ya Marekani mnamo 2019 (15%). Canada pia ilikuwa na sehemu kubwa ya raia wake ambao walikuwa wamehama (kama asilimia ya idadi ya watu wote wanaoishi nchini humo) ikilinganishwa na Marekani.

Kielelezo cha 27. Nchi kuu za uhamiaji huko Kaskazini mwa Amerika mnamo 2019




*Chanzo:* UN DESA , 2019a.

*Maelezo ya 1:* Wingi wa idadi ya watu uliotumika kukokotoa asilimia ya wahamiaji na wahamaji unategemea idadi jumla ya wakazi wa nchi hiyo kulingana na UN DESA, ambayo inajumuisha watu waliozaliwa nje ya nchi.

*Maelezo ya 2:* “Mhamiaji” hurejelea wahamiaji walio wazaliwa wa kigeni wanaokaa nchini humo. “Mhamaji” hurejelea watu waliozaliwa nchini ambao walikuwa wakiishi nje ya nchi yao ya kuzaliwa katika mwaka wa 2019.

Kielelezo cha 28 kinaonyesha njia 10 kuu za uhamiaji zinazohusisha nchi za Kaskazini mwa Amerika, zinazowakilisha mkusanyiko wa harakati za uhamaji za muda mrefu na kutoa picha ya jinsi mikondo ya uhamiaji imebadilika kuwa idadi kubwa ya watu waliozaliwa nje ya nchi katika nchi mahususi walizokwenda. Njia zote kubwa zaidi za wahamiaji huko Kaskazini mwa Amerika zinahusisha wahamiaji ama kutoka Asia au Amerika ya Kusini na Karibiani, kwenda Marekani. Wahamiaji waliozaliwa Meksiko wanaunda kundi kubwa zaidi la wahamiaji, huku zaidi ya milioni 11 wakiishi Marekani katika mwaka wa 2019. Njia kuu zinazofuata za uhamiaji zinahusisha nchi za Asia zenye watu wengi, ikiwa ni pamoja na Uchina, India na Ufilipino. Baadhi ya njia kubwa zingine za uhamiaji kutoka Vietnamu, Jamhuri ya Korea na Cuba kwenda Marekani zilikua haraka baada ya migogoro au mabadiliko ya kisiasa katika nchi asili miaka mingi iliyopita.

## Kielelezo cha 28. Njia 10 kuu za uhamiaji zinazohusisha nchi za Kaskazini mwa Amerika, 2019




*Chanzo:* UN DESA, 2019a.

*Maelezo:* Njia za uhamiaji zinawakilisha mkusanyiko wa harakati za wahamaji kwa muda mrefu na hutoa picha ya jinsi mikondo ya uhamiaji imebadilika na kuwa idadi kubwa ya wazaliwa wa kigeni katika nchi mahususi walikokwenda.

Marekani ilikuwa mwenyeji wa wakimbizi na waomba hifadhi zaidi ya milioni 1 katika mwaka wa 2018. Kama inavyodhihirika kutoka kwa kielelezo cha 29, wengi wao, zaidi ya 700,000, walikuwa waomba hifadhi. Marekani pia ilibaki kuwa mpokeaji mkubwa zaidi wa madai mapya ya hifadhi ulimwenguni katika mwaka wa 2018 (zaidi ya 250,000), ingawa hii ilikuwa imepungua kutoka mwaka wa 2017, wakati madai ya hifadhi yalizidi 300,000. Waomba hifadhi huko Marekani walitoka katika nchi nyingi mbalimbali; hata hivyo, idadi kubwa zaidi ya watu ilikuwa kutoka El Salvador, Guatemala, Jamhuri ya Bolivaria ya Venezuela na Honduras. Pia Canada ni mwenyeji wa idadi kubwa ya wakimbizi na waomba hifadhi. Katika mwaka wa 2018, Canada ilikuwa mwenyeji wa wakimbizi na waomba hifadhi zaidi ya 190,000, ongezeko kutoka mwaka wa 2017, wakati nchi hiyo ilikuwa mwenyeji wa karibu 150,000. Mabadiliko ya hivi karibuni katika kuwapa makazi mapya wakimbizi huko Marekani na Canada yamejadiliwa katika sehemu ya "Sifa muhimu na maendeleo huko Kaskazini mwa Amerika" hapo chini.

## Kielelezo cha 29. Idadi ya wakimbizi na waomba hifadhi ndani na kutoka nchi za Kaskazini mwa Amerika, 2018




*Chanzo:* UNHCR, n.d.

*Maelezo:* "Waliokaribishwa" hurejelea wale wakimbizi na waomba hifadhi kutoka nchi zingine ambao wanaishi katika nchi inayopokea (upande wa kulia wa kielelezo); "Nje ya nchi" hurejelea wakimbizi na waomba hifadhi wanaotoka kwa nchi hiyo ambao wako nje ya nchi yao ya asili.

Ufurushwaji wote mpya wa ndani huko Kaskazini mwa Amerikaulitokana na majanga (kielelezo cha 30). Nchi ya Marekani ilirekodi idadi kubwa zaidi, ikiwa na zaidi ya watu milioni 1.2 wakikimbia makazi yao kutokana na vimbunga viwili vikubwa na moto wa mwituni. Kiwango cha ufurushwaji katika sehemu zilizobaki za Kaskazini mwa Amerika kilikuwa cha chini sana ikilinganishwa na Marekani; Kwa mfano, Canada ilirekodi visa 19,000 vipya katika mwaka wa 2018. Idadi ya ufurushwaji mpya wa ndani kutokana na majanga huko Kaskazini mwa Amerika ilikuwa ya pili tu baada ya Asia, ambayo ilipata ufurushwaji unaosababishwa na majanga zaidi kuliko migogoro (tazama kielelezo cha 12).

## Kielelezo cha 30. Nchi za juu za Kaskazini mwa Amerika kulingana na ufurushwaji mpya wa ndani (janga na mgogoro), 2018




*Chanzo:* IDMC, n.d; UN DESA, 2017.

*Maelezo:* Ufurushwaji mpya unarejelea idadi ya harakati za kufurushwa ambazo zilitokea mwaka wa 2018, si jumla ya idadi ya mkusanyiko wa IDP inayotokana na ufurushwaji unaotokea kwa muda mrefu. Takwimu mpya za ufurushwaji zinajumuisha watu ambao wamefurushwa zaidi ya mara moja na hazilingani na idadi ya watu waliofurushwa katika mwaka husika.

Wingi wa idadi ya watu uliotumika kukokotoa asilimia ya ufurushwaji mpya unaotokana na maafa na migogoro unatokana na jumla ya idadi ya wakazi wa nchi kulingana na makadirio ya idadi ya watu ya mwaka 2017 ya UN DESA, na asilimia inatolewa kwa madhumuni ya kutoa ufafanuzi tu.

## Sifa muhimu na maendeleo huko Kaskazini mwa Amerika

**Mienendo ya uhamiaji nchini Marekani inajulikana na viwango vya juu vya uhamiaji, hasa kutoka Amerika ya Kusini na Asia, ingawa idadi ya wahamiaji wa kimataifa inaendelea kubadilika.** Idadi ya watu waliozaliwa nje ya Marekani iliongezeka kwa asilimia 5 kutoka 2015 hadi 2019, na kufikia karibu watu milioni 51.[315] Kufikia mwaka wa 2019, wahamiaji waliozaliwa Meksiko bado walikuwa idadi kubwa zaidi ya watu waliozaliwa nje ya nchi wanaoishi Marekani, wakiwwa zaidi ya milioni 12.4, wakichangia karibu asilimia 22.7 ya wahamiaji wote nchini Marekani.[316] Hata hivyo, kihistoria, wakati Wameksiko wamekuwa na idadi kubwa zaidi ya wahamiaji wanaokwenda Marekani (angalau tangu 1970), idadi yao imepungua katika miaka michache iliyopita.[317] Waliowasili hivi karibuni wametoka Asia - hasa India, Uchina na Ufilipino - na pia kutoka nchi zingine za Amerika ya Kusini na Karibiani, kama vile Jamhuri ya Dominika, Cuba na El Salvador.[318] Katika mwaka wa 2019, Uchina ilikuwa asili ya idadi kubwa ya pili ya wahamiaji waliokwenda Marekani, na inakadiriwa kuwa Asia itakuwa ukanda wa asili kubwa zaidi ifikapo mwaka 2055.[319] Njia kubwa zaidi ya uhamiaji kwa Waasia wanaohamia Marekani ni kupitia viza zinazofadhiliwa na familia,[320] ingawa wengi pia ni wanafunzi; kulikuwa na zaidi ya wanafunzi wa kimataifa 360,000 wa Kichina nchini Marekani katika mwaka wa masomo 2017/2018.[321]

**Idadi ya wahamiaji nchini Canada inaendelea kuongezeka, ikiwakilisha asilimia inayoongezeka ya idadi ya watu wote wa nchi hiyo.** Katika mwaka wa 2000, watu waliozaliwa nje ya nchi waliwakilisha karibu asilimia 18 ya idadi ya watu wote wa Canada, wakiongezeka hadi karibu asilimia 19 mnamo 2005, karibu asilimia 20 katika mwaka wa 2010 na zaidi ya asilimia 21 katika mwaka wa 2019.[322] Hata hivyo, wakati wahamiaji nchini Canada kimsingi wametoka nchi za Ulaya hapo zamani, mchanganyiko wa idadi ya watu waliozaliwa nje ya nchi hiyo umebadilika na kujumuisha idadi kubwa ya wahamiaji kutoka nchi za Asia. Kwa mfano, katika mwaka wa 2000, nchi kubwa ya asili ya wahamiaji wa kimataifa huko Canada ilikuwa Uingereza (608,000), ikifuatwa na Uchina (412,000), India (319,000) na Italia (315,000). Kufikia 2019, India na Uchina zilikuwa zimeipiku Uingereza kama nchi mbili kubwa asili, zikiwa na karibu wahamiaji 709,000 na karibu 700,000 mtawalia.[323] Nchi zingine za Asia kama Jamhuri ya Kiislamu ya Iran pia zilikuwa katika nchi 10 kuu zenye idadi kubwa zaidi ya watu katika jumla ya watu milioni 7.9 wa Canada waliozaliwa nje ya nchi katika mwaka wa 2019.[324] Katika mwaka wa 2017, Canada ilisajili wakazi wapya wa kudumu zaidi ya 286,000, huku India, Ufilipino na Uchina zikiwakilisha nchi tatu za juu za asili.[325]

**Idadi inayokadiriwa ya wahamiaji wasio halali nchini Marekani inadhaniwa kuwa ya chini kuliko miaka kumi iliyopita, lakini bado ni kubwa zaidi ikilinganishwa na Canada.** Wahamiaji wasio halali wanaokadiriwa kuwa milioni 10.5 walikuwa wakiishi Marekani katika mwaka wa 2017, wakichangia asilimia 3.2 ya idadi ya watu wote.[326] Idadi ya wahamiaji wasio halali imekuwa ikipungua, ikishuka kutoka idadi

315 UN DESA, 2019a.
316 keshatajwa.
317 Zong, Batalova na Burrows, 2019.
318 UN DESA, 2019a.
319 Radford, 2019; UN DESA, 2019a.
320 Malik, 2015.
321 IIE, 2018.
322 UN DESA, 2019a.
323 keshatajwa.
324 keshatajwa.
325 IRCC, 2018.
326 Krogstad, Passel na Cohn, 2019.

ya juu ya milioni 12.2 katika mwaka wa 2007.[327] Kwa mara ya kwanza, Wameksiko walikuwa chini ya nusu (47%) ya wahamiaji wote wasiosajiliwa Marekani.[328] Idadi ya wahamiaji wasio halali wa Amerika ya Kati - wengi kutoka nchi za Pembetatu ya Kaskazini ya El Salvador, Guatemala na Honduras - iliongezeka kutoka milioni 1.5 katika mwaka wa 2007 hadi milioni 1.9 katika mwaka wa 2017.[329] Idadi kubwa ya wahamiaji watu wazima wasio halali nchini Marekani si wageni wapya; zaidi ya asilimia 65 ya watu wazima katika mwaka 2017 walikuwa wameishi Marekani kwa zaidi ya miaka 10.[330] Wahamiaji wasio halali wanaweza kuingia nchini humo bila idhini; hata hivyo, idadi kubwa ni watu waliokaa zaidi ya muda ulioidhinishwa kwenye viza ambao mwanzoni waliingia Marekani kwa njia halali. Kwa mfano, katika mwaka wa fedha wa 2018, kulikuwa na zaidi ya wageni 600,000 ambao walikaa zaidi ya muda ulioidhinishwa na viza zao huko Marekani.[331] Canada pia ina idadi kubwa ya wahamiaji wasio halali, ingawa makadirio yanatofautiana sana, na ni vigumu kupata idadi sahihi. Hata hivyo, kwa miaka miwili kabla ya Juni 2019, zaidi ya wahamiaji 45,000 waliripotiwa kuvuka kwenda Canada kwa njia zisizo halali.[332]

**Marekani na Canada zimetoa makazi mapya kwa idadi kubwa ya wakimbizi, zikiwakilisha nchi mbili zilizotoa makazi mapya mengi zaidi duniani.** Katika mwaka wa 2018, Canada ilitoa makazi mapya kwa wakimbizi wengi zaidi kuliko Marekani, ikiwa mara ya kwanza ambapo Marekani haijaongoza duniani. Kati ya wakimbizi 92,400 waliopewa makazi mapya kote ulimwenguni katika mwaka wa 2018, Canada ilikaribisha karibu 28,000, wakati Marekani ilichukua wanaopungua 23,000 kidogo.[333] Idadi ya wakimbizi waliopewa makazi mapya nchini Marekani imekuwa ikipungua kwa miaka miwili iliyopita; kwa mfano, katika mwaka wa 2016, Marekani ilikubali karibu wakimbizi 100,000.[334] Idadi hii ilipungua sana hadi 33,000 katika mwaka uliofuata.[335] Kumekuwepo pia na ongezeko kubwa la idadi ya raia wa Marekani wanaoomba hifadhi nchini Canada tangu mwaka 2016. Katika mwaka wa 2017 pekee, zaidi ya raia 2,500 wa Marekani waliomba hifadhi nchini Canada,[336] mara sita idadi ya maombi yaliyotolewa katika mwaka wa 2016 na idadi kubwa zaidi iliyorekodiwa tangu Shirika la Canada la Uhamiaji, Wakimbizi na Uraia (IRCC) lianze kuripoti juu ya idadi ya waomba hifadhi zaidi ya miongo miwili iliyopita.[337] Maombi mengi ya hifadhi kutoka kwa raia wa Marekani yalifanywa na watoto wa wazazi wasio na ukazi wa Marekani.[338]

**Sera za uhamiaji nchini Marekani zimeimarishwa, na kupunguza kasi ya mtiririko wa uhamiaji na wanaoingia kwa sababu za kibinadamu.** Kwa mfano, katika mwaka wa 2018, kwa jumla utoaji wa viza kwa wahamiaji na wasio wahamiaji ulipungua kwa mwaka wa pili mfululizo.[339] Zaidi ya viza milioni 10 zisizo za wahamiaji zilitolewa katika mwaka wa 2016; kufikia mwisho wa 2018, idadi hii ilikuwa imeshuka kwa zaidi kidogo ya milioni 9. Marufuku ya kusafiri iliyotolewa na Marekani - ambayo ilianza kutekelezwa mnamo

327 keshatajwa.
328 keshatajwa.
329 keshatajwa.
330 keshatajwa.
331 United States Department of Homeland Security, 2018.
332 Connolly, 2019.
333 UNHCR, 2019a.
334 UNHCR, 2018a.
335 keshatajwa.
336 Patriquin, 2018.
337 keshatajwa.
338 keshatajwa.
339 United States Department of State, n.d.

Januari 2017 na hapo awali ilijumuisha raia wa Jamhuri ya Kiislamu ya Iran, Iraq, Libya, Somalia, Sudan, Jamhuri ya Kiarabu ya Syria na Yemen - imechangia kupungua kwa idadi ya wahamiaji na wageni wanaoingia Marekani. Baada ya kupingwa mahakamani, marufuku ya kusafiri iliyorekebishwa, ambayo iliongeza majina zaidi kwenye orodha ya nchi zilizopigwa marufuku, ilianza kutekelezwa mnamo Septemba 2017. Ilijumuisha Jamhuri ya Kiislamu ya Iran, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Watu wa Korea, Jamhuri ya Bolivara ya Venezuela, Chad, Yemen, Somalia na Libya, ingawa baadaye Chad iliondolewa kwenye orodha.[340] Mabadiliko ya kutatanisha zaidi yalianza Juni 2018, wakati Serikali ilianzisha kile kinachoitwa "sera ya kutovumilia kabisa", iliyotumika kwa wahamiaji, pamoja na familia zinazoomba hifadhi zinazovuka mpaka wa Marekani bila nyaraka. Sera hiyo ilikusudiwa kutumika kama kizuio cha adhabu kwa kuvuka mpaka kwa njia isiyo halali,[341] na utekelezaji wake ulisababisha kutengwa kwa zaidi ya watoto 2,600 kutoka kwa wazazi wao,[342] lakini kilio cha umma kilichofuata kililazimisha Serikali kubadilisha mwelekeo haraka. Sera kali za uhamiaji zimejitokeza baada ya usemi ulioenea dhidi ya wahamiaji, ambao umejaribu kuwachora wahamiaji kama hatari na mzigo kwa jamii ya Marekani; imani za njama juu ya uhamiaji pia zimeenea, na hivyo kujenga mazingira ya kutoaminiana na hofu.[343] Kura ya maoni ya mwaka 2018 iligundua kwamba zaidi ya nusu ya raia wa Marekani waliamini kuwa Serikali yao ilikuwa inaficha habari juu ya gharama halisi ya uhamiaji kwa jamii na walipa kodi.[344] Data za hivi karibuni pia zinaonyesha kuwa idadi ya uhalifu wa chuki nchini Marekani iliongezeka katika mwaka wa 2017, huku waathiriwa wengi wakilengwa kwa sababu ya mbari au kabila lao.[345]

**Jinsi sera za uhamiaji zinavyokuwa zuivu zaidi katika ngazi ya kitaifa, ndivyo "miji ya hifadhi" nchini Marekani imejitokeza, ikitoa ulinzi kwa wahamiaji wasio na hati ambao hadhi yao inawaweka katika hatari ya ama kuzuiliwa au kufukuzwa nchini.** Ingawa dhana ya miji ya hifadhi ipo katika sehemu zingine za ulimwengu, inatumiwa sana huko Marekani, ambapo mamlaka nyingi za maeneo mahususi - kama miji, kaunti au Majimbo - zinapinga wazi sheria za kitaifa za uhamiaji[346] na zimepitisha sheria inayolenga kuwalinda wakazi wasio na hati.[347] Katika mwaka wa 2018, California - jimbo lenye watu wengi zaidi nchini Marekani, na lenye idadi kubwa zaidi ya wahamiaji wasio na hati - lilipitisha a sheria zinazotumiwa katika jimbo zima zinazopunguza ushirikiano wa utekelezaji wa sheria za jimbo na mamlaka ya shirikisho kuhusu utekelezaji wa uhamiaji.[348] Miji ya hifadhi imesababisha upinzani kutoka kwa serikali ya shirikisho, ikiwa ni pamoja na juhudi za kuadhibu mamlaka ambazo hazizingatii sheria za uhamiaji za shirikisho.[349]

## Oceania[350]

Katika mwaka wa 2019, karibu wahamiaji wa kimataifa milioni 7.7 kutoka nje ya Oceania walikuwa wakiishi katika ukanda huo. Kama inavyoonyeshwa kwenye kielelezo cha 31 idadi ya wahamiaji waliozaliwa nje ilikuwa inajumuisha watu kutoka Asia (49%) na Ulaya (38%). Katika kipindi chote cha miaka 30 iliyopita, kundi la wahamiaji kutoka Asia limekua, wakati idadi kutoka Ulaya haijabadilika.

---

340 Chishti na Bolter, 2019.

341 OHCHR, 2018b.

342 Mittelstadt, 2018; Shapiro na Sharma, 2018.

343 Gaston na Uscinski, 2018.

344 keshatajwa.

345 FBI, 2018.

346 Duncan na Popp, 2017.

347 Bauder, 2016.

348 Raphelson, Hobson na Bentley, 2018.

349 Chishti na Bolter, 2019.

350 Tazama kiambatisho cha A kwa maelezo juu ya vijenzi vya Oceania.

Kati ya kanda zote sita za ulimwengu, Oceania ilikuwa na idadi ndogo zaidi ya wahamiaji nje ya ukanda wake katika mwaka wa 2019, kwa kiasi fulani ikiakisi jumla ya idadi ndogo ya watu wa ukanda huo, ingawa kulikuwa na ongezeko la idadi yao katika kipindi cha miaka 30 iliyopita. Wengi wa wale waliozaliwa Oceania wanaoishi nje ya ukanda huo waliishi Ulaya na Kaskazini mwa Amerika.

Kielelezo cha 31. Wahamiaji kwenda, ndani ya na kutoka Oceania, 1990–2019




*Chanzo:* UN DESA, 2019a.

*Maelezo:* "Wahamiaji kwenda Oceania" hurejelea wahamiaji wanaoishi katika ukanda huo (yaani Oceania) ambao walizaliwa katika moja ya kanda zingine (kwa mfano Ulaya au Asia). "Wahamiaji ndani ya Oceania" hurejeleaa wahamiaji waliozaliwa katika ukanda huo (yaani Oceania) na wanaoishi nje ya nchi yao ya kuzaliwa, lakini bado katika ukanda wa Oceania. "Wahamiaji kutoka Oceania" hurejelea watu waliozaliwa Oceania ambao walikuwa wanaishi nje ya ukanda huo (kwa mfano, Ulaya au Asia).

Nchi kadhaa za Oceaniya zimepitia mabadiliko makubwa katika wingi wa idadi ya watu katika mwongo uliopita. Mabadiliko makubwa zaidi, kama inavyoonyeshwa kwenye kielelezo cha 32, yalitokea Vanuatu na Visiwa vya Solomon, ambapo idadi ya watu iliongezeka kwa karibu asilimia 30 kati ya 2009 na 2019. Mabadiliko ya idadi ya watu katika nchi zingine pia yalikuwa ni ya kuongezeka.

Kielelezo cha 32. Nchi zilizo na kiwango kikubwa zaidi cha mabadiliko ya idadi ya watu huko Oceania, 2009-2019




*Chanzo:* UN DESA, 2019c.

*Maelezo:* Ni muhimu kutambua kwamba kiwango kikubwa zaidi cha mabadiliko ya idadi ya watu kutoka 2009 hadi 2019 kina uwezekano mkubwa wa kutokea katika nchi zilizo na idadi ndogo ya watu.

Wahamiaji wengi wa kimataifa huko Oceania walikuwa ama wanaishi Australia au New Zealand (kielelezo cha 33). Nchi nyingi katika ukanda huo zina maelezo mafupi ya uhamiaji yaliyopotoshwa, yakiwa na ama asili halisi kubwa au nchi nyingi halisi wanazokwenda wahamiaji. Kwa mfano, Tonga, Samoa na Fiji zote zina idadi kubwa ya wahamaji ikilinganishwa na idadi ya wenyeji wa nchi hizo, na migao ya chini sana ya watu waliozaliwa nje ya nchi. Wahamaji wao walipatikana hasa New Zealand na, kwa kiwango kidogo, huko Australia. Australia na New Zealand zina migao kubwa ya idadi ya watu waliozaliwa nje ya nchi kama sehemu ya jumla ya idadi yao, ikijumuisha karibu asilimia 29 na asilimia 22, mtawalia.

## Kielelezo cha 33. Nchi za wahamiaji za Oceania mnamo 2019




*Chanzo:* UN DESA, 2019a.

*Maelezo ya 1:* Wingi wa idadi ya watu uliotumika kukokotoa asilimia ya wahamiaji na wahamaji unategemea idadi jumla ya wakazi wa nchi hiyo kulingana na UN DESA, ambayo inajumuisha watu waliozaliwa nje ya nchi.

*Maelezo ya 2:* "Mhamiaji" hurejelea wahamiaji walio wazaliwa wa kigeni wanaokaa nchini. "Mhamaji" hurejelea watu waliozaliwa nchini ambao walikuwa wakiishi nje ya nchi yao ya kuzaliwa katika mwaka wa 2019.

Kielelezo cha 34 chenye njia 10 kuu za uhamiaji zinazohusisha nchi za Oceania kinaonyesha mkusanyiko wa harakati za wahamaji kwa muda mrefu, na kinatoa picha ya jinsi mikondo ya uhamiaji imebadilika kuwa idadi kubwa ya watu wa kigeni katika nchi mahususi. Nane kati ya njia 10 kuu za uhamiaji katika ukanda huo zinahusu wahamaji wanaokwenda Australia, na kubwa zaidi ikiwa ya wahamiaji kutoka Uingereza. Njia hizi kubwa pia zinajumuisha wahamiaji kutoka nchi anuwai kutoka nje ya Oceania - pamoja na Uchina, India, Vietnamu na Ufilipino - nyingi ambazo zimepitia ukuaji wa haraka wa idadi ya watu katika miongo ya hivi karibuni. Kulikuwa na uwezekano mkubwa wa wahamiaji kutoka Oceania kuishia ndani ya ukanda huo kuliko katika kanda zingine. Kwa mfano, New Zealand ilikuwa na sehemu kubwa za wahamiaji nje ya nchi, huku idadi kubwa ikiishi Australia.

Kielelezo cha 34. Njia 10 kuu za uhamiaji zinazohusisha nchi za Oceania, 2019




*Chanzo:* UN DESA, 2019a.

*Maelezo:* Njia za uhamiaji zinawakilisha mkusanyiko wa harakati za wahamaji kwa muda mrefu na hutoa picha ya jinsi mikondo ya uhamiaji imebadilika na kuwa idadi kubwa ya wazaliwa wa kigeni katika nchi mahususi walikokwenda.

Katika mwaka wa 2018, Oceania ilikuwa mwenyeji wa wakimbizi na waomba hifadhi zaidi ya 126,000. Australia ilikuwa nchi kubwa zaidi mwenyeji katika ukanda huu, ikifuatwa na Papua New Guinea na New Zealand. Wakimbizi wengi katika nchi hizi walitoka Asia, kama vile Waindonesia walio Papua New Guinea au Waafugani na Wairani walio Australia. Ulimwenguni kote, kulikuwa na karibu wakimbizi na waomba hifadhi 3,000 kutoka nchi za ukanda wa Oceania katika mwaka wa 2018.

Kielelezo cha 35. Idadi ya wakimbizi na waomba hifadhi ndani ya na kutoka nchi za Oceania, 2018




*Chanzo:* UNHCR, n.d.

*Maelezo:* "Waliokaribishwa" hurejelea wale wakimbizi na waomba hifadhi kutoka nchi zingine ambao wanaishi katika nchi inayopokea (upande wa kulia wa kielelezo); "Nje ya nchi" hurejelea wakimbizi na waomba hifadhi wanaotoka kwa nchi hiyo ambao wako nje ya nchi yao ya asili. Kielelezo hicho kinategemea data ya 2018 na inakokotolewa kwa kuchanganya wakimbizi na waomba hifadhi ndani na kutoka nchi zingine.

Ufurushwaji mpya wa ndani huko Oceania katika mwaka wa 2018 ulitokana na majanga, si migogoro (tazama kielelezo cha 36). Papua New Guinea ilirekodi idadi kubwa zaidi ya ufurushwaji wa ndani unaotokana na janga (61,000), ambao ulianzishwa na tetemeko la ardhi. Ufurushwaji mwingine mkubwa unaohusishwa na majanga ulirekodiwa katika Visiwa vya Mariana Kaskazini (14,000), Vanuatu (13,000) na Australia (11,000). Shughuli za volkano zilisababisha kuhamishwa kwa watu wengi Vanuatu, wakati huko Australia, mioto ya msituni ilihusika na ufurushwaji mwingi uliorekodiwa katika mwaka wa 2018. Ikiwa na ufurushwaji mpya 360 unaotokana na mgogoro, Papua New Guinea ilikuwa nchi pekee huko Oceania ambayo ilipitia ufurushwaji uliochochewa na vurugu na migogoro.

Kielelezo cha 36. Nchi 20 kuu za Oceania kulingana na ufurushwaji mpya wa ndani (janga na mgogoro), 2018




*Chanzo:* IDMC, n.d .; UN DESA, 2017.

*Maelezo:* Ufurushwaji mpya unarejelea idadi ya harakati za kufurushwa ambazo zilitokea mwaka wa 2018, si jumla ya idadi ya mkusanyiko wa IDP inayotokana na ufurushwaji unaotokea kwa muda mrefu. Takwimu mpya za ufurushwaji zinajumuisha watu ambao wamefurushwa zaidi ya mara moja na hazilingani na idadi ya watu waliofurushwa katika mwaka husika.

Wingi wa idadi ya watu uliotumika kukokotoa asilimia ya ufurushwaji mpya unaotokana na maafa na migogoro unatokana na jumla ya idadi ya wakazi wa nchi kulingana na makadirio ya idadi ya watu ya mwaka 2017 ya UN DESA, na asilimia inatolewa kwa madhumuni ya kutoa ufafanuzi tu.

## Sifa muhimu na maendeleo huko Oceania

**Uhamiaji halisi wa kila mwaka kwenda New Zealand na Australia umepungua.** Katika mwaka uliomalizika Novemba 2018, New Zealand ilikuwa na uhamiaji halisi wa zaidi kidogo ya 51,000, chini kidogo kutoka karibu 52,000 katika mwaka unaoishia Desemba 2017;[351] makadirio ya uhamiaji halisi wa nje ya Australia katika mwaka unaoishia Juni 2018 yalikuwa watu 237,200, yakishuka kwa asilimia 10 kutoka mwaka unaoishia Juni 2017.[352] Kanda ambazo wahamiaji kwenda Australia wamezaliwa zimebadilika katika miaka ya hivi karibuni; tangu 2014, idadi kubwa zaidi ya wahamiaji wametoka Asia tofauti na maeneo ya asili ya jadi, pamoja na Oceania na Ulaya.[353] Kwa mfano, idadi ya wahamiaji wanaowasili kutoka Asia Kusini na Kati sasa imewazidi wale kutoka Kaskazini-Magharibi mwa Ulaya na Oceania.[354] Katika mwaka wa 2019, asilimia 30 ya idadi ya watu wa Australia walikuwa waliozaliwa nje ya nchi, ikilinganishwa na asilimia 21.3 nchini Canada na asilimia 15.4 nchini Marekani.[355] Uingereza imekuwa nchi asili ya wahamiaji nchini New Zealand kwa miongo kadhaa, kukiwa na ongezeko kubwa la idadi ya wahamiaji Waesia, hasa kutoka Uchina na India, na pia idadi kubwa ya

351 Stats, New Zealand, 2019.
352 Australian Bureau of Statistics, 2019.
353 keshatajwa.
354 keshatajwa.
355 UN DESA, 2019a.

watu kutoka Visiwa vya Pacific, pamoja na Fiji, Samoa na Tonga.[356] Katika mwaka wa 2017, idadi ya watu wa New Zealand waliozaliwa nje ya nchi ilikuwa karibu asilimia 23 ya idadi ya watu wote wa nchi hiyo.[357] Katika nchi za Australia na New Zealand, kuna idadi kubwa ya wafanyikazi wa muda. Zaidi ya watu 209,000 walipewa viza za kazi huko New Zealand mnamo 2016/2017, ongezeko la asilimia 9 kutoka 2015/2016.[358] Nchi kubwa zaidi ya asili ya wafanyikazi wahamiaji wa muda huko New Zealand ilikuwa India mnamo 2016/2017, ikifuatwa na Uingereza, Uchina na Ujerumani.[359] Nchi zote mbili pia huvutia idadi kubwa ya wanafunzi wa kimataifa. Idadi ya wanafunzi wa kimataifa imeongezeka tangu mwaka wa 2012 huko Australia, na kufikia idadi kubwa zaidi ya karibu 700,000 mnamo 2018,[360] wakati kulikuwa na zaidi ya wanafunzi 91,000 wenye viza nchini New Zealand katika mwaka wa 2016/2017, huku wanafunzi wengi hasa wakitoka Uchina na India.[361]

**Australia na New Zealand hushiriki katika kutoa makazi mapya ya wakimbizi.** Programu ya kutoa makazi mapya ya Australia ni ya tatu kwa ukubwa ulimwenguni, ikiwa na karibu wakimbizi 13,000 waliopewa makazi mapya nchini humo katika mwaka wa 2018.[362] Chini ya Mpango wa Kibinadamu wa Australia, nafasi 12,000 zaidi za kibinadamu zilitolewa katika mwaka wa 2015 kwa watu waliofurushwa na migogoro katika Jamhuri ya Kiarabu ya Syria na Iraq.[363] Idadi ya nafasi katika Mpango wa Kibinadamu wa Australia ziliongezeka hadi 16,250 mnamo 2017/2018 na zilitarajiwa kuongezeka zaidi hadi nafasi 18,750 kutoka 2018 hadi 2019.[364] Sera ya Australia ni kuhamisha wale wanaofika kwa njia zisizo halali kwa mashua kama waomba hifadhi hadi kwenye vituo vya kuandikishwa vilivyo mbali na pwani kwenye Kisiwa cha Manus huko Papua New Guinea na Nauru.[365] Mnamo Julai 2013, Australia pia ilitangaza kuwa watu wote wanaofika kwa mashua na wanaopatikana kuwa wanahitaji ulinzi wa kimataifa hawatapewa makazi mapya Australia.[366] Kama sehemu ya mpango wa kutoa makazi mapya unaohusisha nchi mbili yaani Marekani na Australia, Marekani ilikubali kutoa makazi mapya kwa hadi wakimbizi 1,200 kutoka Nauru na Kisiwa cha Manus cha Papua New Guinea.[367] Kufikia mapema 2019, ni karibu wakimbizi 500 pekee kutoka vituo hivi vya uandikishaji vilivyo mbali na pwani waliokuwa wamepewa makazi mapya nchini Marekani chini ya mpango huo.[368] Wakati huo huo, karibu watu 1,000 ya wale waliohamishiwa hadi Kisiwa cha Manus na Nauru wanabaki huko, baadhi yao wakiwa wale waliokuwa wana matatizo makali ya afya ya mwili na akili.[369] New Zealand pia ni nchi inayotoa makazi mapya kwa wakimbizi, ikitoa makazi kwa wakimbizi 1,000 kila mwaka kupitia Programu yake ya Mgawo wa Wakimbizi.[370] Hii pia inajumuisha nafasi 250 zilizotengwa mahususi kwa wakimbizi wa Syria katika miaka ya

356 keshatajwa.

357 keshatajwa.

358 New Zealand Ministry of Business, Innovation and Employment, 2018.

359 keshatajwa.

360 Australian Department of Education and Training, 2018.

361 New Zealand Ministry of Business, Innovation and Employment, 2018.

362 UNHCR, 2019a.

363 Australian Department of Social Services, 2019.

364 keshatajwa.

365 Refugee Council of Australia, 2017.

366 keshatajwa.

367 Andrew and Renata Kaldor Centre for International Refugee Law, 2019.

368 Davidson, 2019.

369 UNHCR, 2019e.

370 New Zealand Immigration, n.d.

2016/2017 na 2017/2018.[371] New Zealand pia imeanzisha mgawo wa ziada wa nafasi 300 kila mwaka ambao unaruhusu wanafamilia wa wakimbizi huko New Zealand kuomba Makazi ya Kudumu.[372]

**Changamoto za kiuchumi hushawishi uhamaji kutoka nchi za Kisiwa cha Pacific.** Visiwa vingi vya Pacific vinaendelea kupata changamoto zisizoisha zinazohusiana na umasikini na ukosefu wa usawa. Ukuaji wa uchumi wa Visiwa hivi pia umezuiliwa na umbali wake au umbali mkubwa kati yavyo na masoko makubwa, uhaba wa rasilimali asili na uchumi finyu.[373] Zaidi ya hayo, ukanda huu mdogo unapitia "ongezeko ghafla la vijana", huku asilimia 70 ya idadi ya watu katika Visiwa vya Solomon, kwa mfano, wakiwa hawajatimiza umri wa miaka 34.[374] Matokeo yake ni idadi kubwa ya vijana wanaohangaika na ukosefu wa ajira, na kusababisha kiwango cha juu cha uhamaji wa wafanyikazi. Tangu mwaka 2007, mpango wa uhamiaji wa wafanyikazi kwa msimu umesaidia kupunguza uhaba wa wafanyikazi katika Visiwa vya Pacific, na kuanzishwa kwa mpango wa Mwajiri wa Msimu Anayetambuliwa wa New Zealand na Mpango wa Wafanyikazi wa Msimu wa Australia mnamo 2012, iliyolenga kukidhi mahitaji ya wafanyikazi, hasa katika tasnia za kilimo cha bustani na kilimo cha mizabibu.[375] Zaidi ya watu 9,600 kutoka Visiwa vya Pacific walipewa viza katika mpango wa Mwajiri wa Msimu Anayetambuliwa wa New Zealand wakati wa msimu wa 2017/2018 na zaidi ya 8,000 katika Mpango wa Wafanyikazi wa Msimu wa Australia wakati wa msimu huo huo.[376] Katika mwaka wa 2018, mpango mpya wa kazi, Mpango wa Kazi wa Pacific (PLS), ulianzishwa ili kuziba mapengo katika kazi zinazohitaji ujuzi wa chini na ujuzi kiasi huko vijijini na katika kanda za Australia.[377] Muhimu zaidi ni kuwa wakati Australia na New Zealand zikiendelea kuwa sehemu kuu wanakokwenda wahamiaji wa kazi kutoka Visiwa vya Pacific, uhamaji wa wafanyikazi kutoka Visiwa hivi umekuwa anuwai, huku Wafiji na Watonga, kwa mfano, wakizidi kuhamia nchi kama Japani.[378]

**Mabadiliko ya kimazingira na uharibifu pia ni kati ya mambo kadhaa yanayowashawishi wakazi wengi wa Visiwa vya Pacific kuhama.** Ukanda wa Pacific uko katika hali ya kuweza kudhuriwa kwa urahisi na hatari za asili, baadhi zikiwa zile zinazohusishwa na mabadiliko ya tabianchi. Hali ya kuweza kudhuriwa na tabianchi na uhamiaji unaohusiana na hilo, ufurushwaji na uhamishaji uliopangwa hadi kwenye makazi mapya hutofautiana kati ya nchi na maeneo ya Kisiwa cha Pacific. Nusu ya idadi ya watu huko Kiribati na Tuvalu wanaishi katika maeneo ya mjini yenye msongamano kwenye visiwa vya matumbawe vyenye vishoroba vyembamba na upatikanaji mdogo wa maji na ardhi.[379] Ongezeko la kiwango cha usawa wa bahari unaopanda, kuingiliwa na maji ya chumvi na ukame ni mambo muhimu, kati ya mengine, yanayoathiri maamuzi ya watu kuhama katika ukanda huo, ndani na kimataifa.[380] Katika muktadha huu, pia kuna mjadala unaokua juu ya haja ya uhamishwaji uliopangwa wa vikundi na jamii.[381] Kwa mfano Kiribati, moja ya Mataifa yanayoweza kudhuriwa zaidi na athari za mabadiliko ya tabianchi, iliendeleza sera ya "Uhamiaji wenye Heshima" kama

371 UNHCR, 2018b.
372 keshatajwa.
373 Benki ya Dunia, 2019b.
374 Vanderwey, 2019.
375 ILO, 2019.
376 keshatajwa.
377 Australian Department of Foreign Affairs and Trade, 2019.
378 keshatajwa.
379 Curtain et al., 2016.
380 ESCAP, 2015.
381 Tazama, kwa mfano, Chuo Kikuu cha Georgetown, n.d., kwa rasilimali anuwai juu ya uhamishwaji hadi makao mapya uliopangwa.

hatua ya kukabiliana na hali ya muda mrefu.[382] Sera hii inakusudia kuwezesha uhamiaji wa kudumu na wa muda wa wafanyikazi kwa hiari kama njia ya kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi.[383] Wakati huo huo, Serikali ya Fiji imekuwa ikihamisha watu kutoka vijiji kadhaa vya pwani ambavyo vimetambuliwa kuwa vinaweza kudhuriwa kwa urahisi na athari za mabadiliko ya mazingira na uharibifu.[384]

## Hitimisho

Sura hii imetegemea takwimu na habari anuwai ili kutoa muhtasari wa kikanda juu ya uhamiaji wa kimataifa ulimwenguni, msisitizo ukiwa kwenye mabadiliko yanayotokea katika miaka ya kalenda ya 2017 na 2018 (na kutumia nyenzo zilizochapishwa hadi mwisho wa Juni 2019). Sura hii ilijikita katika kanda sita pana za ulimwengu (Afrika, Asia, Ulaya, Amerika ya Kusini na Karibiani, Kaskazini mwa Amerika na Oceania), na ilitoa majadiliano ya maswala muhimu na vilevile maendeleo ya hivi karibuni katika ngazi ya ukanda mdogo.

Kwa jumla, na kama inavyoonyeshwa na grafu zilizowasilishwa katika ngazi ya kikanda, kuna vipengele wazi vya kijiografia kwa uhamiaji na ufurushwaji. Mapitio ya haraka ya takwimu zilizo katika sura hii yanaonyesha dhahiri tofauti kubwa katika mikondo ya uhamiaji kati ya kanda: uhamiaji barani Afrika umefanyika kimsingi ndani ya ukanda (kutoka nchi moja ya Kiafrika kwenda nchi nyingine) na uhamiaji pia ukitokea kwenda kwenye kanda zingine za ulimwengu (kutoka nchi za Afrika hadi kwa nchi zisizo za Kiafrika), wakati ambapo katika Amerika ya Kusini na Karibiani, uhamiaji unatawaliwa na uhamaji kwenda kanda zingine za ulimwengu, hasa Kaskazini mwa Amerika, huku uhamiaji wa ndani ya ukanda ukiwa na nafasi ndogo kabisa.

Kuongezwa kwa grafu mbili za kikanda katika toleo hili la Ripoti ya Uhamiaji Duniani - moja juu ya mabadiliko ya idadi ya watu kwa zaidi ya mwongo mmoja na moja juu ya ufurushwaji mpya wa ndani wa 2018 - kunaangazia na kunaimarisha mienendo mingine ya kuvutia katika kiwango cha ukanda. Kwa mfano, tunaweza kuona kwamba, wakati mabadiliko makubwa ya kiwango cha idadi ya watu katika mwongo uliopita yamekuwa zaidi katika ukuaji, sehemu za Ulaya zimeshuhudia kupungua sana kwa idadi ya watu; hili ni tukio la kipekee ulimwenguni, kwani hakuna ukanda mwingine unaopata matokeo kama haya. Hali hii isiyo ya kawaida ya kupungua kwa idadi ya watu, mienendo ya uhamiaji ya muda mrefu, watu wanaozeeka na uhasama unaolekezwa kwa uhamiaji huibua maswali kadhaa ya sera kimkakati ambayo huenda baadhi ya nchi za Ulaya zitakabiliana nayo kwa miaka mingi ijayo. Wakati huo huo, changamoto za idadi ya watu zinashughulikiwa katika sehemu zingine za ulimwengu, pamoja na katika nchi kadhaa za Asia ya Kaskazini, ambazo zinakadiria tena mbinu zao za uhamiaji kwa kuzingatia masoko ya wafanyikazi, kukidhi mahitaji muhimu ya kikazi na kisekta na kujiandaa zaidi kwa populesheni inayozeeka. Kuongezwa kwa grafu mpya za ufurushwaji wa ndani kunazingatia tofauti kubwa kati ya ufurushwaji unaohusiana na migogoro na ufurushwaji unaohusana na majanga duniani, huku tofauti kubwa zikionekana katika kiwango cha kikanda.

Katika kiwango cha ukanda mdogo, tunaweza kuona kuwa sifa muhimu zinaweza kwa kiasi kikubwa kubaki zilivyo mwaka hadi mwaka, huku mabadiliko ya ongezeko tu yakionekana. Hata hivyo, ni katika uchunguzi wa maendeleo ya hivi majuzi ambapo tunaweza kuona mabadiliko makubwa yakitokea katika maeneo mengine ya dunia. Kwa kiasi fulani, mabadiliko haya yanatokana na "matukio" makubwa ya uhamiaji, kama vile mtiririko mkubwa wa watu kutoka Jamuhuri ya Bolivaria ya Venezuela, au ufurushwaji mkubwa wa wakimbizi

382 Farbotko, 2018; Curtain na Dornan, 2019.

383 keshatajwa.

384 keshatajwa.

wa Rohingya kutoka Myanmar. Tunaona pia mabadiliko yakitokea kwenye utawala wa uhamiaji wakati kanda ndogo zinaposhuhudia mabadiliko katika mikondo ya uhamiaji na mabadiliko ya kimsingi ya idadi ya watu. Huko Asia Kaskazini, kwa mfano, Uchina ilianzisha shirika lake la kwanza la uhamiaji, ikileta pamoja majukumu kutoka kwa mashirika kadhaa kuwa chini ya mamlaka moja iliyounganishwa. Wakati huo huo, Jamhuri ya Korea ilipata wageni wengi wanaoomba hifadhi kutoka Mashariki ya Kati ambao hawajaonekana hapo awali, na kusababisha mjadala mkali wa umma juu ya sera ya maswala yanayohusiana na hayo.

Tofauti na uchangamano wa kikanda, pamoja na maendeleo ya hivi karibuni, hutoa mtazamo muhimu wa kuelewa uhamiaji. Mara nyingi, tunasoma na kusikia juu ya uhamiaji kutoka kwa mtazamo wa kitaifa, hasa katika nyakati za hivi karibuni ambapo umeelezwa kama suala nyeti (hasi) la ndani na la kisiasa. Lakini lengo hili kuu linaweza kuficha ukweli kwamba mikondo na michakato ya uhamiaji imeunganishwa kwa karibu sana na jiografia, na kwamba sifa muhimu za kikanda zilizokuzwa kwa miongo kadhaa, ikiwa si karne, zinaendelea kupewa dhima kubwa kuhusu jinsi na wapi watu wanahamia kimataifa. Utambuzi mkubwa wa mikondo ya uhamiaji ya kikanda na ukanda mdogo, tofauti na uchangamano unaweza kusaidia katika kuunda majibu ya sera ya kimkakati na kiuendelevu. Kiambatisho A. Idara ya Umoja wa Mataifa ya Uchumi na Masuala ya Kijamii: Kanda na Kanda Ndogo

## Kiambatisho A. Idara ya Umoja wa Mataifa ya Uchumi na Masuala ya Kijamii: Kanda na Kanda Ndogo

Tafadhali kumbuka kwamba jedwali hili linaonyesha kanda na kanda ndogo za kijiografia kulingana na UN DESA na halidokezi uidhinishaji au kukubalika rasmi na IOM.

| Afrika | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **Mashariki mwa Afrika[a]** | **Afrika ya Katikati[b]** | **Kaskazini mwa Afrika[c]** | **Kusini mwa Afrika[d]** | **Magharibi mwa Afrika[e]** |
| Burundi | Angola | Algeria | Afrika Kusini | Benin |
| Comoros | Cameroon | Libya | Botswana | Burkina Faso |
| Djibouti | Chadi | Misri | Eswatini | Cabo Verde |
| Eritrea | Equatorial Guinea | Moroko | Lesotho | Côte d’Ivoire |
| Ethiopia | Gabon | Sudan | Namibia | Gambia |
| Jamhuri ya Muungano wa | Jamhuri ya Afrika ya Kati | Tunisia | | Ghana |
| Kenya | Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo | | | Guinea |
| Madagaska | Kongo | | | Guinea-Bissau |
| Malawi | São Tomé na Príncipe | | | Liberia |
| Mauritius | | | | Mali |
| Mayotte | | | | Mauritania |
| Msumbiji | | | | Niger |
| Réunion | | | | Nigeria |
| Rwanda | | | | Saint Helena |
| Somalia | | | | Senegali |
| Sudan Kusini | | | | Sierra Leone |
| Uganda | | | | Togo |
| Ushelisheli | | | | |
| Zambia | | | | |
| Zimbabwe | | | | |

a Mashariki mwa Afrika imejumuishwa na ukanda mdogo wa Afrika ya Kusini katika sura hiyo, ingawa nchi / wilaya / maeneo yaliyomo hubaki vile vile.

b Ukanda huu mdogo umepewa jina jipya la “Afrika ya Kati” katika sura hiyo na kuunganishwa na Magharibi mwa Afrika.

c Ukanda huu mdogo umepewa jina jipya la “Afrika Kaskazini”.

d Ukanda huu mdogo umeunganishwa na Mashariki mwa Afrika.

e Ukanda huu mdogo umepewa jina jipya la “Afrika Magharibi” na umeunganishwa na Afrika ya Kati (UN DESA Afrika ya Katikati) katika sura hiyo.

| Asia | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **Asia ya Kati** | **Mashariki mwa Asia** | **Asia ya Kusini-Mashariki[f]** | **Kusini mwa Asia** | **Magharibi mwa Asia[g]** |
| Kazakhstan | Jamhuri ya Kidemokrasia ya Watu wa Korea | Brunei Darussalam | Afuganistani | Armenia |
| Kyrgyzstan | Jamhuri ya Korea | Cambodia | Bangladeshi | Azerbaijan |
| Tajikistan | Japani | Indonesia | Bhutan | Bahrain |
| Turkmenistan | Mongolia | Jamhuri ya Kidemokrasia ya Watu wa Lao | India | Cyprus |
| Uzbekistan | Uchina | Malaysia | Iran (Jamhuri ya Kiislamu ya) | Georgia |
| | Uchina, Ukanda Maalum wa Utawala wa Hong Kong | Myanmar | Maldives | Iraq |
| | Uchina, Ukanda Maalum wa Utawala wa Macao | Singapore | Nepal | Israeli |
| | | Tailandi | Pakistani | Jamhuri ya Kiarabu ya Syria |
| | | Timor-Leste | Sri Lanka | Jordan |
| | | Ufilipino | | Kuwait |
| | | Vietnamu | | Lebanon |
| | | | | Milki za Kiarabu |
| | | | | Oman |
| | | | | Qatar |
| | | | | Saudi Arabia |
| | | | | Uturuki |
| | | | | Yemen |

f Ukanda huu mdogo umepewa jina jipya la “Kusini-Mashariki mwa Asia”.

g Ukanda huu mdogo umepewa jina jipya la “Mashariki ya Kati”.

| Ulaya[h] | | | |
|---|---|---|---|
| **Mashariki mwa Ulaya[i]** | **Kaskazini mwa Ulaya** | **Kusini mwa Ulaya** | **Magharibi mwa Ulaya** |
| Belaru | Denmark | Albania | Austria |
| Bulgaria | Estonia | Andorra | Liechtenstein |
| Czechia | Iceland | Bosnia na Herzegovina | Luxembourg |
| Hungary | Ireland | Croatia | Monaco |
| Jamhuri ya Moldova | Isle of Man | Gibraltar | Ubelgiji |
| Poland | Latvia | Holy See | Ufaransa |
| Romania | Lithuania | Italia | Uholanzi |
| Shirikisho la Urusi | Norway | Malta | Ujerumani |
| Slovakia | Ufini | Montenegro | Uswisi |
| Ukraine | Uingereza ya Great Britain na Ireland ya Kaskazini | Macedonia Kaskazini | |
| | Uswidi | San Marino | |
| | Visiwa vya Channel | Serbia | |
| | Visiwa vya Faroe | Slovenia | |
| | | Ugiriki | |
| | | Uhispania | |
| | | Ureno | |

h Huenda baadhi ya nchi katika ukanda huu mdogo, hasa wanachama wa Umoja wa Ulaya, zilijumuishwa katika mazungumzo ya Kusini-Mashariki na Mashariki mwa Ulaya, pamoja na majadiliano ya ukanda mdogo wa Kaskazini, Magharibi, na Kusini mwa Ulaya yaliyo katika sura hiyo.

i Kaskazini, Magharibi na Kusini mwa Ulaya zimeunganishwa katika sura hiyo, ukiondoa nchi zifuatazo zilizo Kusini mwa Ulaya: Albania, Bosnia na Herzegovina, Croatia, Montenegro, Serbia na Macedonia ya Kaskazini, ambazo zimejumuishwa katika Kusini-Mashariki mwa Ulaya katika sura hiyo, chini ya ukanda mdogo wa Kusini-Mashariki na Mashariki mwa Ulaya.

| Amerika ya Kusini na Karibiani | | |
|---|---|---|
| **Karibiani** | **America ya Kati**[j] | **Amerika Kusini** |
| Anguilla | Belize | Argentina |
| Antigua na Barbuda | Costa Rica | Bolivia (Taifa la) |
| Aruba | El Salvador | Brazil |
| Bahamas | Guatemala | Chile |
| Barbados | Honduras | Colombia |
| Bonaire, Sint Eustatius na Saba | Meksiko | Ecuador |
| Cayman Islands | Nicaragua | French Guiana |
| Cuba | Panama | Guyana |
| Curaçao | | Paraguay |
| Dominika | | Peru |
| Grenada | | Suriname |
| Guadeloupe | | Uruguay |
| Haiti | | (Jamhuri ya Bolivaria ya) Venezuela |
| Jamaika | | Visiwa vya Falklands (Malvinas) |
| Jamhuri ya Dominika | | |
| Martinique | | |
| Montserrat | | |
| Puerto Rico | | |
| Saint Kitts na Nevis | | |
| Saint Lusia | | |
| Saint Vincent na Grenadines | | |
| Sint Maarten (sehemu ya Udachi) | | |
| Trinidad na Tobago | | |
| United States Virgin Islands | | |
| Visiwa vya Cayman | | |
| Visiwa vya Turks na Caicos | | |

j Ukanda mdogo "Amerika ya Kati" imeunganishwa na Meksiko na Karibiani katika sura hii.

| Northern America |
|---|
| Bermuda |
| Canada |
| Greenland |
| Marekani |
| Saint Pierre na Miquelon |

| Oceania | | | |
|---|---|---|---|
| **Australia na New Zealand** | **Melanesia** | **Micronesia** | **Polynesia** |
| Australia | Fiji | Guam | French Polynesia |
| New Zealand | New Caledonia | Kiribati | Niue |
| | Papua New Guinea | Micronesia (Nchi za Shirikisho la) | Samoa |
| | Vanuatu | Nauru | Samoa ya Amerika |
| | Visiwa vya Solomon | Palau | Tokelau |
| | | Visiwa vya Mariana Kaskazini | Tonga |
| | | Visiwa vya Marshall | Tuvalu |
| | | | Visiwa vya Cook |
| | | | Visiwa vya Wallis na Futuna |

**Simulizi:**

| Ukanda |
|---|
| **Ukanda mdogo**[i] |
| Nchi/wilaya/eneo[ii,iii] |

*Maelezo:* Kwa mbinu pamoja na maelezo ya kiufafanuzi, angalia International Migrant Stock 2019: Maelezo, yanapatikana katika www.un.org/en/development/desa/population/migration/data/estimates2/docs/MigrationStockDocumentation_2019.pdf.

i Huenda kanda ndogo zilizotumiwa katika sura hii zikatofautiana na zile zinazotumiwa na Kitengo cha Takwimu cha UN DESA ama kwa jina, au kwa nchi / wilaya / maeneo yaliyojumuishwa humo.

ii "Majina ya nchi au maeneo hurejelea vifupisho vyake vinavyotumiwa katika shughuli za kila siku za Umoja wa Mataifa na si majina yao rasmi kama yanavyotumiwa katika hati rasmi. Majina haya yanatokana na Hifadhidata ya Istilahi za Umoja wa Mataifa (UNTERM), ambayo inaweza kupatikana katika: https://unterm.un.org/UNTERM/portal/welcome Majina yaliyotumiwa na uwasilishaji wa nyenzo kwenye tovuti hii haumaanishi utoaji wa maoni yoyote yale upande wa Sekretarieti ya Umoja wa Mataifa [au Shirika la Kimataifa la Uhamiaji (IOM)] kuhusu hali ya kisheria ya nchi yoyote, taifa, jiji au eneo au mamlaka yake, au kuhusu uwekaji wa ukomo wa mipaka yake. " Kwa habari zaidi, tazama https://unstats.un.org/unsd/methodology/m49/.

iii Vitu vilivyojumuishwa katika jedwali hili, ambavyo sura ya awali imetegemea, ni pamoja na nchi, na pia wilaya, maeneo na kanda maalum za kiutawala. Tafadhali kumbuka kuwa jedwali hili halijakusudiwa kuwa kamilifu.

# Marejeleo*


ACAPS

2018 *Migration in West and North Africa: Scenarios*. Inapatikana katika www.mixedmigration.org/wp-content/uploads/2018/12/20181130_acaps_mmc_scenarios_report_migration_in_west_and_north_africa_update_2.pdf.

Acosta, D.

2016 *Free Movement in South America: The Emergence of an Alternative Model?* Migration Policy Institute, 23 February. Inapatikana katika www.migrationpolicy.org/article/free-movement-south-america-emergence-alternative-model.

Adepoju, A.

2016 *Migration Dynamics, Refugees and Internally Displaced Persons in Africa*. United Nations Academic Impact (UNAI), 20 September. Inapatikana katika https://academicimpact.un.org/content/migration-dynamicsrefugees-and-internally-displaced-persons-africa.

African Union

2019 Refugees, Returnees and Internally Displaced Persons in Africa at center of 32nd AU Summit Opening of the 37th Ordinary Session of the PRC, Addis Ababa. Inapatikana katika https://au.int/en/pressreleases/20190115/refugees-returnees-and-internally-displaced-persons-africa-center-32nd-au.

Aimsiranun, U.

2018 Regional Approaches to Labour Migration: Mercosur and Asean in Comparative Perspective. Proceedings of New York International Business and Social Science Research Conference, New York. Inapatikana katika www.aabl.com.au/aablConference/public/documents/pdf/2018_11_25_05_17_37_NYIBSRC-216_Full_Paper.pdf.

Altai Consulting na International Organization for Migration (IOM)

